# NAFASI YA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA RIWAYA TEULE: *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA *MKAMANDUME*

**TASNIFU**

**YA**

**KIBUI SARABINA KARIMI**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI, SHULE YA FANI NA SAYANSI YA JAMII YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

**SEPTEMBA, 2022**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine.

Kibui Sarabina Karimi

(C50/CE/26001/2014)

Sahihi…………………… Tarehe……………………

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Prof. Kitula King'ei

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Sahihi……………………Tarehe……………………

## SHUKRANI

Ninamshehenezea Mola shukrani za dhati kwa neema na rehema zake. Amekuwa mwaminifu na kuniwezesha kukamilisha kazi hii.

Namshukuru msimamizi wangu Prof.King’ei kwa kunielekeza, kunishauri, kunirekebisha na kunitia ari ya kufanya kazi hii. Msaada wake umekuwa dira muhimu sana katika ufanisi wa kazi hii. Aidha, naishukuru Idara ya Kiswahili kwa kujitolea kunipa maarifa katika masomo yote. Asanteni sana.

Nawashukuru wazazi wangu; Mamangu Margaret Kibui na marehemu babangu David Kibui kwa kunitunza na kunielimisha. Pia, ndugu zangu Lawrence Muriithi Kibui, Lydia Mutitu Kibui na marehemu Clement Murage Kibui kwa kunifaa kwa hali na mali. Bwanangu  George Kanyoni Kibanya aliyenihimiza kila siku, kunitia moyo wa kuendelea na masomo na kunisaidia kwa hali na mali. Msaada wake hautasahaulika.Mwanangu Ann Yvonne Wanjiku aliyevumilia na kunipa moyo wa kuendelea na safari hii hadi tamati. Subira  yake ilinifaa sana. Marafiki zangu pia walionipa motisha wa kusoma na maombi yao : Lucy Wairimu,Charity Gichugu , Ephraim Muiga Gathogo,Padri Edward Nyamu,  na  wengineo. Mungu awabariki.

Mwisho, nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulianza safari hii pamoja na tumekuwa tukishirikiana katika kufanya kazi ya ziada, mawasilisho na mijadala. Esther Kasinga,Chiringa Mwanyiro, George Kausi na Lilian Gitau,  miongoni mwa wengine. Mchango wenu ni muhimu sana.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa marehemu babangu David Kibui Njuki pamoja na marehemu kakangu Clement Murage Kibui.Mungu mwenye huruma aendelee kuwapa pumziko lisilokwisha na kuwaangazia mwanga wake milele. Moyoni mwangu nimewaweka hadi tutakapokutana tena. Amina.

## YALIYOMO


YALIYOMO ..................................................V

VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA .................................................. IX

MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU..................................................X

IKISIRI .................................................. XI

ABSTRACT .................................................. XII

SURA YA KWANZA .................................................. 1

UTANGULIZI WA UTAFITI .................................................. 1

1.0 UTANGULIZI .................................................. 1

1.1. USULI WA MADA. .................................................. 1

1.2 SUALA LA UTAFITI.................................................. 7

1.4. MALENGO YA UTAFITI .................................................. 8

1.3 .MASWALI YA UTAFITI.................................................. 8

1.5. SABABU ZA KUCHAGUA MADA .................................................. 9

1.6. UPEO NA MIPAKA. .................................................. 12

1.7. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA. .................................................. 14

1.8. MISINGI YA NADHARIA .................................................. 29

1.8.1 MIHIMILI YA NADHARIA .................................................. 32

1.9.1 MUUNDO WA UTAFITI .................................................. 33

1.9.2 MAHALI PA UTAFITI .................................................. 33

1.9.3 UTEUZI WA SAMPULI. .................................................. 34

1.9.4 UKUSANYAJI WA DATA. .................................................. 35

1.9.5 UCHANGANUZI WA DATA .................................................. 37

1.9.6. UWASILISHAJI WA MATOKEO .................... 38
1.10 HITIMISHO .................... 38
SURA YA PILI .................... 39

MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUFANIKISHA

MAUDHUI YA RIWAYA ZA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA *MKAMANDUME*....... 39

2.0 UTANGULIZI .................... 39
2.2. UHUSIKA NA WAHUSIKA KATIKA FASIHI. .................... 40
2.2.1. DHANA YA UHUSIKA .................... 40
2.2.2 DHANA WA WAHUSIKA. .................... 41
2.2.3. DHANA YA USAWIRI .................... 44
2.2.4. WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA RIWAYA. .................... 45
2.2.5.0 MCHANGO WA MHUSIKA MATUKO WEYE KATIKA RIWAYA YA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* .................... 52
2.2.5.1. MHUSIKA MATUKO WEYE ALIVYOSAWIRIWA KAMA .................... 52
MWENDAWAZIMU .................... 52
2.2.5.2 MCHANGO WA MATUKO WEYE KATIKA KUKUZA MAUDHUI .................... 55
2.2.5.2.1 VITA DHIDI YA UDHALIMU. .................... 55
2.2.5.2.2 UKOMBOZI .................... 58
2.2.5.2.3. UONGOZI MBAYA. .................... 62
2.2.6.0 UHAKIKI WA MCHANGO WA MHUSIKA BILAL KATIKA RIWAYA YA *MKAMANDUME*. .................... 68
2.2.6.1 KUSAWIRIWA KWA BILAL KAMA MWENDAWAZIMU .................... 68
2.2.6.2 MCHANGO WA BILAL KATIKA KUKUZA MAUDHUI .................... 71
2.2.6.2.1 UONGOZI MBAYA .................... 71
2.2.6.2.2 ELIMU .................... 73
2.2.6.2.3 DHULUMA .................... 83
2.2.7.0 HITIMISHO .................... 86
SURA YA TATU .................... 88

UHAKIKI WA MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUKUZA MBINU ZA UANDISHI ........ 88
3.0 UTANGULIZI ........ 88
3.1. MCHANGO WA MATUKO WEYE KATIKA MBINU ZA UANDISHI ........ 88
3.1.1 BALAGHA ........ 88
3.1.2 KINAYA ........ 89
3.1.3.KEJELI ........ 91
3.1.4 UCHESHI ........ 92
3.1.5.TASWIRA ........ 94
3.2 MCHANGO WA BILAL KATIKA KUENDELEZA MBINU ZA UANDISHI ........ 95
3.2.1. TASWIRA ........ 95
3.2.2 KEJELI ........ 96
3.2.3 MBINU REJESHI ........ 98
3.2.4 DAYALOJIA ........ 99
3.2.5. BALAGHA ........ 101
3.3. HITIMISHO ........ 103
SURA YA NNE ........ 104
UCHUNGUZI WA MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUENDELEZA DHAMIRA YA MWANDISHI ........ 104
4.0 UTANGULIZI ........ 104
4.1.0 JINSI MHUSIKA MATUKO WEYE ANAVYOENDELEZA DHAMIRA YA MWANDISHI ........ 105
4.1.1 MAONEVU DHIDI YA WANYONGE ........ 105
4.1.2 KUPIGANIA HAKI ........ 106
4.2.0 MCHANGO WA BILAL KATIKA DHAMIRA YA MWANDISHI ........ 106
4.2.2 ATHARI ZA UONGOZI MBAYA ........ 107
4.2.3 KUKASHIFU UJINGA ........ 107

4.3.0 HITIMISHO ........................................................................................................108
SURA YA TANO.........................................................................................................109

MUHTASARI, MATOKEO,MAPENDEKEZO NA HITIMISHO.............................109

5.0 UTANGULIZI.........................................................................................................109
5.1 MUHTASARI WA TASNIFU. ..........................................................................111
5.2 MATOKEO YA UTAFITI......................................................................................112
5.3 MCHANGO WA UTAFITI ....................................................................................122
5.4 MATATIZO YA UTAFITI.......................................................................................123
5.5 MAPENDEKEZO YA UTAFITI ..........................................................................123
5.5.1. MAPENDEKEZO KWA WATAFITI WENGINE ...........................................123
5.5.2. MAPENDEKEZO KWA SERIKALI. ................................................................124
5.5.3. MAPENDEKEZO KWA JAMII. ........................................................................124
MAREJELEO..............................................................................................................125

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

DSM111: The third edition of the American Psychiatric Association's Diagnostic and Statistical Manual of Mental Disorders.

TATAKI :Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.

TAKILUKI :Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.

T.Y :Tafsiri Yangu.

Uk: Ukurasa

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

**Wahusika:** Ni viumbe wa kubuniwa na mwandishi wanaotumiwa katika kazi yoyote ya fasihi.Wanaweza kuwa watu, wanyama, ndege, majini na hata viumbe wengine wa kidhahania.

**Utamaushi :** Ni hali ya kukata tamaa au kutokuwa na furaha kutokana na hali duni ya maisha.

**Saikolojia:** Ni taaluma inayohusisha uchunguzi wa akili, hisia na tabia za mtu au kikundi cha watu.

**Uchanganuzi Nafsia:** Kitengo cha Saikolojia kinachohusiana na uhalisia na kufafanua misukumo inayowafanya wahusika kutenda wanavyofanya.

**Ung'amuzi bwete :** Hii ni sehemu ya akili ya binadamu inayohodhi fikra, mawazo, hofu na mitazamo hasi isiyoweza kukubalika katika jamii.

**Mwendawazimu:** Mtu asiye na akili timamu,mwenye maradhi ya akili,kichaa.

**Wendawazimu:** Tabia ama hali yoyote inayosababisha msongo wa kihisia unaomfanya mtu kuteseka,unaodhuru au usiokubalika na jamii. Ni hali inayotokana na unyevu wa akili zenye masumbufu;hitilafu katika mfumo wa fikra.

## IKISIRI

Utafiti huu unalenga kuchunguza nafasi ya wahusika wendawazimu. Wahusika hawa ni Matuko Weye na Bilal katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora:2012) na *Mkamandume* (Mohamed:2013).Malengo ya utafiti huu lilikamilishwa ambayo ni matatu ni pamoja na: kuchunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui ya riwaya teule, kubainisha mchango wa wahusika hawa katika kuendeleza mbinu za uandishi na kuthibitisha jinsi wahusika wendawazimu wanafaulisha dhamira ya waandishi. Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia ilitumika katika kuchambua data ya utafiti.Kwa mujibu wa Freud (1913), Uchanganuzi Nafsia hufananisha kazi ya fasihi na ndoto. Riwaya, tamthilia na Ushairi ni kazi zinazofananishwa na ndoto kwani ni kazi bunifu. Usanii ni ndoto zinazoashiria matumaini na matamanio ya mwandishi. Aidha, wahusika katika fasihi ni viumbe au binadamu wanaoishi katika ndoto za mwandishi. Wao hushirikiana na mwandishi katika matarajio na matatizo yake. Ukusanyaji wa data ulifanyika maktabani. Riwaya teule za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* zilisomwa pamoja na majarida, tasnifu, vitabu na matini husika kutoka mtandaoni. Tulipitia nyaraka na kusoma kwa umakinifu ili kudondoa data iliyotakikana. Utafiti huu si linganishi . Tulitumia sampuli ya kimaksudi ili kupata data ambayo tulishughulikia kuuendeleza utafiti. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uchanganuzi-nafsia. Uwasilishaji wa matokeo ulifanyika kwa kuzingatia mbinu ya maelezo. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa waandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* waliwashirikisha wahusika wendawazimu ambao ni Matuko Weye na Bilal. Wahusika hawa wamechangia kukuza maudhui ambayo ni pamoja na vita dhidi ya udhalimu, uongozi mbaya, elimu na ukombozi. Utafiti huu pia umefaulu kubainisha mchango wa wahusika hawa katika kuendeleza mbinu za uandishi.Wahusika wendawazimu wamechangia kukuza mbinu za uandishi kama vile taswira, kejeli, mbinu rejeshi, kinaya, balagha, dayalojia na ucheshi. Utafiti pia umebainisha dhamira ya waandishi ya kueleza masaibu yanayowakumba wanyonge katika jamii, kuangazia na kutahadharisha kuhusu athari za uongozi mbaya unaosababisha kugawanywa kwa raia katika misingi ya kitabaka. Changamoto tulizozipitia zimeangaziwa na hatimaye tumetoa mapendekezo kwa watakaofanya tafiti za baadaye kuhusiana na riwaya hizi.Utafiti huu utasaidia jamii kwa jumla. Utawafaa wanajamii, wanafunzi, wahadhiri na wahakiki wa fasihi.

## ABSTRACT

The research is aiming at examining the role of mad characters: Matuko Weye and Bilal in the two sampled novels: *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora:2012) and *Mkamandume* (Mohamed:2013).In order to achieve this aim the research was guided by three objectives which include investigating why the authors involved them, their contribution towards the development of the themes, stylistic devices and the authors' intention. The theory of Psychoanalysis was employed in data analysis. Freud (1913) explained the connection between literature and Psychoanalysis. He compared fantasy, plays, dreams and the work of art in order to understand creativity. For Freud, a literary work is analogous to a daydream. It contains in it's fantasy the fulfillment of an unsatisfied wish and thus improves on an unsatisfactory reality. Data collection was primarily done from the library through reading the sampled novels. Secondary data was obtained through reading journals, books, thesis and other related materials in the internet through reading and analyzing the content. Purposive sampling was done. Two Kiswahili novels were selected in order to get the required data. Data analysis was guided by research questions, objectives and the tenets Psychoanalysis theory. The findings were presented in a descriptive form. The findings reveal that the authors of *Kidagaa Kimemwozea* and *Mkamandume* have depicted the mad characters who have successfully contributed in thematic development as themes which include fight against oppression, bad leadership, education and liberation. Stylistic devices such as description, satire, flashback, irony rhetoric questions, dialogue and humour have been developed through the sampled characters. The authors' intentions of involving these characters as their mouthpiece to condemn the evils in the society which mostly are as a result of poor governance have been illustrated.The challenges faced during the research as well as the recommendations are also considered in this work. Therefore the research will be great benefit to the society students, researchers and tutors in the field of literature.

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI WA UTAFITI

### 1.0 UTANGULIZI

Sura hii inaweka msingi wa utafiti huu. Imeshughulikia usuli wa mada,suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti huu pamoja na sababu za kuchagua mada. Vilevile, mbinu za utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ambayo ilikuwa msingi wa utafiti huu imefafanuliwa.

### 1.1. USULI WA MADA.

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya teule ambazo ni *Kidagaa Kimemwozea* (2012) *na Mkamandume* (2013). Kulingana na Kimaro (2014), wahusika ni wale washiriki ama viumbe waliotajwa katika kazi yoyote ya fasihi. Wanaweza kuwa watu, wanyama, ndege, majini na hata viumbe wengine wa kidhahania. Kwa kuwa ni viumbe wa kubuniwa na mwandishi hawaonekani bali kwa hisia tu, wale tunaowaona waigizapo jukwaani ni wawakilishi wa wahusika jinsi walivyosawiriwa na msanii. Msanii huwatumia wahusika kama vyombo vya kuuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji au watazamaji.

Wahusika ni kipengele muhimu katika uchambuzi wa fani katika kazi ya fasihi. Wahusika hushirikishwa na mwandishi katika kufanikisha mambo mengi kama: kuleta mtiririko mwema wa vitushi, kujenga wahusika wengine,

kuendeleza mbinu za usanii na usanifu, nia ya mwandishi na maudhui. Kwa mujibu wa Carl Jung (1990) kuna aina mbili kuu za wahusika: wahusika bapa na wahusika duara. Anafafanua kwamba wahusika bapa ni wale wasiobadilika kuanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho. Wahusika duara nao ni wale ambao hubadilika, hukua kimawazo na kupevuka.

Mawazo ya Jung yanaungwa mkono na Forster ambaye anasema kuwa wahusika bapa kwa kawaida hawabadiliki toka mwanzo mpaka mwisho wa kazi ya fasihi. Walio na tabia nzuri hubakia na sifa hiyo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Walio na sifa mbaya nao hubakia na sifa hiyo katika kazi nzima. Kulingana naye, wahusika bapa hutumiwa na mwandishi kusimamia dhana au wazo fulani. Maoni haya pia yanafanana na ya Lyon na Leslie (1963), Senkoro (1982), Mlacha (1985) na Msokile (1992). Hawa wanasema kuwa wahusika bapa huumbwa na msanii kwa madhumuni ya kuwakilisha dhana, sifa au wazo moja katika kazi ya fasihi. Tabia yao inabakia kuwa ile ile wala hawabadiliki licha ya mahusiano yao na wahusika wengine, au kutokana na mabadiliko ya mazingira yao.

Rieger (1994) anafafanua masuala nyeti kuhusu dhana ya wazimu katika fasihi. Mathalani, maana yake, mchango wake katika kuelewa fasihi, dhana ya waandishi wendawazimu na matendo ya wahusika wendawazimu. Aidha, ameshughulikia uhusiano kati ya wazimu katika fasihi na ule unaoshughulikiwa na matabibu wa kisaikolojia, mchango wa istilahi za kisaikolojia katika kutuwezesha kuwaelewa wahusika katika fasihi, mtazamo wa wanajamii kuhusu wazimu na mustakabali wa dhana za wazimu.

Aidha, anaeleza kwamba yeyote anaweza kutambua sifa za wendawazimu kwa sababu matukio mengi yaliyokiuka maadili yanabainika barabara yakilinganishwa na yale ya wenye akili timamu. Kadhalika anasema kuwa hakuna jambo linalotenganisha wazimu na urazini barabara.

Debra (1998) akimnukuu Szasz anaeleza kuwa mikatale ya kijamii kama unyanyapaa, kudhibiti tabia za wanajamii na nadharia ya utekelezaji wa majukumu huusawiri wendawazimu kama matokeo ya migogoro katika mahusiano ya kijamii. Wade na Travis (2011) nao wanaeleza wendawazimu kuwa tabia ama hali yoyote inayosababisha msongo wa kihisia unaomfanya mtu kuteseka,unaodhuru au usiokubalika na jamii.

Mutugu (2019) anafafanua kuwa ulemavu wa akili ni hali ambapo mtu hukosa uwezo wa kufanya mambo mbalimbali yanayoambatana na umri na urazini wake kama binadamu. Kutokana na maelezo yake wendawazimu ni mojawapo ya aina za ulemavu ;ni ulemavu wa akili. Kadhalika, akiwanukuu Bennet na Royale (1999) anaeleza kuwa mitazamo kuhusu ulemavu inaweza kujikita katika imani za kidini. Kutokana na jambo hili, inakuwa vigumu sana kueleza dhana ya ulemavu kwani maana yake hutofautiana kutoka itikadi ya dini moja hadi nyingine au kutoka kwa muktadha mmoja hadi mwingine.

Kuna uhusiano kati ya Saikolojia na Fasihi kwani taaluma zote mbili hushughulika kufafanua matendo yasiyo ya kawaida miongoni mwa wanadamu. Ndiposa, istilahi wazimu ni muhimu katika kuelezea baadhi ya wahusika katika fasihi. Sifa zisizo za kawaida, wehu na zile zilizokiuka maadili

miongoni mwa wahusika ni muhimu katika uchunguzi wa wasifu wa mhusika fulani.

Japo taaluma hizi mbili hunuia kufumbua wasifu wa binadamu, kuna baadhi ya mambo ambayo bado hayajaeleweka barabara. Kwa mfano, ni nini hasa chanzo cha wendawazimu na tiba ni gani? Katika taaluma ya utabibu wendawazimu ni jambo la aibu kwa sababu ya mienendo inayoambatana nao kama maangamizi na tabia zisizokubalika katika jamii. Pia katika fasihi wendawazimu una sifa mbili kinzani. Waweza kuhuzunisha, kuleta balaa na pia kutuburudisha kama vitendo vya King Lear au the Underground man sababu wahusika hawa wameelezea mambo ambayo watu wengi huhofia kuyaeleza.

Ni bayana kuwa watu wengi hudhibiti hisia za wendawazimu kwa sababu ya miiko ya jamii. Kwa hivyo katika fasihi kuna uwezekano wa kueleza hisia hizi bila wasiwasi. Japo watu wengi sio wendawazimu,huwa wana migogoro ya kinafsia. Waandishi wameweza kuandika kazi zinazosawiri hali halisi ya kisaikolojia ya watu kupitia kwa wahusika.

Freud (1913) naye alichangia kuleta suluhisho kupitia kwa tiba yake kwa kuwapa wagonjwa wa akili nafasi za kusimulia kadhia zao.Tiba hii pia iliwawezesha wataalamu kuelewa chanzo cha waja kuwa na ugonjwa wa akili. Hata hivyo, unyanyapaa na kutowaelewa wagonjwa hawa kulilemaza juhudi za kuwatibu wagonjwa wa akili kwa sababu wendawazimu hudhihirishwa kwa vitendo vya ghasia, mauaji, ulaghai, usaliti, tamaa na upweke kwa kina.

Wade na Tavris (2011) nao wanaeleza wendawazimu kuwa tabia ama hali yoyote inayosababisha msongo wa kihisia unaomfanya mtu kuteseka, unaodhuru au usiokubalika na jamii. Kulingana nao,wendawazimu kwa mtazamo wa kisanii umetumika kama njia ya uhakiki kwa namna tatu: kwanza, mwandishi anaweza kusawiriwa kuwa mwendawazimu. Pili, wahusika waliosawiriwa kuwa wendawazimu na mwandishi na tatu, kuna njia ya uhakiki ambayo istilahi za kisaikolojia zinazotokana na utafiti wa kitabibu kuhusu wendawazimu zinatumika kueleza wendawazimu wa kisanii.

Katika kuzingatia namna ya kwanza ambapo wahusika husawiriwa kuwa wendawazimu na waandishi,waandishi huwasawiri wahusika wakiwa na mienendo au tabia zisizo za kawaida kwa sababu kadhaa kama vile kueleza yaliyo katika fikra zao/ migogoro ya kinafsi na pia kuelezea hisia za binadamu. Aidha, mhusika anaweza kuwa na sifa zinazothibitisha dosari za kisaikolojia kama msongo wa akili. Pili, kuna wahusika waasi ambao wanapinga kanuni dhalimu za jamii kwa kuonekana wendawazimu au wenyewe kurukwa na akili. Wendawazimu wa wahusika hawa hutuwezesha kuwaelewa wahusika wenyewe na pia hufichua mengi kuhusu jamii husika.Tatu, wahusika wanaweza kukengeuka na hali hii iwatenganishe na jamii

Ukengeushi huu unawatenga wanajamii katika jamii yenye watu wanaoishi maisha kulingana na matakwa ya jamii husika. Aghalabu mwandishi hushirikisha wahusika wendawazimu kisanii kukejeli jamii na pia matendo ambayo wanajamii hutenda yanayosababisha wahusika wake kurukwa na akili. Mtazamo huu wa pili unachangia katika kazi hii kwa kiasi kikubwa kwani ndio

utafiti wetu unaegemea; kuwachunguza wahusika waliosawiriwa kuwa wendawazimu na waandishi.

Rieger (1994) akimnukuu Shakespeare anafafanua kuwa wahusika hawa husema ukweli mchungu ambao wanajamii wanahofia kusema na hata wakati mwingine wasioutilia maanani. Wahusika hawa huchukua nafasi ya waasi au wanaopinga udhalimu katika jamii. Waandishi huwasawiri wahusika hawa kama watu ambao wamejitenga au wametengwa na jamii ama kwa kutaka, kwa kulazimishwa, kuugua au inapofaa.Wao huwasilisha maadili ambayo wanajamii huyachukulia kuwa muhimu na ambayo wahusika hawa huasi kupitia kwa maisha, imani au matendo yao. Matatizo haya ya tabia za binadamu yameshughulikiwa sana katika kazi za Wamarekani. Hali hii ya wahusika kuwa na kichaa kinachowafanya kufurahia mateso imefafanuliwa na Fiddick katika mhusika aliyemsawiri kama *Underground man. (*Rieger,1994)

Debra(1998) ameeleza sifa za wendawazimu katika tendi za kale. Anaeleza kuwa mbali na wahusika kuwa wendawazimu, hali ya wendawazimu ina mchango mkubwa katika maudhui ya kazi za fasihi. Anafafanua changamoto zilizopo katika kufasiri wendawazimu na kufasiri dhana hii kwa kirefu katika mashairi.

Waandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* ambao ni Walibora na Mohamed ni wazaliwa wa Afrika Mashariki ambapo Walibora ni Mkenya naye Mohamed ni mzaliwa wa nchi jirani ya Tanzania. Walibora na Mohamed wameandika kazi nyingi za fasihi andishi kama vile, tamthilia, hadithi fupi , mashairi na riwaya. Japo waandishi hawa wamelelewa nchi

tofauti na kusomea shule na vyuo vikuu tofauti, tajriba yao kuhusu jamii ina mshabaha mkubwa. Wanawasawiri wahusika wendawazimu kama vipaza sauti vya kuwasilisha ujumbe mzito katika jamii ambao walio na akili zao razini wanachelea kusema.

Utafiti huu umewachunguza wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* ambao ni Matuko Weye na Bilal mtawalia. Umebainisha mchango wao katika kuwasilisha maudhui ya waandishi. Utafafanua jinsi wamechangia kuendeleza mbinu za uandishi. Kadhalika, unakusudia kuthibitisha jinsi wahusika wendawazimu wamefanikisha kuwasilisha dhamira ya waandishi. Hii ni kwa sababu waandishi mbalimbali wa kazi za fasihi wamesawiri wahusika ainati katika kazi zao kama wanawake, makahaba na walemavu ila kulingana na utafiti wetu, hakuna utafiti unaoshughulikia wahusika wendawazimu kwa malengo tuliyotaja.

## 1.2 SUALA LA UTAFITI.

Utafiti huu ulichunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwoze*a ya Ken Walibora na *Mkamandume* ya Said .A.Mohamed. Uliwabainisha wahusika wendawazimu katika riwaya hizi, kisha kueleza na kuchanganua nafasi zao. Utafiti ulichunguza jinsi wahusika hawa wanachangia maudhui katika riwaya. Vilevile, ulilenga kutathmini jinsi wahusika hawa wanaendeleza mbinu za usanifu mathalani: kinaya, kejeli na chuku. Aidha, kupitia kwao maudhui ya vita dhidi ya udhalimu, ukombozi na uongozi mbaya yamefafanuliwa. Kadhalika, wamethibitisha dhamira ya

waandishi ya kuwatumia wahusika wendawazimu kama kipaza sauti cha kuwasilisha ukweli mchungu katika jamii.

## 1.4. MALENGO YA UTAFITI

(i) Kuchunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui ya riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume.*

(ii) Kubainisha mchango wa wahusika hawa katika kuendeleza mbinu zauandishi katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume.*

(iii) Kuthibitisha jinsi wahusika wendawazimu wanafaulisha dhamira ya waandishi katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*.

## 1.3 .MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

(i) Wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* wamefanikisha maudhui ambayo waandishi wananuia kueleza?

(ii) Ni kwa kiasi gani wahusika Matuko Weye na Bilal wanaendeleza mbinu za uandishi katika riwaya husika?

(iii) Wahusika hawa wawili wanachangia vipi katika kuendeleza dhamira ya waandishi?

## 1.5. SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Utafiti uliofanywa kuhusu wahusika katika riwaya za Kiswahili kwa muda mrefu umekuwa ukishughulikia wahusika wanawake, wanaume, vijana, watoto na wenye ulemavu. Mutugu (2019) ameshughulikia taswira za ulemavu kama mtindo katika riwaya teule. Kulingana na utafiti wake ulemavu wa akili ni mojawapo ya mtindo uliotumiwa na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi katika kuwasilisha maudhui yao.

Naye Mayieka (2015) anajadili masuala ibuka katika riwaya za Kisasa ambazo ni *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi yangu* yakiwemo ulemavu, ukiukaji wa haki za binadamu, kutowajibika kazini, ufisadi, elimu,uongozi wa kiimla na lugha ya Kiswahili. Anarejelea ulemavu wa aina mbalimbali na kutambua kuwa jamii za kiafrika zina imani potovu kuhusu ulemavu. Anafafanua kuwa ulemavu unachukuliwa kama laana katika jamii na walemavu hawaonyeshwi upendo wanadharauliwa , kupuuzwa na kuchukiwa. Katika jamii ulemavu ni mwiko. Anamrejelea mhusika Matuko Weye ambaye maoni yake yanapuuzwa kwa vile ni mwendawazimu.

Wahusika wendawazimu wameshughulikiwa kwa mtazamo kuwa wazimu ni ulemavu ambao unachangia katika kazi husika kama mtindo na kama suala ibuka mtawalia. Vilevile, utafiti wa Mayieka umemshughulikia mhusika Matuko Weye katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ambaye utafiti wetu unamtafitia pia. Tofauti iliyopo kati ya tafiti hizi na utafiti wetu ni kuwa, utafiti wetu unazamia nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya mbili ambazo ni *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* kwa lengo la kuthibitisha

nafasi yao katika kuendeleza maudhui, mbinu za uandishi na dhamira ya waandishi. Kwa hakika utafiti huu unadhihirisha jinsi wahusika hawa wametumiwa kama vipaza sauti vya waandishi katika kuangazia mambo ambayo wahusika wengine wanachelelea kuyazungumzia wazi wazi.

Uchunguzi wa wahusika hawa umewawezesha waandishi kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kipekee na yenye uzito zaidi, jambo ambalo halingewezekana iwapo wangetumia wahusika wa kawaida. Utafiti huu unalenga kuweka wazi maudhui, mbinu za uandishi na dhamira ya waandishi ambazo hazijitokezi moja kwa moja katika riwaya teule. Uchunguzi wa wahusika hawa unafafanua umuhimu wa kutathmini kauli za wahusika wendawazimu katika riwaya teule ili kufahamu mchango wao katika kufanikisha baadhi ya ya vipengele vya fani.

Kadhalika, uchunguzi wa nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* unafafanua umuhimu wa kupiga darubini maneno, vitendo na uchoraji wa wahusika katika kazi ya fasihi ili kutambua mchango wao katika kufanikisha kazi ya mwandishi. Hii ni kwa sababu hawabwagwi tu katika kazi ya fasihi bali kila mhusika huwa na majukumu mahususi ya kutekeleza ili kufaulisha kazi ya mwandishi.

Utafiti huu unazindua wasomaji wa fasihi kuwatathmini wahusika wendawazimu sio tu kama wendawazimu bali kama wahusika wenye dhima maalumu katika kazi ya fasihi. Kuna uwezekano kuwa wale wahusika wanaoaminika kuwa na akili razini ndio kiwango chao cha wendawazimu kiko juu kuwapiku wanaoonekana kutokuwa na akili timamu.

Kwa vile waandishi huchota maudhui, kutoka katika jamii na huwatumia wahusika kuyawasilisha maudhui hayo, wahusika wendawazimu wanatumiwa na waandishi kuelezea maudhui mazito na kueleza yale mambo ambayo watu walio na akili timamu wanachelea kuyasema hadharani. Wao ni vipaza sauti vya mambo ambayo wanajamii wanahofia kuyasema waziwazi. Vilevile, uchunguzi wa nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* haujashughulikiwa kwa malengo tuliyoainisha japo riwaya hizi zimewashirikisha wahusika hawa.

Kuna haja yakutafitia kuhusu wahusika wendawazimu katika riwaya hizi teule. Mada hii inafaa ili kutathmini nafasi ya wahusika hawa katika riwaya husika. Ni muhimu kuchunguza kwa kina kinachowafanya waandishi hawa kuwashirikisha wahusika wendawazimu. Mada hii ya kutafitia itafaa hasa wakati huu ambapo wahusika wendawazimu wanaendelea kuongezeka katika jamii ilikufahamu mchango wao katika kazi za waandishi. Wahusika hawa wanaibua tajriba ya waandishi ya kijamii kwani kazi zao za kisanii zinasawiri uhalisia wa maisha.

Uchunguzi huu ulichochewa na hali ya kutaka kufanya uchunguzi kwa mapana kuhusu nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za Kiswahili kwani katika kuwachambua wahusika hawa, zitaeleweka zaidi kwa sababu mchango wao utajitokeza katika kuendeleza mbinu za uandishi, maudhui na dhamira ya waandishi. Kwa hivyo, umuhimu wao utabainika barabara.Aidha, watafiti wengine watapata shauku ya kutafitia wahusika wendawazimu katika riwaya

nyingine na pia wahusika wengine kama wazee, watoto, vijana na wenye ulemavu katika riwaya mbalimbali.

Mtafiti aliamua kuchunguza kazi za waandishi hawa wawili kwa kuwa ingawa wanatoka katika mazingira tofauti, mtazamo wao wa dhana ya wendawazimu unafungamana na Imani na utamaduni wa jamii. Mutugu (2019) akiwanukuu Ingstad na Whyte (1995) anaeleza kuwa ulemavu ni swala la kiitikadi na hujikita katika falsafa ya jamii ya mwandishi. Anaendelea kufafanua kuwa kila jamii ina mtazamo wake kuhusu ulemavu. Mtazamo huu unahusiana moja kwa moja na utamaduni wa jamii. Kadhalika, kila mwandishi katika utunzi wake huathiriwa kwa namna moja au nyingine na jamii inayomzunguka. Hali hii husababisha kuzuka kwa mtazamo na taswira mbalimbali kuhusu ulemavu.

**1.6. UPEO NA MIPAKA.**

Uchunguzi huu ulijikita katika kutafiti suala la nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya teule katika fasihi andishi ya Kiswahili. Katika kutalii mada hii tulichambua wahusika ambao ni MatukoWeye katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na Bilal katika riwaya ya *Mkamandume*. Japo waandishi wa riwaya hizi wameshirikisha wahusika ainati mathalani wazee, vijana, wenye ulemavu na wengineo, wahusika wendawazimu wamepewa dhima muhimu katika riwaya husika. Riwaya hizi zinateuliwa kimaksuudi kwa vile wahusika hawa wametumiwa kama vipaza sauti vya waandishi katika kuangazia mambo ambayo wahusika wengine wanachelelea kuyazungumzia wazi wazi.

Kadhalika, uchunguzi wa wahusika hawa umewawezesha waandishi kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kipekee na yenye uzito zaidi, jambo ambalo halingewezekana iwapo wangetumia wahusika wa kawaida. Utafiti huu unalenga kuweka wazi maudhui, mbinu za uandishi na dhamira ya waandishi ambazo hazijitokezi moja kwa moja katika riwaya teule.

Riwaya hizi tulizoteua ziliwakilisha kikamilifu mtazamo wa waandishi hawa kuhusu suala la wahusika wendawazimu. Waandishi hawa tuliwachagua kwa sababu wamewapa wahusika wendawazimu nafasi muhimu. Wamewashughulikia kwa upana na kujaribu kudhihirisha mchango wao kwa mapana. Vilevile, uteuzi huu uliongozwa na ukweli kwamba mada ya kuwepo kwa wahusika wendawazimu ni suala bia ambalo hupatikana katika jamii nyingi sio tu tatizo la nchi moja. Japo Walibora ni mzaliwa wa Kenya na Mohamed ni mzaliwa wa Tanzania, kazi zao zimewasawiri wahusika hawa. Ni tatizo ambalo linashuhudiwa likiwaathiri waja wengi katika jamii siku hizi.

Vilevile, waandishi wanasimulia sababu za wahusika hawa kuwa katika hali hii au wanawafanya wahusika wenyewe kusimulia historia zao zilizochangia hali zao. Waandishi wamewasawiri wahusika hawa kwa njia inayobainisha kuwa hawa kubwagwa tu riwayani, bali wanayo malengo wanayotimiza. Wao ni kipaza sauti cha waandishi cha kutekeleza wajibu muhimu. Katika hali yao ya wendawazimu, wanayakashifu maovu hadharani, jambo ambalo wahusika wa kawaida hawana ujasiri wa kulifanya na linalowafanya wahusika wengine kushangaa kwamba wahusika wendawazimu wanayaelewa matatizo yaliyomo katika jamii.

Utafiti huu uliweza kufafanua mchango wa wahusika wendawazimu katika riwaya hizi teule. Tulichunguza mchango wao katika kuendeleza maudhui, mbinu za uandishi na dhamira ya waandishi.Utafiti ulifanyika katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, kusoma kazi teule, majarida, magazeti, tasnifu na katika mtandao.

## 1.7. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.

Kwa kupitia vitabu, majarida, tasnifu na makala mbalimbali, mtafiti alibainisha kuwa tafiti zilizofanywa kwa lugha ya Kiswahili zimeshughulikia wahusika mbalimbali kama walemavu, makahaba, wanawake, wanasiasa, vijana na wanaume miongoni mwa wengine.Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu wahusika wendawazimu zimefasiri hali hii kama mojawapo ya aina mbalimbali za ulewavu zinazowakumba wanadamu katika jamii.

Mayieka (2015) alishughulikia masuala ibuka katika riwaya za kisasa akirejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi Yangu*. Masuala ibuka anachunguza ni pamoja na: ulemavu,ukiukaji wa haki za binadamu, kutowajibika kazini, elimu, uongozi wa kiimla na lugha ya Kiswahili. Kuhusu ulemavu anaeleza kuwa jamii nyingi za Kiafrika zina Imani potovu kuhusu ulemavu. Akimnukuu Siva (2015) anaeleza kuwa ulemavu unachukuliwa kama laana katika jamii. Walemavu hawaonyeshwi upendo,wanadharauliwa, wanapuuzwa na kuchukiwa. Ulemavu unachukuliwa kuwa mwiko katika jamii.

Akiirejelea familia ya Mwalimu Majisifu iliyojaliwa pacha wawili walemavu, mwalimu anamlaumu bibi yake Dora kwa kujifungua watoto walemavu.

Mwalimu anamwona mkewe kama mwenye laana kutokana na dhambi alizofanya kwao na kusababisha kumzalia watoto walemavu.

Kadhalika Mayieka akimrejelea mhusika Matuko Weye, anafafanua kuwa maoni ya mhusika huyu yanapuuzwa kwa vile yeye ni mwendawazimu. Mtemi Nasaba Bora anayaona maneno yake kama uchochezi kwa wananchi na kuamuru awekwe rumande. Kulingana na utafiti huu, licha ya ulemavu wake anachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwazindua Wanasokomoko kuhusu dhuluma za Mtemi. Hii ni ishara kuwa hata walemavu wana sehemu muhimu katika ukombozi wa nchi. Aidha, anamrejelea mhusika Mashaka ambaye anawehuka baada ya mchumba wake Ben Bella kukatiza uchumba wao. Kuwehuka kwa mhusika huyu kunaiua ndoto yake ya kuwa mwandishi.

Utafiti wa Mayieka una mchango mkubwa kwa utafiti wetu kwa sababu umerejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na zaidi ya hayo ukamchunguza mhusika Matuko Weye . Tofauti ya utafiti wake na huu ni kwamba utafiti wetu unachunguza mchango wa hali ya wendawazimu wa Matuko Weye katika kuendeleza maudhui, mbinu na dhamira ya mwandishi. Kadhalika, utafiti wake uliongozwa na nadharia ya uhalisia ilhali wetu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi nafsia.

Usawiri wa vijana katika ujenzi wa jamii mpya katika riwaya teule za Kiswahili umechunguzwa na Mwangi (2022). Alifafanua jinsi vijana walifanikiwa kubadilisha mtazamo wa watu kuhusu walemavu katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Katika utafiti wake anathibitisha jinsi mhusika Imani alivyokubali na kujituma kuwatunza watoto walemavu wa mwalimu

Majisifu ambapo wawili walitokwa na udenda mdomoni na wengine wawili waliolemaa na kutoweza kutembea. Japo baba yao aliwadharau na mama yao alilalamikia kazi kubwa ya kuwalea, Imani aliwalea na kuwapenda bila kulalamika. Kadhalika, anafafanua kuhusu msichana mlemavu aliyekutana na Mtemi katika matwana na Mtemi akamtongoza lakini mwisho wa safari alipogundua kuwa msichana alikuwa mlemavu akabadili nia. Kwa kufanya hivi, anaweka wazi umuhimu wa kuwaona walemavu kama binadamu. Utafiti huu umerejelea ulemavu na kusisitiza umuhimu wa kuwathamini kama binadamu. Kinyume na wetu, huu unarejelea viungo na kusisitiza kuwa hali hii wahusika walizaliwa nayo .Vilevile, utafiti wetu unatathmini wahusika wendawazimu tu na mchango wao. Kadhalika, mtafiti alitumikiza nadharia ya uyakinifu wa kijamii ilhali utafiti wetu umejikita katika uchanganuzi nafsia.

Mutugu (2019) alichunguza taswira za ulemavu kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Amefafanua ulemavu kama hali ya kimsingi ya tofauti zinazopatikana miongoni mwa binadamu. Katika utafiti wake amerejelea aina tatu za ulemavu zilizosawiriwa na waandishi kama mtindo ukiwemo ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo. Utafiti wake uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni nadharia ya mtindo na ile ya semiotiki.

Mutugu ameeleza jinsi taswira za ulemavu wa akili zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Utafiti wake una mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa sababu: kwanza, unaufafanua wendawazimu kama ulemavu wa akili na

kufafanua mchango wa mtindo huu wa waandishi kama njia ya kuwasilisha maudhui yao. Tofauti ya utafiti wake na huu ni kwamba alishughulikia uwasilishaji wa maudhui lakini utafiti wetu ulichunguza jinsi wahusika wendawazimu wamechangia kuendeleza sio tu maudhui mbali mbinu za uandishi na dhamira za waandishi wa riwaya teule. Kadhalika utafiti wetu ulishughulikia riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*

Devlieger (1999) ameshughulikia miktadha ya kimaisha na kimaana inayojitokeza katika methali hamsini na tano zinazohusu ulemavu katika makala yake. Amezingatia lugha kutoka Malawi, Senegal, Tanzania,Zambia, Zaire na Zimbambwe. Alichunguza methali katika lugha hizi na kubainisha maana bayana na batini. Katika makala yake anatambua kuwa ulemavu kama tukio unahusisha taashira nzito. Anabainisha kuwa kwa upande mmoja, mtu mwenye ulemavu anadhihirisha taashira ya maisha yenye matumaini, ubunifu na maadili na kwa upande mwingine ulemavu umewashilishwa kama uovu ambao chanzo chake lazima kichunguzwe.

Utafiti wa Devlieger unachangia utafiti huu katika kubainisha kuwa wahusika wenye ulemavu wanaweza kutumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya kimaadili. Vilevile, utafiti wake ulimhimiza mtafiti kudadisi kiini nna mwingiliano wa ulemavu wa akili na tabia na hivyo basi kuhamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa kuchunguza kiini cha ulemavu huu badala ya kuwalaumu na kuwatenga waathiriwa.Tofauti na Devlieger ambaye ameshughulikia methali katika makala yake na ulemavu kwa jumla, utafiti huu umejikita katika riwaya za Kiswahili na kushughulikia ulemavu

mahsusi ambao ni wa akili; umechunguza nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya teule.

Ongechi na Ruto (2002) wametafitia makala kuhusu ulemavu kama ulivyosawiriwa katika majina ya methali za jamii za Ekegusii na Nandi. Wamejadili mitazamo mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu kwa kuchanganua mfumo wa kupatiana majina na methali katika Ekegusii na Nandi. Lugha hizi mbili huzungumzwa nchini Kenya. Katika makala yao wanadai kuwa mitazamo mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu na nafasi walizopewa katika jamii ni mambo yanayoongozwa na mifumo ya Imani zao asilia.

Watafiti hawa wanatambua kuwa katika jamii hizi mbili ulemavu wa aina mbalimbali unaelezwa kikamilifu ukiwemo ulemavu wa akili na wa viungo. Jamii hizi zinawaona watu wenye ulemavu wakiwa sawa na wengine ila, wenye tofauti za kimaumbile. Vilevile, wanajamii wana imani kuwa kila hali, ikiwemo ulemavu ina chanzo maalum kama vile kutokana na laana ya mababu wa zamani. Wenye ulemavu wanapewa majina yanayooana na ulemavu wao hivi kwamba majina yao halisi yanatoweka na haya ya ulemavu yakawa majina yao halisi ya kuwatambulisha. Utafiti wao unatofautiana na huu kwa sababu wetu unashughulikia wahusika wenye ulemavu wa akili katika riwaya teule za Kiswahili.

Muundo wa majina na methali za Kiswahili huwadhalilisha watu wenye ulemavu. Waliaula (2009) alithibitisha haya katika makala yake yaliyozingatia matumizi ya kiambishi Ki- katika muundo wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili

na jinsi unavyoingiliana na ulemavu pamoja na athari zake katika ufasiri wa ulemavu. Alitambua kuwa matumizi ya kiambishi ki- katika ki-lema, ki-pofu, ki-wete, ki-ziwi, ki-gugumizi, ki-chaa, ki-guru na mengineo kabla ya mzizi wa neno ni dhalilishi na inashusha hadhi ya anayerejelewa. Utafiti wake unaufaa huu kwa kuwa unashughulikia walemavu na jinsi wanajamii wanavyowadhalilisha. Tofauti ya utafiti wake na wetu ni kwamba ameegemea zaidi kutambua nafasi ya watu wenye ulemavu katika suala ambalo ni la kishosolojia zaidi ilhali utafiti huu ulizingatia mtazamo wa kifasihi kwa kushughulikia mchango wa wahusika wendawazimu katika kukuza maudhui, mbinu na dhamira ya waandishi wa riwaya.

Mulready (2003) alichunguza jazanda zinazotumika katika tamthilia ya Mfalme Edipode na uhusiano wake na maudhui ya ujuzi na ujinga miongoni mwa jamii. Alitumia nadharia ya mtindo ambapo alihusisha jazanda mbalimbali na hali ya maisha ya binadamu kama vile mahusiano yake na wenzake miungu na uharibifu wa mazingira. Jazanda mbalimbali zilizotumika katika tamthilia ya Mfalme Edipode zilichunguzwa kwa kuzingatia jinsi zinavyohusiana na mazingira na athari zake. Alizingatia ulemavu wa kutoona kama jazanda ya ujuzi na ukweli na kutambua kuwa katika tamthilia hii ulemavu wa kutoona unachukua nafasi mbili. Kwanza, mwandishi anauwasilisha ulemavu huu kama ulemavu wa viungo unaowaathiri wahusika Edipode na Teresia. Pili, ulemavu umetumika kijazanda kupitisha ujumbe kuhusu mtafaruku, maovu na unyonge unaomkumba binadamu.

Sofokile anatumia hali ya kutoona kwa nabii Teresia kuashiria kuwa watu wanaweza kukosa kutambua uovu unaowazunguka katika jamii na hali hii inaweza kuwaletea madhara makubwa. Matumizi ya kejeli yanajitokeza kupitia kwa mhusika Edipode ambapo licha ya kwamba ana uwezo wa kuona hajitambui. Nabii Teresia hana uwezo wa kuona lakini ana uwezo wa kutambua uozo ambao umezunguka Edipode na maisha yake. Hata hivyo Edipode anapotambua ukweli anajitia upofu ili asione tena. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa misingi ya utanzu, nadharia na aina ya ulemavu ulioshughulikiwa.

Wright (2006) ameshughulikia maadili ya wahusika wenye ulemavu katika kazi zilizoandikwa na Lawrence kama Lady Chatterly's Lover. Wahusika wengi wenye ulemavu wanapata taabu kupigania nafasi zao katika jamii. Kadhalika, wanapata changamoto wanapojaribu kujitambua na kujitathmini. Anatambua ulemavu wa wahusika kama taswira inayotumika katika kazi za fasihi kama mtindo mwafaka wa kuwasilisha maudhui katika kazi husika. Kazi yake inaufaa utafiti huu kwani imethibitisha kuwa aina mbalimbali za ulemavu zinaweza kuingiliana. Ulemavu wa akili unaweza kusababisha ulemavu wa tabia ambapo mtu hukiuka kaida za jamii kwa sababu amepungukiwa kiakili na hana uwezo wa kufanya maamuzi yenye urazini. Tofauti ni kuwa riwaya iliyorejelewa ni ya Kiingereza na mtafiti ametumikiza nadharia ya kishosolojia.

Irwin na Moeller (2010) wameshughulikia usawiri wa ulemavu katika riwaya za michoro ya vijana. Uchanganuzi wao unajikita katika misingi ya Imani chapwa za kiasili zinazoshikiliwa na jamii kuhusu watu wenye ulemavu.

Walitafitia riwaya thelathini zilizoteuliwa kimaksuudi kulingana na malengo ya utafiti wao. Wanatambua kuwa katika riwaya hizi wahusika wenye ulemavu katika jinsia zote wamewakilishwa. Wengi wao wamechorwa kwa njia hasi. Wa kiume wamechorwa kama wahusika waovu ilhali wa kike wamesawiriwa kama wanyonge wanaohitaji huruma. Utafiti huu unalingana na wetu kwa kuwa jamii ina imani chapwa kuhusu watu wenye ulemavu. Tofauti ya wao na wetu ni kuwa wao unashughulikia riwaya za Kiingereza na wetu unashughulikia wahusika wendawazimu tu katika riwaya teule za Kiswahili.

Wahusika wa kibwege wamechunguzwa na Njue (2003). Alifanya utafiti kuhusu Mtazamo wa Sanaa ya Ubwege akirejelea vichekesho vya Machang'i - *Mundurume ni Mugambo* na Kihenjo-*Kiama kia ng'ombe*. Ametumikiza nadharia za sanaa ya ubwege na uchanganuzi usemi hakiki. Wahusika wa kibwege wametamauka ilhali katika utafiti wetu, japo wahusika Matuko Weye na Bilal ni wendawazimu, wanaonekana wakiendelea kupigania haki zao na za wananchi kwa jumla.

Rieger (1994) anauliza masuala nyeti kuhusu dhana ya wendawazimu katika fasihi. Mathalani, maana yake, mchango wake katika kuelewa fasihi, dhana ya waandishi wendawazimu na matendo ya wahusika wendawazimu. Aidha, ameshughulikia uhusiano kati ya wendawazimu katika fasihi na ule unaoshughulikiwa na matabibu wa kisaikolojia, mchango wa istilahi za kisaikolojia katika kutuwezesha kuwaelewa wahusika katika fasihi, mtazamo wa wanajamii kuhusu wendawazimu na mustakabali wa dhana za wendawazimu.

Rieger (1994) akimnukuu Robert anafafanua jinsi nadharia za fasihi zimechangia katika dhana ya wendawazimu. Kulingana naye wendawazimu ni istilahi inayohusiana na tafsiri nyingi. Ni hali inayoshuhudiwa miongoni mwa wanajamii. Ndiposa mara nyingi watu hulalamika kuhusu mambo yanayosababisha wendawazimu. Wendawazimu unaoshuhudiwa mara nyingi ni ule wa wenye mahoka ambao waweza kuogofya watu wenye roho dhaifu. Hasira hufasiriwa kama ishara ya wendawazimu. Mambo mengi ambayo binadamu hushindwa kujidhibiti kuyatenda, ashiki na mengineyo ambayo ni kinyume na maadili pia ni ishara za kutokuwa na akili razini.

Mtaalamu huyu anafafanua kuwa kuna uhusiano kati ya saikolojia na fasihi kwani taaluma zote mbili hujizatiti kufafanua matendo yasiyo ya kawaida miongoni mwa wanadamu. Ndiposa, istilahi wendawazimu ni muhimu katika kuelezea baadhi ya wahusika katika fasihi. Sifa zisizo za kawaida, wehu na zile zilizokiuka maadili miongoni mwa wahusika ni muhimu katika uchunguzi wa wasifu wa mhusika fulani.

Japo taaluma hizi mbili hunuia kufumbua wasifu wa binadamu, kuna baadhi ya mambo ambayo bado hayajaeleweka barabara. Kwa mfano,chanzo cha wendawazimu na tiba yake.Katika taaluma ya utabibu wenda wazimu ni jambo la aibu kwa sababu na mienendo inayoambatana nao kama maangamizi na tabia zisizokubalika katika jamii. Pia katika fasihi wendawazimu una sifa mbili kinzani.

Anaeleza kuwa ni bayana kuwa wengi wetu hudhibiti hisia za wendawazimu kwa sababu ya miiko ya jamii. Ndiposa katika fasihi kuna uwezekano wa

kueleza hisia hizi bila wasiwasi. Japo wengi wetu sio wendawazimu huenda tuna migogoro ya kinafsia. Waandishi wameweza kuandika kazi zinazosawiri hali halisi ya Kisaikolojia ya watu kupitia kwa wahusika.

Watunzi wa ushairi wa enzi za Urasmi waliaminika kuwa ilhamu yao ilitokana na Mungu au nguvu zisizoeleweka. Dionysus aliaminika kuwa mungu aliyewapagaza wendawazimu tabia zisizo za kawaida na ashiki katika visasili vya Wagiriki. Plato pia aliweza kutofautisha wazimu wa kitabibu na ule wa waandishi wa kazi za kubuni unaohusishwa na Dionysus.

Wahusika wendawazimu huwasilisha maadili ambayo wanajamii huyachukulia kuwa muhimu na ambayo wahusika hawa huasi kupitia kwa maisha, imani au matendo yao. Matatizo haya ya tabia za binadamu yameshughulikiwa sana katika kazi za Wamarekani.Mtazamo huu wa pili wa wahusika kuwa wendawazimu utachangia katika utafiti wetu ambao kimsingi, unachunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika riwaya mbili teule za Kiswahili, *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Wahusika Matuko Weye na Bilal wanaonekana kuwa na migogoro ya kinafsi inayochangiwa na udhalimu wa utawala uliopo.

Namna ya tatu ni njia ya uhakiki ambayo istilahi za Kisaikolojia zinazotokana na utafiti wa kitabibu kuhusu wendawazimu zinatumiwa kuelezea wazimu wa kisanii. Istilahi za kisaikolojia zinaweza kunukuliwa kutoka kazi za Freud, Jung, Horney au hata wananadharia wengine wa kisasa ama zitokane na maelezo halisi kama yale ya namna ya DSM 111. Fasihi na Saikolojia ni taaluma mbili zinazotegemeana kwani zote huchangia katika kuelewa tabia za

watu. Ndiyo sababu, uchunguzi kuhusu mada ya wendawazimu katika fasihi unachangia kumaizi tabia za wanadamu. Uhakiki wa kisaikolojia umekuwa nguzo muhimu hasa wakati wa Freud na umejikita katika mwandishi, uandishi, matini au msomaji wa kazi husika.

Licha ya mtazamo wa Ki-freud, msukumo wa tatu wa Kisaikolojia umetumika katika uhakiki wa kisaikolojia. Msukumo huu wa tatu hurejelea Saikolojia inayohusiana na ubinadamu unaoshirikisha kazi za Carl Rodgers, Abraham Maslows na Karen Horney wanaotoa mchango mbadala wa Utabia na Uchanganuzi Nafsia. Jambo hili ni la muhimu na la kuleta matumaini kuliko njia za kijadi na Saikolojia ya Kisayansi.

Uhakiki wa Kisaikolojia unaohusisha mitazamo ya Ki-Freud, Ufreud mpya, Jung, msukumo wa tatu wa Kisaikolojia, Lacan na njia nyingine za uchanganuzi nafsia za kufasiri fasihi umeshamiri sana. Kwa mfano, Debra (1998) amefafanua haya akirejelea kazi ya Berman inayochunguza jinsi waandishi wa leo hutumia uchanganuzi nafsia kuchunguza wahusika katika fasihi. Berman huchunguza uhusiano baina ya ubunifu na masuala ya utabibu kwa kuzingatia jinsi wasanii wanaweza kujiponya wenyewe na kuwaponya wengine kwa kubadili mateso kuwa kazi ya usanii. Anajadili baadhi ya dhana za kimsingi za Uchanganuzi Nafsia kama kuwalaumu wengine, uwili na ubinafsi.

Kwa mujibu wa Robert akiwanukuuu Welleck na Warren (1982) anaeleza kuwa mshairi ni mtu aliye na ilhamu, aliyepandwa na mapepo na mwenye wazimu unaomfaidi. Baada ya Segmor Krim kupatwa na wazimu alibadilisha

mtazamo wake kuhusu wendawazimu. Wakati huo wendawazimu ulichukuliwa kuwa jambo mbaya zaidi ambalo liliwahi kumtendekea binadamu japo ni machache sana yaliyojulikana kuhusu hali hii.Anadai kuwa sharti watu wazinduke, walizungumzie suala hili lau sivyo watabaki kuwa wafungwa wa mtazamo wa jamii kuhusu wendawazimu huku wakishiriki katika wendawazimu ulio na kila mja unaotufanya sote kutokuwa razini.

Robert anaendelea kueleza kuwa uhusiano kati ya fasihi na wendawazimu hutuwezesha kujielewa, kuuelewa ulimwengu kupitia kwa ubunifu (ulimwengu wa kidhahania). Uhusiano huu ukishamiri katika kazi yoyote ya fasihi huiboresha zaidi. Martin katika makala yake anafafanua kuwa waandishi wengi walio na kipawa cha uandishi aghalabu hali yao ya kiakili huwa si imara jambo linalothibitisha kuwa wendawazimu na kazi zote za kisanii zinahusiana. Mtazamo wa kazi za kubuni kuathiriwa na hali ya akili kutokuwa timamu ni wa kale, hata nyakati za kina Plato. Katika karne ya kumi na tisa mtafiti wa Kisayansi Lombroso, alithibitisha kuwa mbali na usanii na wendawazimu kuwa na uhusiano, dhana hizi mbili zimehusishwa na jinai sababu zote zina chimbuko moja.

Waandishi kama wendawazimu husawiriwa vizuri katika taaluma ya Elimujamii. Kwa mujibu wa tafiti nyingi zilizofanywa watafiti walithibitisha na kunukuu mifano halisi katika maisha yao. Aidha, mtazamo huu huungwa mkono na tafiti za wataalamu kama Freud, Jung, Rank na watafiti wengine katika taaluma ya Utabibu wanaosisitiza uhusiano kati ya ubunifu na hali ya kutokuwa na akili razini maishani mwa binadamu. Wao husisitiza kuwa

wasanii hukiuka mipaka ya urazini ndiposa waweze kusimulia yaliyo katika sehemu ya ung’amuzi bwete akilini mwao, mengi ambayo ni yale waliyopitia wakiwa wadogo.

Martin anaendelea kufafanua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya Saikolojia na Fasihi. Taaluma hizi mbili huchunguza akili, roho, moyo na msukumo ulio ndani ya mhusika na kuoanisha mambo haya na athari zake katika tabia za mhusika (Rieger,1994,uk.34) . Kwa hivyo, Saikolojia imechunguza mengi katika fasihi yakiwa ni pamoja na: muundo na matini ya kazi ya fasihi, athari za kazi hiyo kwa akili na hisia za msomaji wa kazi husika, tatu, muktadha wa kazi ya mwandishi ikiwa ni pamoja na athari zake kwa waandishi wengine, hadhira, soko na asasi zinazowaleta hadhira na mwandishi pamoja. Nne, wandishi wenyewe, wasifu wao, motisha,uwezo wao wa kiakili, ufaafu wao na ubunifu wao.

Rieger (1994) anachangia utafiti huu kwa sababu makala katika kitabu chake yanafafanua dhana ya mwendawazimu kwa mitazamo mitatu. Miwili kati yake ni muhimu katika kuwasawiri wahusika wendawazimu na pia mtazamo wa kisaikolojia changanuzi uliojadiliwa kwani ndio unaoweka misingi ya nadharia ya utafiti wetu. Vilevile, unafafanua uhusiano uliopo kati ya Fasihi na Saikolojia.Hata hivyo pengo lingalipo kwani kazi zilizorejelewa ni za fasihi ya Kingereza. Utafiti wetu utajikita katika riwaya teule za Kiswahili

Kwa mujibu wa Debra (1998) hakuna kijelezo mwafaka cha wazimu. Toleo la nne la jarida lake linaeleza kwamba hakuna kijelezo kilichotolewa kinachotoa maana mahsusi ya magonjwa ya akili. Wengi waliojaribu kuelezea wanatoa

maana inayotokana na chanzo cha wendawazimu wenyewe. Maelezo yao yanaweza gawika katika makundi matatu, japo makundi haya yanaingiliana.Kundi la kwanza ni la kiunzi kinachoangazia jinsi ubongo wa binadamu hufanya kazi na ambacho hudhamiria kuchunguza chanzo cha kasoro zinazopatikana katika utendakazi wa akili. Chanzo cha kiunzi hiki ni sayansi changamani ikilinganishwa na tafiti zinazohusisha vipengele vingine. Szasz anaeleza kuwa tafiti nyinginezo hazihusishi matokeo ya kiutafiti bali kadhia. Kulingana naye ugonjwa wa akili ni sawa na ugonjwa wowote unaoathiri mwili wa binadamu kwa hivyo kuuchukulia kama ugonjwa sugu ni kama fumbo. Udhaifu wa kiunzi hiki ni kuwa huzigeuza tajriba za watu kuwa wendawazimu .

Viunzi hivyo vingine viwili kimsingi huchunguza wazimu na chanzo chake. Mikatale ya kijamii kama unyanyapaa, kudhibiti tabia za wanajamii na nadharia ya utekelezaji wa majukumu huusawiri wendawazimu kama matokeo ya migogoro katika mahusiano ya kijamii.

Viunzi vya Kisaikolojia hasa vile vya Freud vya uchanganuzi nafsia hufasiri wendawazimu kama upotovu wa kiakili wa mhusika. Mitazamo kuhusu wendawazimu imegawika kimsingi katika makundi matatu. Viunzi vya kimapokeo vinavyofanana na vya kisasa vya magonjwa ya kiakili ni viunzi vya kitabibu vinavyotumikiza njia za kisayansi. Debra (1998) anafafanua dhamira yake kuwa ni kuweka wazi chanzo cha ugonjwa huu ili kutia kikomo mitazamo mingi inayofafanua dhana hii. Yeye haamini kuwa kuna maradhi yanayosababishwa na nguvu za kiungu. Kulingana naye kila ugonjwa una

chanzo na dalili zake. Hali ya wendawazimu kuwa tofauti na maradhi mengine ndiyo huufanya uonekane kama unatokana na nguvu za kiungu.

Kwa mujibu wa Debra, waganga wa mitishamba, waponyaji wa imani za kidini, madaktari wa kienyeji na walaghai hudai kuwa wendawazimu ni ugonjwa unaotokana na nguvu za kiungu. Wao hufanya hivi ili kuficha ujinga wao kuhusu kutofahamu kuhusu chanzo na tiba yake. Hata hivyo Hippocratics wanaweza kutoa maarifa yanayotokana na utafiti wa kisayansi kuhusu wazimu.

Japo mwandishi alijikita katika ugonjwa wa kifafa utafiti wake una uhusiano na mawazo kuhsusu wendawazimu kwa kuwa hali zote mbili zilionekana kuhusiana enzi za kale kama inavyoelezwa katika wendawazimu wa mhusika mkuu katika Euripides Heracles. Katika mjadala wake kuhusu tafsiri ya kibayolojia ya chanzo cha wazimu, mwandishi anaeleza kuwa wendawazimu hutokana na unyevu wa akili zenye masumbufu.

Szasz anahitimisha kwa kusema kuwa DSM111 ina mchango mkubwa kwani waandishi wake wanafafanua dhana ya matatizo ya kiakili na yote yanayohusiana nayo. Jambo muhimu na la msingi kwa mwandishi ni kuwa kifafa na maradhi mengine yanasababishwa na au hitilafu fulani mwilini ama nguvu za kiungu. Katika jamii za kale ambazo mitazamo yake ya kidini wendawazimu ulionekana kama ugonjwa na chanzo chake hakimo ndani ya mhusika mbali nje ya mhusika. Wazimu unaotokana na kutiwa najisi ni dhihirisho la mahusiano kutokuwa imara kati ya binadamu na wenzake na kati na binadamu na Mungu au miungu.

Ni bayana kuwa pana pengo linalofaa kujalizwa kwani tafiti tulizorejelea zimeshughulikia wendawazimu kwa mtazamo tofauti na wetu ambao umejikita katika kuthibitisha kuwa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* mtawalia zimewashirikisha wahusika hawa. Ulifafanua nafasi ya wahusika hawa katika kuwasilisha maudhui, mbinu za uandishi na lengo la mwandishi. Aidha, nadharia ya uchanganuzi nafsia iliyotumiwa katika utafiti huu ilisaidia kuthibitisha jinsi waandishi wa kazi fasihi huwatumia wahusika kama kipaza sauti cha kuwasilisha mtazamo wao kuhusu mambo muhimu na ukweli mchungu katika jamii.

## 1.8. MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliegemezwa kwenye nadharia ya uchanganuzi nafsia. Kwa mujibu wa Wafula (2007), saikolojia changanuzi huzungumzia hali za hisia za mtu. Kitengo hiki cha saikolojia pia kinahusiana na uhalisia kwa vile ambavyo kinajaribu kufafanua misukumo inayowafanya wahusika kutenda wanavyofanya.Uhakiki wa uchanganuzi nafsia umewekewa msingi wake na mawazo yake kutokana na Mwanasaikolojia wa Austria, Sigmund Freud. Baadaye mawazo yake yaliungwa mkono na wanataaluma wengine ambao ni Karl Gustav Jung na Jacques Lacan .

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) Freud alitumia neno *Psychoanalysis* kwa mara ya kwanza katika mwaka wa 1896. Freud (1915) anafafanua mambo matatu makuu yanayoongoza maisha ya binadamu kama mahitaji, matamanio na wasiwasi. Mahitaji hushughulikia anasa hasa za kingono. Wasiwasi ni woga na mashaka kuhusu ufanisi au kutofanikiwa katika maisha. Miongoni mwa

mambo haya matatu, Freud anaeleza kuwa matamanio ndiyo humwongoza binadamu. Nadharia hii ina mikondo mingi. Hata hivyo, inayojulikana sana na uhakiki wa fasihi ni ile inayotokana na fikra za Freud, Karl Gustav Jung na Jacques Lacan.

Freud na Jung walikuwa wakiwasiliana na kushirikiana katika utafiti wao kabla ya kutofautiana na baadaye kutengana mwaka wa 1913. Freud na Jung walishikilia misimamo kinzani kuhusu ufasiri wa matukio yaliyopita katika maisha ya mhusika jambo ambalo lilisababisha utengano wao. Waitifaki wa nadharia hii wanashikilia kuwa utamaduni wa binadamu ulingana na wanadamu wengine waliokuwepo kabla ya miaka mingi iliyopita. Jung ana maoni kuwa, japo utu wa binadamu ni wa kibinafsi, binadamu huyo huathiriwa na jamii inayomzunguka. Ni muhali kukwepa athari ya jamii hiyo. Mhakiki anayetumia nadharia hii ya kisaikolojia sharti ainishe vikale vinavyopatikana kwenye sanaa husika na vilevile kuonesha umuhimu wa vikale hivyo katika ujenzi wa sanaa hiyo.

Lacan ni mhakiki wa kisaikolojia aliyeathiriwa na mkondo wa Umuundo Leo au 'baada umuundo'. Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba Lacan anaelekea kuingiza mawazo ya Kimuundo na kuzua kile kinachoweza kuelezeka kama Saikolojia Changanuzi ya Kimuundo. Lacan anatalii nadharia yake ya kisaikolojia kuanzia mahali Freud alikomea. Anaafikiana na Freud kuwa ndoto huwa zao la migogoro tofauti inayomkabili mhusika na ambayo kusumbuliwa kwake kunaweza kusuluhisha migogoro hiyo.

Lacan anaziona ndoto za mhusika kama lugha inayoweza kutafsiriwa kwa ajili ya kujua hali yake. Anadai kwamba uhusiano unaopatikana kati ya lugha na saikolojia ni kitengo cha lugha kinachomwezesha binadamu kujifafanulia uwezo alionao wa kutenda na mtazamo wake kuhusu maisha. Mtazamo wa Lacan unaweza kumhurutisha binadamu akapata uwezo wa kujiamulia anavyotaka na anavyofikiria.

Utafiti huu ulizingatia mkondo wa Freud(1900) alipoandika makala kuhusu ufasiri wa ndoto. Alihamasishwa kuandika kuhusu mada hii kutokana na mtagusano wake mkubwa na wagonjwa wa kisaikolojia. Aghalabu wagonjwa hawa waliishia kuwa na hali za pekecho, fadhaa na kiwewe cha kiwango cha juu. Freud alitahimidi historia ya mgonjwa na ugonjwa wake kutokana na uzindushi wa ung'amuzi bwete na mshiriki anayehusika. Wamitila (2003) anaueleza ung'amuzi bwete kama sehemu ya akili ya mtu inayohodhi fikra, mawazo, hofu na mitazamo hasi isiyoweza kukubalika katika jamii. Hofu na mawazo hayo hujitokeza katika ndoto. Kulingana na Freud, ndoto ni kichochoro kinachomwezesha mchunguzi nafsi kuufikia ukweli kamili wa maisha ya mwotaji husika.

Freud anailinganisha kazi ya fasihi na ndoto. Kwa vile riwaya, tamthilia na ushairi ni kazi bunifu, kazi hizi huashiria matumaini na matamanio ya mwandishi. Nao wahusika wanaopatikana katika fasihi ni wanadamu wanaoishi katika ndoto na njozi za mwandishi. Hawa ni kama vile wanadamu wanaoshirikiana na mwandishi katika matarajio na matatizo yake. Aidha, anaiona kazi ya fasihi: maudhui yake, mtindo na wahusika wake kuwa ndoto

inayoweza kumliwaza anapoipitia. Vitengo hivi vya fasihi humwathiri msomaji kikweli licha ya kwamba anayoyasoma ni ya kubuni.

Kulingana na fikra za Freud, inakusudiwa kuwa mhakiki anatazamiwa kuichanganua kazi ya fasihi kwa nia ya kubainisha bayana saikolojia ya mtunzi. Msomaji anaweza kujisoma katika maandishi anayoyasoma. Kutokana na usomaji, msomaji anaweza kuililia au kusherehekea pamoja na nafsi yake. Aidha anaweza kuonyesha uafikiano uliopo kati ya tajriba zake na tajriba za wahusika anaokabiliana nao.

Freud anathibitisha kwa shauku kuwa wahusika katika kazi ya fasihi hukua na kubadilika kutokana na misukumo mbalimbali ya maisha yao. Pia, nadharia hii inamhamasisha mhakiki wa fasihi kutilia maanani mshikamano uliomo katika kazi ya fasihi hata ile ambayo sentensi zake hazionyeshi muwala na mshikamano waziwazi.

### 1.8.1 MIHIMILI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ni:

i) Msanii huathirika na mazingira anamoishi hivi kwamba atakapoiandika kazi ya kifasihi atakuwa kama anaeleza imani, ndoto na tamaa zake. Mhimili huu utatumiwa kuthibitisha kuwa waandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* wanaathiriwa na mambo yale wanayopitia katika jamii na hivyo wanayashughulikia kama maudhui katika kazi zao.

ii) Kuna uhusiano kati ya Saikolojia Changanuzi na mtindo katika kufafanua hali halisi ya maisha ya binadamu. Mhimili huu utathibitisha jinsi wahusika wendawazimu wamefaulisha kukuza mbinu za uandishi katika riwaya teule.

iii) Kazi ya fasihi huonyesha mwandishi amebeba mizigo gani moyoni na analenga uchafu gani katika jamii. Kwa mujibu wa Freud kazi ya fasihi ni chombo cha mtunzi cha kuyalipulia majipu yaliyomlemea. Mhimili huu umefanikisha kufafanua jinsi wahusika wendawazimu wamefaulisha dhamira ya waandishi wa riwaya teule. Wamesawiriwa kama kipaza sauti cha kukashifia wahusika ambao japo akili zao ni timamu wanafanya maovu,kukandamiza wananchi na kukiuka haki zao katika jamii.

### 1.9.1 MUUNDO WA UTAFITI

Huu ni utafiti wa kimaelezo. Kwa hivyo muundo huu ulitumiwa kufafanua nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya zilizoteuliwa kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uchanganuzi-nafsia.

### 1.9.2 MAHALI PA UTAFITI

Utafiti huu ni wa maktabani ambapo mtafiti alisoma na kuchanganua kwa kina matini. Mbinu hii ilitumika ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Aina mbili za data zilikusanywa ambazo ni data ya msingi na data ya upili.

Kwa mujibu wa Kothari (2004), Data ya msingi ni ile inayokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo basi ni data halisi. Data hii ya msingi haijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa mara ya kwanza. Data hii ilikusanywa kutoka katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Riwaya hizi zilichanganuliwa kwa kina.

Data iliyokusanywa na kuchapishwa au kuandikwa na watafiti wengine ndiyo data ya upili kulingana na Kothari. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data ya upili kutoka machapisho mbalimbali ya waandishi. Data ya upili ilichangia kudhihirisha data ya msingi. Katika hali hii, ilisaidia katika na kufikia lengo la utafiti huu. Data hii ilipatikana baada ya kusoma makala mbalimbali maktabani kama vitabu, majarida, makala, magazeti na mtandao ili kupata data iliyofaa ya mada ya utafiti katika riwaya zilizoteuliwa kwa kuzingatia misingi ya nadharia teule. Vitabu vinavyofafanua nadharia ya uchanganuzi nafsia vilisomwa ili kubainisha mihimili iliyoongoza kuchanganua data ya utafiti. Tafiti zilizotangulia zinazohusiana na nafasi ya wahusika wendawazimu zilichunguzwa ili kupata data iliyoufaa utafiti huu.

### 1.9.3 UTEUZI WA SAMPULI.

Katika utafiti huu uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksuudi. Uteuzi huu pia hujulikana kama uteuzi shahada au uteuzi lengwa. Uteuzi shahada ni ule unaohusisha hali ambapo mtafiti huchagua kundi fulani la watu,vitu au dhana analoamini kimaksuudi kama linalofaa utafiti wake. Ni utafiti usiokuwa na shaka kwa kuwa hutoa majibu ya uhakika (Kombo na Tromp, 2006). Kazi

teule za fasihi andishi ya Kiswahili ziliteuliwa. Mtafiti alitumia uteuzi huu ili kupata riwaya mbili alizoziteua kuzishughulikia. Riwaya hizo mbili ni *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume.*

Uteuzi huu pia ulitumika kuteua kundi maalum la watafitiwa kulingana na mada ya utafiti.Wahusika wendawazimu katika riwaya hizi ambao ni Matuko Weye na Bilal ndio wameteuliwa ili kutoa data zitakazojibu maswali ya utafiti kuafikiana na malengo ya utafiti huu. Data nyingi katika utafiti huu ilipatikana kutoka katika riwaya zilizoteuliwa.Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksuudi kutokana na jinsi ambavyo wamewasawiri wahusika wendawazimu ili kuwasilisha maudhui, mbinu za uandishi na dhamira yao.

Kadhalika,uteuzi wa riwaya hizi ulifanywa kimaksuudi baada ya utafiti wa awamu ya kwanza ambapo mtafiti alisoma riwaya mbalimbali za waandishi hawa kwa lengo la kubaini ni riwaya zipi ambazo zingetosheleza malengo ya utafiti na kumwezesha mtafiti kupata data ya kutosha.

Riwaya hizi ziliteuliwa kama sampuli kwa kuzingatia kigezo kuwa wahusika wendawazimu wametumiwa na waandishi kama vipaza sauti katika riwaya husika.Zinamulika mambo yanayotukia katika jamii ya kisasa na zitawakilisha kikamilifu mtazamo wa waandishi hawa kuhusu suala la wahusika wendawazimu.

### 1.9.4 UKUSANYAJI WA DATA.

Buliba na wengine (2014) wanaeleza kuwa data ndiyo malighafi ya utafiti. Hii ni kwa sababu data hiyo ndiyo hutumika kujibu maswali ya utafiti. Hatimaye,

data hiyo hupangwa kwa kuihariri, kuiainisha na kuitenga kutegemea vigezo vya mahusiano mtafiti alivyojiwekea. Mbinu ya uchambuzi wa makala maktabani, mtandaoni na usomaji wa riwaya teule ilitumiwa katika ukusanyaji wa data ya utafiti huu. Kwa vile utafiti huu ni wa kimaelezo ulifanikiwa ulipofanyika maktabani kwa kuwa vitabu, machapisho, makala na tasnifu zinazohusiana na mada ya utafiti zilipatikana kwa urahisi kwa kuwa huhifadhiwa huko. Adam (2014) anaunga mkono hoja hii anapoeleza kwamba maktabani mtafiti hupata data ya kutosha kwa urahisi na zaidi ya hayo, hupunguza kiwango cha gharama kwa mtafiti.

Mtafiti alikusanya aina mbili za data ambazo ni data ya msingi na data ya upili. Kwa mujibu wa Kothari (2004), Data ya msingi ni ile inayokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo basi ni data halisi. Data hii ya msingi haijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa mara ya kwanza. Data hii ilikusanywa kutoka katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Riwaya hizi zilichanganuliwa kwa kina.

Kothari anaendelea kufafanua kuwa data ya upili hutokana na kazi za watafiti wengine. Utafiti huu ulifaidi kutokana na tasnifu, makala na machapisho ya watafiti wengine. Data ya upili ilichangia kufanikisha lengo la utafiti huu kwa vile ilithibitisha data ya msingi. Vitabu vinavyofafanua nadharia ya uchanganuzi-nafsia vilisomwa ili kuthibitisha mihimili inayoongoza uchanganuzi wa data ya utafiti. Tafiti zilizoandikwa kuhusu mada hii

zilichunguzwa kwa kusudi la kupata data iliyofaa ambayo ilidondolewa na kunakiliwa.

Utafiti huu ulifanyika kutokana na kusomaji na kuhakiki kwa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Hii ni mbinu ya ukusanyaji wa data iliyosaidia kupata data iliyohusu mada ya utafiti. Katika usomaji wa sura na aya zilizokuwa na matini iliyofafanua kwa kina kuhusu wahusika Matuko Weye na Bilal mtafiti alinakili matini yote iliyohusiana na malengo ya utafiti. Hatimaye, baada ya kusoma matini iliyoteuliwa kwa kina,data ilichambuliwa Mbinu hii imetumika katika ukusanyaji wa data ya msingi na pia data ya upili.

### 1.9.5 UCHANGANUZI WA DATA

Buliba na wengine (2014) wanafafanua kuwa uchanganuzi wa data hufanyika kwa njia mbalimbali kutegemea aina ya utafiti unaohusika. Kwa vile utafiti huu ni wa kimaelezo ulijikita katika uchanganuzi wa hoja za mtafiti. Ithibati zake zilitokana na matini kutoka katika riwaya teule. Data ya utafiti huu ilipokusanywa ilichanganuliwa kufuatia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Adam (2014) hii ni mbinu ya uchambuzi ambayo huidhinisha mtafiti kusoma au kuisikiliza kazi ya fasihi, kufahamu maudhui, mtazamo na falsafa ya kazi hii miongoni mwa mambo mengine muhimu. Matumizi ya mbinu hii pia huhusisha uchanganuzi wa lugha iliyotumiwa na mwandishi. Jambo hili humwezesha mtafiti kutoa maelezo ya kina kuhusu data iliyokusanywa kwa njia inayofanikisha kutoa majibu ya maswali ya utafiti wake.

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili mitatu ya nadharia ya Uchanganuzi Nafsia.

### 1.9.6. UWASILISHAJI WA MATOKEO

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalizingatia ufafanuzi wa nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya teule. Uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule.

## 1.10 HITIMISHO

Sura hii ilishughulikia utangulizi wa tasnifu. Ilifafanua usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia ya utafiti na mbinu za utafiti. Mbinu za utafiti zilijumlisha:muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Sura ya pili imeshughulikia mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui ya riwaya teule za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*.

# SURA YA PILI

## MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUFANIKISHA MAUDHUI YA RIWAYA ZA *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA *MKAMANDUME*

### **2.0** UTANGULIZI

Sura hii inalenga kuchunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui katika riwaya teule za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Ili kufaulisha jambo hili, dhana ya uhusika na wahusika katika fasihi na sifa za wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* zimefafanuliwa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi za fasihi walio na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa zinazotambulishwa na wanayoyasema, wanayoyatenda na pia maelezo ya mhusika au msimulizi. Wafula (2007) anaeleza kuwa msanii huathirika na mazingira anamoishi hivi kwamba atakapoiandika kazi ya kifasihi atakuwa kama anaeleza imani, ndoto na tamaa zake. Kwa hivyo, ili kuelewa malengo ya waandishi na sababu zao za kutumia wahusika wendawazimu katika kuendeleza maudhui, mhimili huu utatumiwa kuthibitisha kuwa waandishi wa riwaya hizi wanaathiriwa na mambo yale wanayopitia katika jamii na hivyo wanayashughulikia kama maudhui katika kazi zao. Ili kufaulisha dhima hii,

waandishi wamewafinyanga wahusika wake kwa jinsi ambayo watatimiza wajibu huu.

Katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* waandishi wamewahusisha wahusika wendawazimu ambao ni Matuko Weye na Bilal kama vipaza sauti vya kuyaeleza maudhui ambayo watu wanachelea kuyaeleza waziwazi katika jamii kama vile uongozi mbaya, udhalimu na unyanyapaa miongoni mwa mengine.

## 2.2. UHUSIKA NA WAHUSIKA KATIKA FASIHI.

### 2.2.1. DHANA YA UHUSIKA

Uhusika ni mbinu inayotumiwa na mwandishi wa fasihi kuwatambulisha wahusika. Athari inayotolewa na matukio ndiyo huwa na uzito katika fasihi na huleta matokeo mengi ya kazi inayowasilishwa. Uhusika pia ni hali ya kufananisha vitendo vya  wahusika katika fasihi na viumbe wanaopatikana katika ulimwengu halisi (Nyamari,2016).

Wahusika wa zamani walisawiriwa kihalisi. Walifanana kitabia na binadamu waliopatikana katika ulimwengu halisi (Njogu na Chimera,1999). Wawili hawa wanaendelea  kueleza kuwa wahusika hugawika katika makundi mawili makuu kulingana na namna wanavyotokea katika kazi fulani. Kuna wahusika wa kihalisia na wale wa kifantasia. Sifa za mhusika wa kihalisia hushabihiana na zile za binadamu wa kawaida ilhali zile za mhusika wa kifantasia hukosa ukawaida. Fasihi ya kijonzi huelezea kuhusu matukio yasiyo ya kawaida.

Mawazo ya kijonzi huwa ya kiwango cha juu kabisa. Sifa hukuzwa kuliko kawaida.

Nao Ndalu na wengine(2014) wanaeleza kuwa uhusika ni ile hali ya kuwasawiri watu au viumbe katika kazi za kinathari na za drama. Usawiri huu unaweza kuwa wa moja kwa moja kama kuwapa wahusika sifa kulingana na maumbile au kwa njia isiyo ya moja kwa moja yaani kisanii kwa kuchunguza matendo,maneno, yanayosemwa kuwahusu na mengineyo. Kwa kuwa ni viumbe wa kubuniwa na mwandishi hawaonekani bali kwa hisia tu, wale tunaowaona waigizapo jukwaani ni wawakilishi wa wahusika jinsi walivyosawiriwa na msanii. Msanii huwatumia wahusika kama vyombo vya kuuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji au watazamaji.

Mambo yatendwayo na wahusika katika kazi za fasihi ni yale ya kawaida katika maisha yetu. Hulingana na kazi za watu, tamaduni zao, tabia zao, migogoro itokeayo maishani mwao, hisia zao na mazingira yao kwa jumla. Hii ni kwa sababu fasihi huhusiana na jamii ya binadamu. Endapo mwandishi atatumia wahusika ambao si binadamu, atajitahidi na kuwapa uwezo na sifa za binadamu. Katika hali hii, atakuwa ametumia mbinu ya uhuishi/tashihisi. Kwa hivyo, wahusika ni kipengele mojawapo na muhimu cha fani.

### 2.2.2 DHANA WA WAHUSIKA.

Culler (1975) anafafanua uhusika kama kipengele cha msingi katika riwaya. Kulingana naye, matukio yaliyomo katika riwaya hunuia kufafanua kuhusu mhusika na maendeleo yake. Barthes anatoa kijelezo cha mhusika kama kitu kilichochorwa katika fikra au kwa kutumia maneno kulingana na vielelezo

vya kiutamaduni ili kumwezesha mhusika wa fasihi ya jamii fulani kueleweka vizuri katika jamii hiyo.

Kwa mujibu wa Madumulla (2009), anamtazama mhusika kama picha inayochorwa na fasihi na kuwa chanzo cha vitu vyote vipya zikiwemo dhamira na mada katika fasihi. Kadhalika anafafanua dhana ya uwili katika usawiri wa mhusika ambapo kuna usawiri wa kisanaa na wa sura ya mtu. Ufafanuzi huu unashadidia hoja kuwa wahusika si watu halisi bali watu wa kubuni. Ubunifu wa msanii humwezesha kuwaumba au kuwasawiri wahusika kinafsia, kiakili na kimwili. Usawiri wa wahusika unaofanywa na msanii hutegemea mbinu mbalimbali ambazo msanii huyo amezitumia.

Kadhalika, mhusika anarejelewa kama mtendaji katika kazi ya kifasihi. Ni kielelezo cha viumbe walio duniani japo si sharti sifa zote za mhusika zifanane na zile za binadamu (Wamitila,2008). Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa wahusika ni viumbe wanaotumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi kubeba na kuwasilisha ujumbe katika kazi husika.

Kimsingi wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi. Viumbe hivi vinaweza kuwa watu, wanyama, mimea, majini na kingine kile ambacho hupewa uhai na uwezo wa kutenda na mtunzi wa kazi ya kisanaa.Viumbe hivi ndivyo huipa kazi ya sanaa uhai kwani ndio watendaji na kwa namna hii huunda ulimwengu hai wa hadithi husika. Katika mtazamo wa kihalisia, hawa viumbe huakisi hali halisi katika ulimwengu wa binadamu, ingawa uhalisia unaorejelewa hapa si wa moja kwa moja (Hawthorn,2010 na Senkoro,1983 )

Viumbe hawa hubadilika kulingana na mabadiliko yanayokumba binadamu katika ulimwengu halisi. Hivyo uwasilishaji wao pia hubadilika ili kulandana na mabadiliko haya. Msingi wa mabadiliko haya huweza kuwa ni ukweli kwani ni vigumu kumfahamu binadamu kwa kila hali kwani kila wakati binadamu hubadilika. Hata hivyo mabadiliko ya uwasilishaji wa wahusika yanaweza pia kuongozwa na maendeleo katika uwanja wa usanii hasa riwaya (Hawthorn, 2010)

Kimaro (2014) anaeleza kuwa ili kuwasawiri wahusika kikamilifu katika kazi ya fasihi, wasanii huwatumia wasimulizi horomo na wasimulizi penyezi. Msimulizi horomo ni yule anayetoa taarifa kuhusu anavyowaona wahusika, wanavyosema na wanavyotenda bila kuwaingilia katika maoni yao. Naye msimulizi penyezi ni yule anayeweza kuona na kufahamu fikra za wahusika na kisha kutoa maoni yake kuwahusu. Wahusika hawa hupatikana zaidi katika tamthilia.

Wahusika hushabihiana na watu kwa kuwa fasihi huandikwa kwa ajili ya watu na kwa hiyo huwahusu watu hao. Kwa kawaida wahusika si watu halisi, bali ni matokeo ya ubunifu wa msanii ili kuakisi masuala kadhaa ya kijamii ambayo msanii ameyakusudia. Ni viumbe wa kubuni wanaotokana na fantasia, mwigo na kumbukumbu. Ni watu bandia wasio na damu na nyama. Mhusika si binadamu lakini anafanana na binadamu. Hana akili, haiba,itikadi wala uwezo wa kutenda bali ana sifa zinzomwezesha kumtolea maelezo ya kisaikolojia na kiitikadi (Bal,1997)

Mwandishi anapoumba wahusika wake anaumba watu wasioishi katika ulimwengu wetu bayana , bali wenye kuishi katika ulimwengu wao wa hadithi au tamthilia ambamo wakitolewa watakuwa hawana maisha (Mohamed,1995,uk.72)

Kulingana na ufafanuzi uliotolewa kuhusu wahusika, basi imedhihirika kuwa katika kazi ya fasihi, wahusika ni watu wanaowakilisha tabia za binadamu katika maisha halisi. Katika hadithi za mapokeo na baadhi ya hadithi fupi, wahusika wakuu kwa desturi huwa wadudu, wanyama, mimea, miungu, mashetani, na wengineo. Kitabia wahusika hao hugawika katika makundi makubwa mawili ya ubaya na wema.

### 2.2.3. DHANA YA USAWIRI

Ponera (2014) anafafanua usawiri wa wahusika kama hali ya kuwachora, kuwafafanua, kuwatambulisha na kuwajenga wahusika. Jambo hili hufaulu kufuatia uteuzi wa maneno,matendo, hadhi na uwezo unaoafikiana nao. Watunzi hutumia mbinu mbalimbali katika kusawiri wahusika katika kazi zao. Wamitila (2002) anafafanua kuwa mwandishi anaweza kutumia njia kadhaa na tofauti katika kuwasawiri wahusika wake. Msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuiteua namna ya kuwawasilisha wenyewe. Kama wasomi na wahakiki wa fasihi tunategemea sifa kadhaa kuwaelewa wahusika hao: maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusik wengine na kadhalika.

### 2.2.4. WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA RIWAYA.

Dhana ya wendawazimu imefafanuliwa na wataalamu mbali mbali.Wade na Tavris (2011) wanaeleza wendawazimu kuwa tabia au hali yoyote inayosababisha msongo wa kihisia unaomfanya mtu kuteseka, unaodhuru au usiokubalika na jamii.Kulingana na wawili hao, wendawazimu kwa mtazamo wa kisanii umetumika kama njia ya uhakiki kwa namna tatu: kwanza, mwandishi kusawiriwa kuwa mwendawazimu. Pili, wahusika kusawiriwa kama wendawazimu na mwandishi na tatu, kuna njia ya uhakiki ambayo istilahi za Kisaikolojia zinazotokana na utafiti wa kitabibu kuhusu wendawazimu zinatumika kueleza wendawazimu wa kisanii.

#### 2.2.4.1.Mwandishi kusawiriwa kama mwendawazimu

Wade na Tavris (keshatajwa) wanahusisha mtazamo huu na Plato na waandishi wengine wa Kirasmi na inadai kuwa waandishi wa kazi za kubuni ni wendawazimu, wao huendeshwa na nguvu zisizodhibitika za kiungu na hawana fikra timamu. Hata hivyo, mtazamo huu umepingwa na utafiti wa Porter unaothibitisha kuwa magonjwa ya kiakili yanaweza kuathiri uwezo wa kubuni.

#### 2.2.4.2. Kuhusu wahusika waliosawiriwa kuwa wendawazimu

Waandishi huwasawiri wahusika wakiwa na mienendo au tabia zisizo za kawaida kwa sababu kadhaaama vile kueleza yaliyo katika fikra zao/ migogoro ya kinafsi na pia kuelezea hisia za binadamu. Wahusika kama Hamlet, Antigone, Underground man, Gregor, Samsa Edner Pontellier wamefafanuliwa kama wendawazimu kwa mujibu wa jamii wanazotoka. Kuna jinsi tatu ambazo wahusika wendawazimu hujitokeza katika za fasihi. Kwanza, mhusika anaweza

kuwa mwenda wazimu kama Ophelia, mhusika Macbeth, Mfalme Lear miongoni mwa wengine. Mhusika anaweza kuwa na sifa zinazothibitisha dosari za Kisaikolojia kama msongo wa akili.

Pili, kuna wahusika waasi ambao wanapinga kanuni dhalimu za jamii kwa kuonekana wendawazimu au wenyewe kurukwa na akili kama mhusika Edgar katika hadithi ya mfalme Lear au katika mapambano ya Murphy dhidi ya makazi ya wagonjwa wa akili katika makala ya Rieger (1994).Wendawazimu wa wahusika hawa hutuwezesha kuwaelewa wahusika wenyewe na pia hufichua mengi kuhusu jamii husika.

Tatu, wahusika wanaweza kukengeuka na hali hii iwatenganishe na jamii kama ilivyotukia kwa mwanamke msimulizi katika hadithi fupi ya Charlotte Perkin Gilman. Ukengeushi huu unawatenga wanajamii katika jamii yenye watu wanaoishi maisha kulingana na matakwa ya jamii husika. Aghalabu, mwandishi hushirikisha wahusika wendawazimu kisanii kukejeli jamii na pia matendo ambayo wanajamii hutenda yanayosababisha wahusika wake kurukwa na akili.

Rieger (1994) anafafanua maswala nyeti kuhusu dhana ya wendawazimu katika fasihi. Mathalani, maana yake, mchango wake katika kuelewa fasihi, dhana ya waandishi wendawazimu na matendo ya wahusika wendawazimu. Ameshughulikia uhusiano kati ya wendawazimu katika fasihi na ule unaoshughulikiwa na matabibu wa kisaikolojia, mchango wa istilahi za kisaikolojia katika kutuwezesha kuwaelewa wahusika katika fasihi, mtazamo wa wanajamii kuhusu wendawazimu na mustakabali wa dhana za

wendawazimu. Kadhalika, anaeleza kwamba yeyote anaweza tambua sifa za wendawazimu sababu matukio mengi yaliyokiuka maadili yanabainika barabara yakilinganishwa na yale ya wenye akili timamu.

Mtaalamu huyu anasema kuwa hakuna jambo linalotenganisha wendawazimu na urazini barabara.Katika makala yake anachunguza wahusika wa kisanii ambao mitazamo yao ni kinyume na maadili ya kijamii na tabia zao zinapinga urazini. Wahusika kama Oedipus, Antigone, Edna na Underground Man wanaoonekana kuwa wendawazimu na wanajamii hutokea kuwa wahusika wenye akil razini zinazopiku kipindi cha kihistoria wanachoishi.

Rieger anaendelea kufafanua kuwa wahusika hawa husema ukweli mchungu ambao wanajamii wanahofia kusema na hata wakati mwingine wasioutilia maanani. Wahusika hawa huchukua nafasi ya waasi au wanaopinga udhalimu katika jamii. Waandishi huwasawiri wahusika hawa kama watu ambao wamejitenga au wametengwa na jamii ama kwa kutaka, kwa kulazimishwa, kuugua au inapofaa.Wao huwasilisha maadili ambayo wanajamii huyachukulia kuwa muhimu na ambayo wahusika hawa huasi kupitia kwa maisha, imani au matendo yao. Matatizo haya ya tabia za binadamu yameshughulikiwa sana katika kazi za Wamarekani. Hali hii ya wahusika kuwa na kichaa kinachowafanya kufurahia mateso imefafanuliwa katika makala ya Fiddick katika mhusika Underground man ( Rieger,1994,uk.89)

**2.2.4.3. Istilahi za Kisaikolojia zinazotokana na utafiti wa kitabibu kuhusu wendawazimu zinavyotumiwa kuelezea wazimu wa kisanii.**

Istilahi za kisaikolojia zinaweza kunukuliwa kutoka kazi za Freud, Jung, Horney au hata wananadharia wengine wa kisasa ama zitokane na maelezo halisi kama yale ya namna ya DSM 111. Fasihi na Saikolojia ni taaluma mbili zinazotegemeana kwani zote huchangia katika kuelewa tabia za watu. Ndiposa uchunguzi kuhusu mada ya wendawazimu katika fasihi unachangia kumaizi tabia za wanadamu.

Uhakiki wa kisaikolojia umekuwa nguzo muhimu hasa wakati wa Freud na ungejikita katika mwandishi, uandishi, matini au msomaji wa kazi husika.Licha ya mtazamo wa Ki-freud, msukumo wa tatu wa Kisaikolojia umetumika katika uhakiki wa kisaikolojia.Msukumo huu wa tatu hurejelea Saikolojia inayohusiana na ubinadamu unaoshirikisha kazi za Carl Rodgers, Abraham Maslows na Karen Horney wanaotoa mchango mbadala wa Utabia na Uchanganuzi Nafsia. Jambo hili ni la muhimu na la kuleta matumaini kuliko njia za kijadi na Saikolojia ya Kisayansi.

Uhakiki wa Kisaikolojia unaohusisha mitazamo ya Ki-Freud, Ufreud mpya, Jung, msukumo wa tatu wa Kisaikolojia, Lacan na njia nyingine za Uchanganuzi Nafsia za kufasiri fasihi umeshamiri sana. Kwa mfano, Debra (1998) anafafanua haya akirejelea kazi ya Berman inayochunguza jinsi waandishi wa leo hutumia Uchanganuzi Nafsia kuchunguza wahusika katika fasihi. Berman huchunguza uhusiano baina ya ubunifu na masuala ya Utabibu kwa kuzingatia jinsi wasanii wanaweza kujiponya wenyewe na kuwaponya

wengine kwa kubadili mateso kuwa kazi ya usanii. Anajadili baadhi ya dhana za kimsingi za uchanganuzi nafsia kama kuwalaumu wengine, uwili na ubinafsi.

Waandishi kama wendawazimu husawiriwa vizuri katika taaluma ya Elimujamii kwa mujibu wa tafiti nyingi zilizofanywa watafiti walithibitisha na kunukuu mifano halisi katika maisha yao. Aidha, mtazamo huu huungwa mkono na tafiti za wataalamu kama Freud, Jung, Rank na watafiti wengine katika taaluma ya Utabibu wanaosisitiza uhusiano kati ya ubunifu na hali ya kutokuwa na akili razini maishani mwa binadamu. Wao husisitiza kuwa wasanii hukiuka mipaka ya urazini ndiposa waweze kusimulia yaliyo katika sehemu ya ung'amuzi bwete akilini mwao, mengi ambayo ni yale waliyopitia wakiwa wadogo.

Mikatale ya kijamii kama unyanyapaa, kudhibiti tabia za wanajamii na nadharia ya utekelezaji wa majukumu huusawiri wendawazimu kama matokeo ya migogoro katika mahusiano ya kijamii (Debra ,1998) . Kulingana naye, hakuna kijelezo mwafaka cha wazimu. Toleo la nne la jarida lake linaeleza kwamba hakuna kijelezo kilichotolewa kinachotoa maana mahsusi ya magonjwa ya akili. Wengi waliojaribu kuelezea wanatoa maana inayotokana na chanzo cha wendawazimu wenyewe. Maelezo yao yanaweza gawika katika makundi matatu, japo makundi haya yanaingiliana.

Kundi la kwanza ni la kiunzi kinachoangazia jinsi ubongo wa binadamu hufanya kazi na ambacho hudhamiria kuchunguza chanzo cha kasoro zinazopatikana katika utendakazi wa akili. Chanzo cha kiunzi hiki ni sayansi

changamani ikilinganishwa na tafiti zinazohusisha vipengele vingine. Szasz anaeleza kuwa tafiti nyinginezo hazihusishi matokeo ya kiutafiti bali kadhia. Kulingana naye ugonjwa wa akili ni sawa na ugonjwa wowote unaoathiri mwili wa binadamu kwa hivyo kuuchukulia kama ugonjwa sugu ni kama fumbo. Udhaifu wa kiunzi hiki ni kuwa huzigeuza tajriba za watu kuwa wendawazimu .

Viunzi hivyo vingine viwili kimsingi huchunguza wazimu na chanzo chake. Mikatale ya kijamii kama unyanyapaa, kudhibiti tabia za wanajamii na nadharia ya utekelezaji wa majukumu huusawiri wendawazimu kama matokeo ya migogoro katika mahusiano ya kijamii. Viunzi vya kisaikolojia hasa vile vya Freud vya uchanganuzi nafsia hufasiri wendawazimu kama upotovu wa kiakili wa mhusika. kuhusu wendawazimu imegawika kimsingi katika makundi matatu. Viunzi vya kimapokeo vinavyofanana na vya kisasa vya magonjwa ya kiakili ni viunzi vya kitabibu vinavyotumikiza njia za kisayansi.

Debra (1998) anafafanua dhamira yake kuwa ni kuweka wazi chanzo cha ugonjwa huu ili kutia kikomo mitazamo mingi inayofafanua dhana hii. Yeye haamini kuwa kuna maradhi yanayosababishwa na nguvu za kiungu. Kulingana naye kila ugonjwa una chanzo na dalili zake. Hali ya wendawazimu kuwa tofauti na maradhi mengine ndiyo huufanya uonekane kama unatokana na nguvu za kiungu.

Anaendelea kufafanua kuwa, waganga wa mitishamba, waponyaji wa imani za kidini, madaktari wa kienyeji wa walaghai hudai kuwa wendawazimu ni

ugonjwa unaotokana na nguvu za kiungu. Wao hufanya hivi ili kuficha ujinga wao kuhusu kutofahamu kuhusu chanzo na tiba yake. Hata hivyo Hippocratics wanaweza kutoa maarifa yanayotokana na utafiti wa kisayansi kuhusu wazimu.

Japo mwandishi alijikita katika ugonjwa wa kifafa utafiti wake una uhusiano na mawazo kuhusu wendawazimu kwa kuwa hali zote mbili zilionekana kuhusiana enzi za kale kama inavyoelezwa katika wendawazimu wa mhusika mkuu katika Euripides Heracles. Katika mjadala wake kuhusu tafsiri ya kibayolojia ya chanzo cha wazimu, mwandishi anaeleza kuwa wendawazimu hutokana na unyevu wa akili zenye masumbufu. Ingawa wanasayansi wana uwezo wa kufafanua chanzo cha wazimu na maradhi yanayohusiana nao, wameshindwa kueleza jinsi wenye hali hiiwanavyohisi na kwa nini dalili zake zinatofautiana na kuajabisha.

Rieger (1994) alichangia utafiti wetu kwa sababu makala katika kitabu chake anafafanua dhana ya mwendawazimu kwa mitazamo mitatu. Miwili kati yake ni muhimu katika kuwasawiri wahusika wendawazimu na pia mtazamo wa kisaikolojia changanuzi uliojadiliwa kwani ndio ulioweka misingi ya nadharia ya utafiti wetu.Vilevile, makala yake yanafafanua uhusiano uliopo kati ya Fasihi na Saikolojia. Hata hivyo pengo lingalipo kwani kazi zilizorejelewa ni za fasihi ya Kiingereza. Utafiti wetu ulijikita katika riwaya teule za Kiswahili.

Makala ya Debra yana mchango muhimu katika utafiti huu sababu yanaangazia chanzo cha wendawazimu, dhana ya wahusika wendawazimu na uhusiano wa Fasihi na Saikolojia mambo haya ni muhimu kwa kuwa utafiti huu unaegemezwa katika nadharia ya uchanganuzi nafsia.

## 2.2.5.0 MCHANGO WA MHUSIKA MATUKO WEYE KATIKA RIWAYA YA *KIDAGAA KIMEMWOZEA*

Sehemu hii imeangazia nafasi ya mhusika Matuko Weye ambaye amesawiriwa na mwandishi kama mwendawazimu katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Imejadili sifa zake kama mwendawazimu na kufafanua jinsi anavyofanikisha kuwasilisha maudhui ya mwandishi katika riwaya kama vita dhidi ya udhalimu, ukombozi na uongozi mbaya.

### 2.2.5.1. MHUSIKA MATUKO WEYE ALIVYOSAWIRIWA KAMA MWENDAWAZIMU

Mhusika Matuko Weye amesawiriwa kama mwendawazimu na mwandishi. Hii ni kwa sababu mwandishi anaeleza kuwa siku ya sherehe ya Sikukuu ya Wazalendo, anajitokeza ghafla na kupanda jukwaani kwa haraka. Bila idhini au mwaliko alikitwaa kipaza sauti na kuhutubu kwa sauti ya kutisha yenye king'ong'o. (Walibora,2012,uk.71). Kadhalika, mwandishi anaeleza kuwa hakumiliki chochote. Hakuwa na shamba, au mke, mwana wala binti. Aliweza kulala popote pale. Alivaa kaptura juu ya suruali, zote mararumararu.

Mhusika huyu alipopewa chakula kinachohitaji kutowelea, alipenda kufagia kitoweo kikesha mwanzo kabla ya kuanza kukila chakula chenyewe. Ilmuradi alipopewa sima na mboga, kwanza alifyeka mboga zote zikaisha. Ndiposa akaanza kubugia sima kavu. Apewapo kuku na chapati hufukamia kuku ikesha ndipo ageukie chapati. Na kila apewapo chakula au kinywaji hula na kunywa na kuondoka bila shukrani wala rabsha. Akipenda kupiga kwata na kusema *marktime* na *about turn,left right* akili zake zilipompeleka miaka ya nyuma

huko alipokuwa jeshini. Alipata kutoa simulizi za vituko na visa vya vitani, simulizi ambazo nusu nyingine vifundiro vya akili yake chakaramu(Walibora,2012, uk.72-73).

Mwandishi anaendelea kutueleza kuwa baada ya kukamatwa na askari wa Mtemi na kuwekwa seli, Amani na Imani walimkuta huko. Sababu ya kutiwa ndani ni kuzua rabsha katika sherehe ya Sikukuu ya Wazalendo. Ajabu ni kuwa ndani alimolala mlikuwa na mnuko kama wa mfu au kitu kilichokufa lakini harufu hii haikumsumbua Matuko. (Walibora,2012, uk.83).

Askari wanapozidi kuwazomea Amani na Imani mizomeo inamwamsha mzee Matuko anayewaambia,

> "Sitaki kelele hapa kwenye ikulu ya Rais. Bado nalala na mwaniletea kelele". (Walibora,2012, uk.84).

Kwa kawaida, seli si pahali pa kujivunia mtu anapowekwa pale. Hali yake ni duni . Mtu mwenye akili zake timamu hawezi kulinganisha pahali hapa na ikulu ambapo ni pahali pa fahari na utulivu. Wapatikanao pale ni watu waheshimiwa, kama vile Rais. Katika kauli hii ni bayana kuwa Matuko anakejeli hali yake. Akiwa miongoni mwa Mashujaa waliopigana katika Vita vya Pili vya Dunia, inasadifu kuwa badala ya kumheshimu kwa kumtunza na kumpa hadhi katika Sikukuu ya Wazalendo wanavyofanya ni kumkamata na kumwaibisha hadharani.

Waliopigana vita hivi ndio waliochukua nafasi muhimu katika kuwaandaa wapiganaji wa Afrika katika kupigania uhuru kwani tajriba na motisha waliowapa Waafrika wenzao ni baadhi ya mambo yaliyofaulisha vita vya

Mwafrika dhidi ya Mkoloni. Alipolazimishwa kutoka seli 'ikulu' aliamka ghafla na kuondoka mbio huku anaboboja bo bo bo maneno yasiyoandikika wala kutamkika. (Walibora,2012, uk.87)

Kando na asemayo na atendayo, wengine pia wanamwona Matuko Weye kuwa mwendawazimu. Jambo hili linadhihirishwa na bintiye Mtemi ambaye ni Mashaka. Mwandishi anaeleza kuhusu Mashaka na kusema,

> "Alimpita mzee Matuko Weye, aliyekuwa amesimama tisti karibu na vyoo. Hili jina 'weye' kapewa kwa sababu hakosi kusema weye katika kila tamko lake. Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye shereze hizi? Anafikiria ni za watu wenye kichaa kama yeye? Mashaka alijiuliza mwenyewe, akakosa jibu. (Walibora,2012, uk.69)

Kwa mujibu wa Kimaro (2014) kuna njia mbili za kufahamu sifa za wahusika katika kazi za fasihi. Njia ya kwanza ni ya moja kwa moja au wazi ambapo mwandishi anawajuza wasomaji kuhusu mhusika. Hili linawezekana kupitia kwa msimulizi, mhusika mwenyewe au mhusika mwingine kama anavyofanya mhusika Mashaka anapomrejelea Matuko Weye.

Njia ya pili ni iliyo fiche au isiyo wazi. Hii ni ile hali ambapo wasomaji au hadhira inastahili kutathmini wahusika kwa kurejelea mawazo, kauli zao (jinsi wahusika wanavyozungumza, uteuzi wao wa maneno) maumbile yao, tabia zao, mtagusano wao na wahusika wengine miongoni mwa mambo mengine.

### 2.2.5.2 MCHANGO WA MATUKO WEYE KATIKA KUKUZA MAUDHUI

Msanii kama zao la jamii anapoandika kazi yake huwa na azma ya kueleza yale yanayotukia katika jamii. Ili kufaulu kufanya vile, yeye anaweza kueleza matukio hayo moja kwa moja au kutumia wahusika kuwasilisha ujumbe anaokusudia kuipasha jamii. Anapofanya hivi, wahusika hawa huwa ni kipaza sauti chake.Walibora alidhamiria kumtumia mhusika Matuko Weye kama kipaza sauti cha kueleza yanayomkera katika jamii. Amemsawiri Matuko Weye akiwa mwendawazimu. Katika hali hii anatekeleza jukumu la kukuza maudhui ya vita dhidi ya udhalimu, ukombozi na uongozi mbaya.

#### 2.2.5.2.1 VITA DHIDI YA UDHALIMU.

Matuko Weye analalamika kuhusu dhuluma zinazochangiwa na Bwana Mtemi. Anafafanua kuwa wamepokonywa mashamba, mali, mabinti na hata wake zao. Analalamika kuwa wananchi wanadhalilishwa. Kadhalika, akiwa seli analalamika kuwa hata baada ya kufungiwa anaachiliwa bila ya kufikishwa kortini.

> "Tumetoshwa.Weye mwananchi mlalahoi huoni hivyo, weye? Tumetoshwa na dhuluma za Bwana Mtemi. Anatudhulumu sana, sana. Anatupokonya mashamba, mali, mabinti na hata wake zetu wenyewe.' (Walibora,2012, uk.71)

Kauli hii ya Matuko ni ya kweli kwa sababu kupitia urejeshi mhusika Imani anamweleza Amani alichokuwa amepania kufanya pale Ziwa Mawewa na kwa nini. Anafafanua jinsi Askari walitumwa kuwaondoa katika shamba lao huko Baraka wakidai kuwa lilikuwa la mwenyewe. Mama yao alipokatalia katika shamba, alichapwa kichapo kilichosababisha kifo chake baadaye. Ajabu ni

kuwa hata mama yake alipotoa hatimiliki, askari walikuwa na nyingine waliyopewa na ‘mwenyewe’ (Walibora,2012, uk.53-55). Kakake Imani, Oscar Kambona aliondoka na kusema angerudi kwa moto na radi. Imani alimweleza Amani kuwa japo hakujua aliyewatuma askari hao, alidhani ndugu yake Oscar alimjua mtu huyo. Baadaye nyumba yao iliteketezwa moto akaona heri aende ajichupe katika Ziwa Mawewa. Ni dhahiri kuwa Mtemi ndiye kanyakua shamba lao. Amani anamkuta Mtemi na kimada wake Lowela wakiwa mikononi mwa Oscar na wenzake, bunduki mikononi akiwa tayari kulipiza kisasi kwa Mtemi.

> “Basi hili dude lazima litakufa leo yakhe”, alimwelekeza bastola Mheshimiwa Mtemi Nasaba Bora. Ati Nasaba Bora?Nasaba Bora gani hizo zisizoenda dobi zikatakata?”… sitalipiza leo. Lakini nitalipiza.Wasikia Bwana Nasaba mbaya Mbovu?’’ (Walibora,2012, uk .145-146)

Vita dhidi ya udhalimu vinajidhihirisha wakati ambapo Amani na Imani wanawekwa kizuizini kwa amri ya Mtemi kwa tuhuma za kukiua kitoto Uhuru. Matuko Weye anawatetea vijana hawa kwa kusema,

> “Ala bwan’mdogo hata weye ushaletwa humu ikuluni?…na hata kama umeua weye sasa nini?Weye askari njoo umfungulie huyu kijana aende zake weye. Au mnishitaki miye kwamba nimeua Eeh? (Walibora,2012, uk.84)

Ukweli ni kwamba kitoto kilifariki kutokana na ugonjwa wa kichomi kama Mwalimu Majisifu anavyomweleza kakake Mtemi Nasaba Bora, “Sitaki ujali maslahi yangu. Jali maslahi ya watu wengine wote wa Sokomoko. Huu ndio ubinadamu. Kama ungekuwa unajali maslahi ya wengine, yule mchungaji wako na mtumishi wangu hawangekuwa wanapigwa na baridi kule ndani kwa kosa ambalo hawakulitenda. Nimepata *first hand information* kutoka kwa

daktari aliyepima maiti ya kitoto hicho naye amesema kimekufa kwa ugonjwa wa kichomi, ambao ni kawaida kwa watoto. Wale vijana umewafunga ndani kwa nini?"

Matuko anapolalamika kuhusu kupokonywa mabinti anaongea ukweli uliopo.Barua ya Ben Bella kwa Mashaka inadhihirisha kuwa Lowela ana uhusiano wa kimapenzi na Mtemi. Uhusiano huu unamfanya Ben avunje ahadi ya kumwoa Mashaka na kufafanua wazi kuwa babamkwe hawezi kuwa shemeji. Ben anamweleza Mashaka:

> … "Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri. Aliniambia kuwa alipelekwa huko na mtemi Nasaba Bora. Alisema kapata mimba aliyoificha kwa kujifunga kamba tumboni wala wazazi wangu hawakuweza kugundua. Naye babako ndiye kamtunga mimba hiyo.Basi siku zake zilipokaribia babako alimtoa nyumbani kisirisiri na kumpeleka mtoto aliyezaliwa mlangoni kwa mchungaji wenu Sokomoko" (Walibora,2012, uk.81)

Vilevile,madai ya dhuluma hii ya kupokonywa kwa mabinti na Mtemi inadhidhirishwa na Lowela mwenyewe. Anasisitiza haya katika barua aliyomwandikia Mtemi anaposema:

> *Bwana Nasaba Bora,*
>
> *Nakupenda lakini kama ujuavyo, mahaba yangu ni ghali. Hii ni kwa sababu thamani yangu kubwa. Hebu litazame umbo langu, na umri wangu na haiba yangu. Je, kweli nalinganishika na Yule ajuza wako mwenye manyama tembweretembwere kama ya nguruwe? Nitaendelea kukuengaenga kwa mahaba yasiyokuwa na mfano mpaka ujisahau, lakini kwa masharti…* (Walibora,2012, uk. 105-106)

Kama Matuko alivyodai kuwa Nasaba Bora aliwanyang'anya mali, tunaelezwa kuwa baada ya Amani kuwaokoa na Lowela kutoka mikononi mwa majambazi, walipofika kwake na kumwambia Amani aombe atakalo, Amani

alisema kwa utulivu, "Bwana Mtemi, naomba unipe hatimiliki zote za shamba zilipo kwenye sefu" mikono ya Mtemi ilikuwa ikitetemeka alipotoa kwenye sefu rundo la hatimiliki za mashamba zilizokuwa katika bahasha moja kubwa. Alipompa Amani bila kusita akazikagua kwa makini hati zote moja baada ya nyingine. Hatimiliki zilikuwa za mashamba tofautitofauti katika janibu mbalimbali. Akathibitisha mambo aliyofichuliwa na amu yake Yusufu.

> "Mbona kuna hatimiliki mbili tofauti kwa kila shamba?''Amani aliuliza."Moja ni bandia na nyingine ni halali"alijibu."Kwa nini?" kimya kikajiri. "Kijana we' ni nani?" aliuliza Mtemi hatimaye. "Mimi ni mjukuu wa Chichiri Hamadi na mpwa wake Yusufu Hamadi uliowatenda uliyoyatenda."Mtemi alitikisa kichwa." (Walibora,2012, uk.149)

Imani anapomweleza Amani kuhusu kadhia iliyoipata familia yake anamwambia,

> "….halikupita juma moja baada ya mama kuzikwa nikanusurika kuteketezwa ndani ya nyumba yetu. Wanakijiji wa Baraka walichelea hata kukaribia kitende chetu. Nilipotoka katika nyumba ile niliona watu wa Baraka wanashughulika na hamkani zao na kunong'onezana. Hawakutaka kuonekana kana kwamba wananionea imani.Waliogopa, waliogopa kuwakinza waliotumwa kutupoka shamba letu halali. Kimya chao ndicho kinikeracho nikumbukapo mpaka leo. Yaani wanyonge wamekubali kutazama tu wenzao wakinyongwa vivi hivi" (Walibora,2012, uk.58).

### 2.2.5.2.2 UKOMBOZI

Ukombozi ni hali ya kunusuru watu kutoka matesoni au udhalimu wa aina fulani. Wanasokomoko ni watu ambao japo walipata uhuru kutoka kwa wakoloni, uhuru wao ulikuwa wa bendera tu. Mtemi wao anawanyanyasa zaidi ya walivyonyanyaswa na mkoloni mzungu. Matuko anafafanua haya

anapoeleza kuwa afadhali mkoloni mzungu kuliko Mkoloni mweusi kwani mweusi huwadharau wenzake vibaya na kuwatumia Waafrika Wenzake kama kopo la msalani (Walibora,2012, uk.85).

Matuko Weye aliwaeleza wananchi kuwa wangetaka kiongozi wao aondoke madarakani na kumfananisha na nduli kwa vitendo vyake dhalimu. Mhusika huyu amechoshwa na uongozi wa mtemi hadi anampachika jina ‘Mtemi Nasaba Mbaya’. Anamtahadharisha mtemi kwa methali isemayo, “Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi” (Walibora,2012, uk.72).

Katika riwaya hii kuna wahusika ambao nia yao ilioana na kauli ya Matuko Weye. Kwa mfano, mwanawe wa kiume Mtemi ambaye ni Madhubuti anamweleza mhusika Amani ya kwamba alikuwa ameamua kujiiua kinasaba na kuzaliwa upya kusudi asiwe na uhusiano wowote na nasaba ya Mtemi Nasaba Bora. Pia anapendekeza kuwa watu wengine nchini Tomoko walipaswa kujiiua kikabila na kujiiua kitabaka ili nchi yao iweze kupiga hatua za kimaendeleo. Maoni haya yanamfanya Amani kufahamu na kuhakikisha kuwa lengo lao lilikuwa moja, nalo ni kumwondoa mtemi madarakani.

> “Kama nakuelewa ndugu yangu,” alisema Amani hatimaye.Unataka kuleta mapinduzi” “Ndiyo, ili kuwazindua wanyonge wasiokuwa na chochote kingine wapotezacho ila minyororo yao iliyowafunga”.“Nimeitikia wito”, alisema Amani. “Tena nina sababu ya kibinafsi ya kuitikia wito, sababu inayoambatana na kuja kwangu kujikalifu katika ajira duni kwenye shamba la babako. Nitakueleza punde.Lakini sharti tutahadhari ndugu yangu”. (Walibora,2012,uk.119).

Nia ya Matuko Weye ya kupanda jukwaani na kutwaa kipaza sauti na kuhutubia watu ilikuwa ni moja: kuwazindua watu ili wapigane na utawala dhalimu wa Mtemi na wapate ukombozi wa pili. Anawaeleza kuhusu udhalimu waliotendewa na mtemi. Anaposhikwa na kuwekwa seli, akili zake hazijafungwa. Yeye anaunga mkono kauli ya mshairi Abdilatif Abdalla (1973) katika Shairi lake *N'shishiyelo ni Lilo* anaposema:

*Ubeti 15.* *Mno wanganiadhibu, adhabu kila namna*
*Na mangi yanganiswibu, ya usiku na mtana*
*Hayatakuwa sababu, ya kuniasa kunena*
*Kweli nitapoiyona, tanena siinyamai*

*Ubeti 16.* *Mateso yao yangawa, nda kuumiza mtima*
*Hayatakuwa ni dawa, ya kutonipa kusema*
*Ni bure wajisumbuwa, nilipo nnasimama*
*Si 'mi wa kurudi nyuma, kweli ilipo 'tasonga.*

Japo Matuko Weye ametiwa kizuizini, akili zake ziko huru. Anakabiliana na askari na kuwaeleza kwamba halikuwa jambo la haki kuwafungia Amani na Imani bila makosa.Anawalaumu na kuwafananisha na wendawazimu. Kadhalika anafananisha hali hiyo na mahakama kuwa na makossa nao washtakiwa wakiwa bila hatia. (Walibora,2012, uk.86)

Matuko weye anawasisitizia askari kuwa hatoki seli kama hajakunywa chai.

> Weye, nitoke na hata chai sijanywa? Mlinilet nao a hapa jana mkanilaza njaa. Mlinishikia nini kama sasa mwaniachilia? Kama mlitaka kunifikisha mahakamani, nifikisheni. Kama mlitaka kunipiga risasi nipigeni tu. Lakini hata mkiniua kumbukeni ya kwamba watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi toka pale nilipowachia. Waikomboe nchi hii ya Mwafrika kutoka kwa mkoloni mweusi. Ukoloni wa pili.. Walibora,(2012, uk.86-86).

Kutokana na maneno haya ni bayana kuwa Matuko weye anafahamu haki za wafungwa. Kwa mfano, anajua kuwa mfungwa anafaa kulishwa, mtu hafai kushikwa kama hana makosa yoyote na mtu ashikwapo anafaa kufikishwa mahakamani na ashtakiwe kwa makosa aliyoyafanya. Kwa hivyo, kulingana naye, kuachiliwa kwake ni ithibati tosha kuwa hakuwa na makosa/kesi ya kujibu, hivyo, alizuiliwa bila makosa na hiyo ni dhuluma-ukiukaji wa haki.

Kwa mujibu wa katiba ya Kenya 2010; Sura ya Nne, kifungu cha 49 ,haki za waliotiwa mbaroni zinaelezwa:

> *"Kila mtu aliyetiwa mbaroni ana haki ya kuarifiwa kwa upole na kwa lugha anayoielewa kuhusu sababu za kukamatwa, haki ya kunyamaza na matokeo ya kutonyamaza…kutolazimishwa kutubu au kukiri hatia, hali ambayo inaweza kutumiwa katika ushahidi dhidi yake;… kufikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo, lakini si baada ya saa ishirini na nne baada ya kukamatwa; …kufunguliwa mashtaka au kuarifiwa sababu ya kuendelea kuzuiliwa kwake,au kuachiliwa huru siku yake ya kwanza ya kufikishwa mahakamani"*

Matuko anapomweleza askari kuwa mama aliyemzaa alikosea wanadamu, nakuwa siku moja hata yeye atakuja kuongezewa jina marehemu (kuaga dunia) wakiwa na Mtemi wao Nasaba Mbaya-Mbovu. Anawaeleza kuwa kama mlitaka kunipiga risasi nipigeni tu. Lakini hata mkiniua kumbukeni kwamba watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi toka pale nilipowachia. Waikomboe nchi hii ya Mwafrika kutoka kwa mkoloni mweusi. Ukombozi wa pili" (Walibora,2012, uk.87). Maneno haya ni ithibati kuwa Matuko weye ana imani na matumaini makubwa kwamba sharti wananchi watakombolewa kutoka udhalimu wa wakoloni weusi, ambao ni viongozi waafrika waliotwaa mamlaka na uongozi baada ya uhuru lakini

badala ya kulinda haki na kuhakikisha raia wanapata maendeleo, wanawakandamiza huku wakiwadhulumu wenzao.

Anawaeleza kuwa watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi toka pale alipowachia. Hili linakuja kutukia kwa kuwa tunaelezwa kuwa Amani na Madhubuti walishirikiana kuleta mapinduzi kwa kusudi la kuikomboa Sokomoko kutoka kwa Mtemi. Walipigania ukombozi wa pili. (Walibora,2012, uk.87).

Baada ya mipango ya Amani na Madhubuti kufanikiwa,Amani anamtunukia Matuko Weye kasri ya Mtemi na kusema:

> "Alimpigania malkia wa Uingereza", "Ni nini alichopewa ila wehu na ukata? Na ni nini serikali ya Tomoko huru ilichofanya kumchonjomoa maskini mzee Matuko Weye? Acha aishi kwenye nyumba hii ya mzungu maadamu angali hai. Tutamtafutia daktari wa akili na wauguzi wa kumsaidia .(Walibora,2012, uk.156).

Matuko weye alipoyapata makao haya alifurahi sana. Hili ni thibitisho kuwa mhusika huyu alifurahia kupata makao ambao ni mojawapo wa mahitaji ya kimsingi kwa kila binadamu. Katika kumtunuku nyumba hii, Matuko Weye anapata nafuu na kuhifadhiwa kutokana na hatari ya kulala popote na kuathiriwa na hali mbaya ya anga usiku. Hii ni hatua ya mojawapo ya ukombozi kwani nyumba hii haikufaa kumilikiwa na kiongozi bali ilikuwa mali ya umma.

### 2.2.5.2.3. UONGOZI MBAYA.

Mtemi Nasaba Bora aliongoza wanasokomoko isivyofaa. Hii ni kwa sababu kama kiongozi anaunga mkono na kushiriki katika matendo

yanayowadhalilisha na kuwadhulumu wananchi.Matuko anamkumbusha askari kuwa hatimaye atakuja kuongezewa jina "marehemu" siku moja, yeye pamoja na huyo mtemi wao Nasaba Mbaya Mbovu. Matendo maovu ya mtemi ndiyo yaliyomfanya Matuko amrejelee kama Nasaba Mbaya Mbovu. Mathalani:

Amani na Imani waliteseka sana kutokana na uovu wake. Alipokuwa waziri wa ardhi alibadilisha hati za wamiliki halali na kughushi zake. Anatumia hati ghushi kudai sehemu hizo. Udhalimu huo ndio ulimfanya mamake Imani apigwe na Askari katili. Kipigo hicho kilisababisha kifo chake(Walibora,2012, uk.145)

Oscar Kambona kakake imani aliathirika na kitendo hicho na kutoroka nyumbani. Uovu huo uliotendwa kwa amri ya Mtemi ndio uliosababisha Oscar kuwa mhalifu na kutumia bangi kisha kufungwa jela (Walibora,2012:146)

Mtemi ndiye aliyepanga njama ya kuuawa kwa Chichiri Hamadi ili anyakue shamba lake. Kifo hicho kilibebeshwa mwanawe Yusufu baada ya kutekelezwa na majambazi waliotumwa na Mtemi. Hila hizo zilimfanya Yusufu afungwe jela kifungo cha maisha bila hatia (Walibora,2012, uk.149)

Mtemi alitumia mali ya umma kumpeleka mwanawe Madhubuti Urusi kusoma. Pia,alikuwa ameshatoa rushwa kwa wanajeshi ili akirudi apate ajira jeshini, ingawa Madhubuti alikataa kushirikiana na babake na kujitafutia ajira mwenyewe mjini Songoa.

> "Alaa, bwan'mdogo hata wewe ushaletwa humu ikuluni?" alimwambia Amani huku akichekacheka. "weye miye naweza kukufanya waziri wa ufisadi na magendo ukitaka. Lakini mwanzo sharti utoe kitu kidogo weye" . (Walibora,2012, uk.84).

Katika kauli hii Matuko Weye anakejeli hali ilivyo Sokomoko.Ili mtu afanyiwe jambo au apandishwe madaraka, sharti atoe kitu kidogo.Kwa mfano, kabla ya Madhubuti kutoka Urusi, alikuwa ameshatengewa nafasi jeshini. Hii ni kwa sababu babake alikuwa ameshawahonga viongozi wa kikosi cha wanajeshi. Hata hivyo barua yake kwa babake inaonyesha kwamba hakuwa tayari kushirikiana naye alipomjuza kuwa hangeichukua nafasi hiyo iliyopatikana kwa mlungura na ushawishi wa kisiasa. Kijana huyu alihiari kujitafutia kazi bila kutegemea udugu. Msimamo wake mkali ulizua mgogoro kati yake na babake kwa sababu aliuona kama uasi. (Walibora,2012, uk.88).

Tabia ya Mtemi kuwashinikiza watu kupata huduma kwa njia haramu ilianza mapema. Haya yanajitokeza katika kurasa za awali za riwaya hii. Ndiyo maana wahusika kama Matuko wanakiri kuwa walikuwa wamechoshwa na kiongozi wao.Tunaelezwa haya kumhusu Mtemi:

> "….huko kwenye Wizara ya Ardhi na Makao ndiko alikojifunzia mengi zaidi, mbali na kuambukizwa yale maradhi yasiyosikia dawa ambayo baadhi ya dalili zake ni kufichaficha faili za watu ili kujipatia milungura. Maradhi ambayo mhasiriwa wake haoni haya kumwibia hata asiyekuwa na chochote. (Walibora,2012, uk.8)

Ni bayana kuwa serikali ya Mtemi haikufanya uchunguzi wa visa vya kihalifu kwa makini. Utepetevu huu kazini unadhihirishwa na kufungiwa kwa vijana wawili; Amani na Imani.Hii ni kwa sababu Matuko Weye anakutana nao seli wakiwa wamefungiwa kwa tuhuma za mauaji ya kitoto Uhuru. Askari wa Mtemi wanawachapa na kuwadhulumu sana n ahata kuwatishi kuwa wao pia wangehukumiwa kifo na kutiwa kitanzi. Matuko Weye anatambua jambo hili na kulalamika akisema,

> “Kijana hariri sana weye usiyeweza kuudhi hata nzi weye kaifa mwanadamu”, aliuliza mzee Matuko Weye.“Nani kakuleta Weye hapa?Kwani umefanya nini weye?”“Wanasema mimeua”, alijibu Amani kwa minong’ono.”Weye umeua! Hapana! Hapana weye! Kuua si laiki yako weye.Ni urongo. Na hata kama umeua weye sasa nini?” (Walibora,2012, uk.84).

Anayoyasema Matuko Weye kuwa Amani hawezi kuua yanathibitishwa na Mwalimu Majisifu, Bi. Zuhura, Dj na Oscar Kambona.

Bi. Zuhura, mkewe Mtemi, anamwuliza,

> “…isitoshe, ukiwapeleka vijana hao kortini utakuwa na ithibati gani kwamba wameua? Mwanzo wewe ndiwe uliyemtwisha Amani mzigo wa kumlea mtoto asiyemhusu damu wala usaha? “wewe wajuaje hamhusu?” Mtemi aliuliza kwa tuhuma na mshangao kumsikia mkewe anazungumza na ghera namna ile. “Hata nisipojua angalau Mungu ajua babake mtoto yule marehemu ni nani” (Walibora,2012, uk.104-105)

Kadhalika, kakake Mtemi ambaye ni Mwalimu Majisifu anamtembelea kakake kumjulia hali na kumjuza mambo kadhaa. Moja wapo ya mambo hayo ilikuwa ni kuweka wazi kuhusu kesi iliyowakabili Amani na Imani. Anamweleza Mtemi,

> “ Sitaki ujali maslahi yangu. Jali maslahi ya watu wengine wote wa Sokomoko. Huu ndio ubinadamu. Kama ungekuwa unajali maslahi ya wengine, Yule mchungaji wako na mtumishi wangu hawangekuwa wanapigwa na baridi kule ndani kwa kosa ambalo hawakulitenda. Nimepata *first hand information* kutoka kwa daktari aliyepima maiti ya kitoto hicho naye amesema kimekufa kwa ugonjwa wa kichomi, ambao ni kawaida kwa watoto. Wale vijana umewafunga ndani kwa nini?” (Walibora,2012, uk.94)

Vilevile Mtemi mwenyewe anamsimulia bibiye kuhusu habari ambazo alielezwa na mhusika Dj. Maneno ya mhusika huyu pia yanasisitiza kuwa

madai ya Matuko kuwa wale vijana walitiwa seli kwa tuhuma zisizokuwa za kweli.Mtemi anamweleza mkewe,

> "…Yule kijana anenaye kama mkora? Mtundu wa mwisho… juzi tulikutana mjini akaniuliza eti kwa nini siwezi kuwaachilia wale vijana-kumbe wanaitwaje vile" Amani na Imani… basi kanikuta juzi na kuniuliza kwa nini nisiwaachilie ilhali hawana hatia. Nikamuuliza kama hawana hatia yeye ajuaje. Akanijibu kwa takaburi kwamba na mimi najuaje kama wanayo hatia. Mtoto kama huyo ni hatari kwa usalama". (Walibora,2012, uk.104)

Kutokana na maneno ya Dj ni bayana kuwa alifahamu fika kuwa Amani na Imani hawakuwa na hatia kwa sababu ndiye aliyetumwa na Imani kwenda kumfikishia Amani ujumbe kuhusu kuugua kwa Uhuru. Dj alipotumwa na Imani akamjuze Amani kuwa mwanao Uhuru alikuwa Mgonjwa,alipompata alimweleza Amani:

> "Basi nimekutafuta sana.Nimetoka kwako sasa hivi. Aisee jo! Mambo si fit. Yule mwanao Uhuru ni mgonjwa. Imani amenituma nikuite wende haraka. Maze fanya faster, jo" (Walibora,2012, uk uk.73)

Mwandishi anatueleza kuwa baada ya kupata ujumbe huu Amani alishika njia kuelekea kwake kuitikia wito . Mvua ilipopusa waliandamana na Imani hadi zahanati ya Mtemi Nasaba Bora walikokumbana na mapuuza, uzembe na dhihaki ya wauguzi. Wauguzi waliokuwa wakifuma fulana waliwabeza kwa kudai walimpata mtoto huyo wakiwa wachanga, yaani kupata mtoto mapema na kudai hawangewahudumia Sikukuu. Wakiwa njiani wakirudi, kitoto kikakata roho (Walibora,2012, uk.76-77).

Kiongozi huyu alimnyanyasa Amani kwa kumsukumia kitoto kichanga ambacho hakikumhusu ndewe wala sikio. Isitoshe,aliwaweka ndani Amani na Imani bila hatia yoyote kwa kuwasingizia kuwa walihusika katika kifo cha kitoto Uhuru.

Mtemi ana uhusiano wa kimapenzi na Lowela binti Maozi na kumtelekeza mkewe Zuhura. Jambo hili pia linasababisha wehu wa bintiye Mashaka. Tabaka tawala lilikuwa linashindwa kutimiza majukumu kwa wananchi wao kutokana na wizi wa fedha za umma zilizokuwa zinatolewa na wafadhili. Kwa mfano, zahznati ya Nasaba Bora ilikuwa mbovu na yenye kutoa huduma duni kwa sababu ya wizi huo (Walibora,2012, uk.144)

Mtemi pia anawahutubia wananchi waliohudhuria sherehe za wazalendo kwa lugha ya Kingereza japo wengi wao hawafahamu lugha hii. Sherehe hii ilihudhuriwa na wazee kwa vijana wengi wao hawakuielewa lugha ya Kingereza. Hata hivyo Mtemi anajikakamua kuwahutubia kwa lugha hii wasiyofahamu.

> *"Ladies and gentlemen, fellow countrymen, …A word is enough for the wise one. We are gathered here today to remember the glorious sons of this country who died that others might live…*" "Jua litatua kama bado tunasikiliza hizi *fwot fwot* hizi!" Amani alimsikia yule Bi. Kizee akimnong'onezea mwanamume wa makamo aliyekuwa karibu naye sikioni. "Mkubwa leo asema nini?" "Sijui", alijibu yule mwanamume. "Huoni tulivyonyamaza ji, hatujui wapi pa kushangilia wapi pa kunyamazia""Mbona asisome tafsiri ya Kiswahili ya hotuba hiyo maana twajua ipo?" (Walibora,2012, k.69-70)

Matuko Weye anapomwambia askari kuwa mama aliyemzaa aliwakosea wanadamu anaeleza jinsi askari wanawadhulumu raia badala ya

kuwalinda.Wanazifuata amri za kiimla za mtemi kipofupofu. Mathalani, Imani anamweleza Amani jinsi askari walitumwa kwao kwenda kuwalazimisha kuondoka shambani mwao, jinsi walivyompiga mama yao kitutu kama nyoka na vile kaka yao Oscar alipojaribu kumwauni alilengwa teke moja la kichwa lililompa kisulisuli ghafla, akaona vimulimuli na kuanguka (Walibora,2012, uk.57). Naye Imani aligongwa teke lililomwangusha chini.

## 2.2.6.0 UHAKIKI WA MCHANGO WA MHUSIKA BILAL KATIKA RIWAYA YA *MKAMANDUME.*

Katika sehemu hii tumeangazia nafasi ya mhusika Bilal ambaye amesawiriwa kama mwendawazimu na mwandishi katika riwaya ya *Mkamandume.* Imejadili na kuthibitisha kuwa mhusika huyu ni mwendawazimu kutokana na vitendo vyake na wanayoyasema wahusika wengine. Kadhalika,tumechunguza namna mhusika huyu mwendawazimu amechangia kufanikisha maudhui ya vita dhidi ya udhalimu, elimu na uongozi mbaya.

### 2.2.6.1 KUSAWIRIWA KWA BILAL KAMA MWENDAWAZIMU

Mhusika Bilal amesawiriwa na mwandishi kama mwendawazimu. Vilevile, maneno, matendo na mawazo yake yanadhihirisha kuwa ni mwendawazimu. Katika riwaya ya *Mkamandume* hali hii imedhihirishwa kupitia kwa maneno ya mwandishi mwenyewe na wakati mwingine kupitia kwa maneno ya mhusika Bilal. Mwandishi anaeleza :

> "…kinyago cha mtu kilikuwa kimekaa juu ya kiti mbele yake. Upongoo wa mtu, mweusi wa rangi ya maumbile na wa guo la uchafu alilovaa kwa kutojitia maji kwa miezi kama si miaka. Mwili wake ni mwili wa chungu kisichotoka mekoni. Alikuwa kajitupia shuka kwa mtindo wa lubega, shuka ambayo upya

> wake ilikuwa nyeupe lakini sasa imechukua rangi isiyo na jina. Na kisha imeshirai mafuta, majasho, mavumbi na mapuuza. Mbele imeraruka kukashifu kifua kilichoota dasi na jasho la kila siku lililogandia. Nywele zimesokotanasokotana na kukaliana na kuganda na kugandamana na kupoteza weusi wake wa asili kwa kukaliwa na vumbi lisilosita kuzitua. Yote hayo yalikuwa ni matokeo ya uchakaramu wake kama watoto mitaani walivyokuwa wakimwita. (Mohamed,2013,uk.241)

Kwa hakika taswira anayochora mwandishi ni ya mtu ambaye amewehuka. Kutothamini usafi wa mwili wa mtu binafsi na mavazi yake ni ishara kuwa kuna jambo linaloenda ndivyo sivyo katika maisha yake . Tunaelezwa kuwa hata watoto wa mitaani walifahamu uchakaramu wa Bilal.

> "… kiumbe huyo alimtazama Soud kijichoupembe. Katu hakuwa kiumbe wa kutazama jicho kwa jicho au uso kwa uso. Siku hizi macho yake yalikuwa yameupiga wekundu utadhani pilipili kichaa. Usingizi labda, pondeponde za pombe zisizomtoka kichwani mwilini mwake daima, sumu ya unga au masalio ya haba au yote labda! Alipokaa lile lubega lake lilipanda juu na Soud akasadifu kumwona bamkubwa akining'inia na nanga zake katikati ya kichaka. Mwili wake wote ulikuwa umemwota ukurutu, upele na vidonda. Miundu miembamba kama spoki na miguu imegawana viatu vibovu, wa kulia umevalia maklipa yaliyochanikachanika na kushoto malapa yaliyokatika kanda. Bahasha yake ya matambara na jumla ya vitu anavyoviokota majaani na kwenye mapipa ya taka alikuwa kaiweka chini sasa. Ananuka utadhani fungo!" (Mohamed,2013,uk.242).

Maelezo haya ya mwandishi yanathibitisha kuwa Bilal hana akili timamu. Anatuchorea taswira ya mtu mchafu, aliyevalia nguo chafu, anayevunda na hata viatu vibovu alivyovaa havifanani. Mguu mmoja ni maklipa na mwingine malapa. Kama mazoea ya wendawazimu, tunaelezwa kuwa alivyobeba aliviokota katika majaa na mapipa. Ni nadra sana kumwona mtu mwenye akili timamu akiishi bila kujali kuonekana uchi wake na wenzake.

Kwa Bilal jambo hili linatendeka na kutokana na hali yake ya uchakaramu halimshughulishi.

Bilal anamwambia Soud,

> "Usiseme mimi si mwendawazimu. Hata wendawazimu wenzangu wanajua kwamba mimi ni kichaa si mwendawazimu tu… (Mohamed,2013,uk.244)

Katika kauli hii Bilal mwenyewe anakili kuwa ni mwendawazimu. Bila shaka kauli yake inaambatana na alivyosawiriwa na mwandishi.

> Kufumba na kufumbua,alikuwa kasimama uchi kama alivyozaliwa. Na kabla mwemeo huo haujapita vyema machoni mwa waliokuwepo, alimshika bamkubwa wake kwa mkono wa kulia na mkono wa kushoto alikamata ile picha na kuanza kuikojolea, huku akisema,"Nitakukojolea kila siku mpaka nitakapokufa. Jicho kwa jicho! Kisasi changu! Huyu ndiye aliyesababisha yote haya! Huyu ndiye adui wa kila mtu!" (Mohamed,2013,uk.251)

Binadamu huona haya kuonekana uchi wake. Hata akiwa nyumbani peke yake, na awe amefunga mlango wa nyumba yake, hutokea kwamba akitaka kuingia msalani kuoga, bado atajifungia katika chumba chake ili avue nguo. Akiingia msalani utampata tena amejifungia humo.Bila shaka vitendo vya kuvua nguo hadharani, mchana wa Mungu, bila kujali waliopo ni ishara ya wendawazimu. Wendawazimu huu unamwelekeza Bilal kufikiri kuwa kuikojolea picha ya aliyemhini ni kisasi tosha. Ukweli ni kwamba, aliyemhini hana habari kuwa picha yake inakojolewa. Hili linaishia kuwa dua la kuku lisilompata mwewe.

### 2.2.6.2 MCHANGO WA BILAL KATIKA KUKUZA MAUDHUI

Msanii kama zao la jamii anapoandika kazi yake huwa na azma ya kueleza yale yanayotukia katika jamii. Ili kufaulu kufanya vile, yeye anaweza kueleza matukio hayo moja kwa moja au kutumia wahusika kuwasilisha ujumbe anaokusudia kuipasha jamii. Anapofanya hivi, wahusika hawa huwa ni kipaza sauti chake. Mohamed alidhamiria kumtumia mhusika Bilal kama kipaza sauti cha kueleza yanayomkera katika jamii. Amemsawiri Bilal akiwa mwendawazimu. Katika hali hii anatekeleza jukumu la kukuza maudhui ya uongozi mbaya, elimu na udhalimu.

#### 2.2.6.2.1 UONGOZI MBAYA

Wazimu wa Bilal ni athari za uongozi mbaya. Anamweleza Soud kwamba alipojiunga na taaluma ya ualimu, waalimu waliheshimiwa, lakini baadaye wanajeshi na askari walitukuzwa. Jambo hili lilwafanywa walimu kudharauliwa na kusababisha kutoheshimiwa na kutokubaliwa na wasichana wa jamii yao. Wasichana wakawapendelea wanajeshi bila kujali wasifu wa mhusika. Anafafanua,

> "Kwa kweli ilifika hadi kwamba ukienda kuposa pahala kwanza utaulizwa kazi yako. Ukiwa wewe mwanajeshi hata hukuchunguzwa kama wewe una akili timamu au la, mwizi, lusu au mnyang'anyi, ulipewa mtoto wa watu tu. Ndiposa kila msichana alitamani kuolewa na askari au mwanajeshi. Ni wakati huu ambapo haramu ilihalalishwa na halali kuharamishwa. (Mohamed,2013, uk.250)
>
> Walimu waliooa iliwabidi kuwalinda wake zao wasichukuliwe na askari. Mkewe Bilal, Bishara alichukuliwa na Brigadia. Bilal aliumia sana moyoni anasema," "Kwa bahati mbaya nilikuwa mwalimu masikini. Si mwanajeshi!... maluuni yule!". Alisita kidogo halafu ghafla akahitimisha kauli yake. "Lakini

> simlaumu Brigadia, nawalaumu waliohalalisha hali hii". (Mohamed,2013,uk. 251)

Mhusika Soud alikubaliana na mawazo ya Bilal. Alikiri kimoyomoyo kuwa hata wafanyakazi na wakulima waliolipia nafuu za watu hawa wanadharauliwa. Hata yeye hakuridhika na hali na sera za kutukuza wanajeshi na polisi. Katika dondoo hili Bilal anamweleza taratibu kuhusu taaluma yake ya Ualimu. Taaluma hii iliheshimiwa na wakubwa kwa wadogo. Kauli hii ina ukweli ndani yake na Soud anakubaliana naye. Anaendelea kumweleza mabadiliko yaliyotokea. Ualimu ulidharauliwa na yeye kama mwalimu hakusazwa. Jambo hili lilimwathiri binafsi kwani ni wakati wa mabadiliko haya ambapo mkewe Bishara anachukuliwa bila hiari yake.

> " Mke wangu alichukuliwa na mkuu wa jeshi. Brigadia nakusudia."… "Kwa bahati mbaya nilikuwa mwalimu masikini. Si mwanajeshi!... maluuni yule!". Alisita kidogo halafu ghafla akahitimisha kauli yake. "Lakini simlaumu Brigadia, nawalaumu waliohalalisha hali hii". (Mohamed,2013,uk. 250)

Kadhalika, anamweleza Soud dhuluma aliyopitia mwalimu wake Seyyid Kakhtan.

> Anasema namkumbuka mwalimu wetu mmoja…Nani vile? Alijivuta kufikiri, "Nani vile?"…Aaa! Seyyid Kakhtan…marehemu maskini, Mungu amlaze pahala pema huko aliko…walimdhulumu vibaya vibaya. Walimwachisha kazi na kumwacha atambe na njia ugenini-alikuwa akitwambia, kufanikiwa masomoni si kufanikiwa na maisha." (Mohamed,2013,uk.244 )

Dukuduku hili linaeleza kuwa ni wengi walioathiriwa na uongozi wa kikatili. Mwalimu wake Bilal aliachishwa kazi na kuachwa akiteseka. Kutokana na

maelezo ya Bilal ni kweli kuwa hakuwahi rejeshwa kazini kwani hatimaye anaeleza kuhusu mauko yake.

Aidha, kutokana na maneno hayo hili ni kweli kuwa Bilal ana kumbukumbu nzuri. Anamkumbuka mwalimu wao, anaudhika na alivyodhulumiwa.Hili ni dhihirisho kuwa anaelewa kuwa kuachishwa kazi bila sababu ni uonevu. Kama binadamu anayefahamu dini, anamwombea Mungu aendelee kumlaza mahali pema peponi.

Mifano hii ineleza jinsi uongozi mbaya unavyowaletea watawaliwa hasara. Viongozi wakitawala visivyofaa wananchi wanaumia. Bilal anasema kuwa analaumu waliohalalisha hali hiyo. Mwishowe, Bilal anamshukuru Soud kwa kumnunulia bia. Anatambua kuwa Soud amemfanyia hisani ambayo ilikuwa nadra kwake kufanyiwa. Kadhalika anaomba msamaha kwa mahoka yake. Hili linaonyesha kuwa anatambua kuwa sio yote aliyofanya yaliyomfurahisha mhisani wake Soud.

**2.2.6.2.2 ELIMU**

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni,vyuoni na maishani (TATAKI,2013). Wazazi wa Soud wamemwelimisha hadi ng’ambo hadi akawa wakili. Elimu ilimwezesha kusafiri na kutangamana na watu ambao baadaye waliishia kuwa marafiki zake kama Nadia. Taaluma yake inamwezesha kuwatetea wananchi pindi wanapokabiliwa na kesi. Kwa hivyo, elimu inawawezesha wanannchi kupata haki. Aidha,elimu iliwasaidia watu kupata ajira. Bilal anaeleza kwamba alisoma na kuhitimu kuwa mwalimu,sawa na mwalimu wake Seyyid Khakhtan . Wahusika wengine

kutokana na mafunzo waliyopata walihitimu kuwa wanajeshi kama Brigadia aliyemtwaa na kumwoa mkewe Bilal;Bishara.

Anamwagia Soud dukuduku lake:

> *Mimi nilikuwa na akili nyingi kama wewe pia au zaidi…*
>
> *"Najua"*
>
> *Lakini ncha za akili na wendawazimu hazitengani kwa masafa makubwa mno… au unasemaje?*
>
> *"Kweli"*
>
> *"Unakubali?"*
>
> *"Ndiyo nakubali kabisa"*
>
> *"Kwa nini basi wewe ulipasi mtihani wa kuingia sekondari?'*
>
> *"Mitihani si kigezo cha akili nyingi, ni ufundi wa kuhifadhi na kukariri mambo tu au kujua namna ya kujibu masuala unayoulizwa…"*
>
> *"La, la,la! Usiniambie mambo hayo bwana".*
>
> *"Nakwambia kweli"*
>
> *"Hapana, tokea utotoni, akili zangu miye zimekuwa zikiruka hewani. Zako zimo kichwani mwako timamu kabisa"* (Mohamed,2013,uk.243).

Katika mazungumzo haya kati ya Bilal na Soud, ni kweli kuwa Bilal anaelewa kuwa ncha za akili na wendawazimu hazitengani kwa kiwango kirefu mno. Aidha, anafahamu kuwa kuna tofauti kati ya wenye akili timamu na wendawazimu. Anamthibitishia Soud kuwa uwezo wake wa kupita mtihani na kujiunga na shule ya Sekondari ni ishara kuwa alikuwa na akili nyingi. Kutokana na dayalojia hii ni kweli kwamba Bilal ana

uwezo wa kuwatambua watu na kukumbuka mambo yaliyojiri katika maisha yao.

Kutokana na hali ya kufahamu kuwa Mhudumu wa baa,Kinibu alimdharau, Bilal alimshambulia kwa hamaki kwa maneno yafuatayo:

> “Watu wengine bwana …nini wewe? Kama hatukununua sisi bia huli wewe! Tazama vile! Muuzapombe ana heri gani? (Mohamed,2013,uk.244)

Kadhalika, alitambua kuwa Kinibu alimdharau ndiyo maana anamweleza kuwa katika maisha watu hutegemeana, hakuna aliyejitosheleza kwa hali na mali. Anamweleza kuwa wasiponunua bia hatapata ujira, hivyo asiwadharau wateja. Ukweli ulioje!

> ‘‘…Bilal alimwambia Kinibu achukue mwenyewe gilasi yake akawape wastaarabu wake wanaokunywa bia kwa gilasi. Yeye atapiga tarumbeta.’’ (Mohamed,2013,uk.245)

Kauli hii inaonyesha kuwa Bilal alifahamu kuwa yalikuwepo matabaka katika jamii; waliostaarabika na wasiostaarabika, matajiri na walalahoi. Alijua kuwa kulingana na Kinibu alikuwa mmoja wa wasiostaarabika. Hivyo anaona hakuna haja ya kung’ang’ana kuinywa bia kwa gilasi, ainywe kwa chupa kama alivyozoea.

Mwandishi pia anaeleza kuwa Bilal kila siku katika wendawazimu wake, alijichukia kwamba kabakiwa na sehemu ndogo ya ubinadamu. Alitaka awe mnyama kamili. Alitaka awe mwendawazimu wa kwenda uchi.

> Kuna ubaya gani kuwa mnyama? Kuna hasara gani kupoteza akili yote? Kuna aibu gani kwenda uchi? Sote si tulizaliwa wanyama na kila siku tunadhihirisha unyama wetu. Kwa ushahidi kamili sisi sote ni wendawazimu watupu. Sote sisi

> tulizaliwa uchi na tunakwenda uchi bila kujiona- nguo au bila ya nguo! Tatizo liko wapi basi? Alijiambia kichwani mwake huku nishai ya bia inapanda polepole.
>
> "Niambie…"alimwelekea Soud sasa baada ya kupiga mafunda matatu ya haja na kuvuta wakati katika kimya kilichowazunguka wote wawili.
>
> "Niambie, hivi wewe ni mnyama?"
>
> "Hapana, mimi sidhihaki- yaani nakuuliza kweli kama wewe mnyama au…"
>
> "Asili yangu labda" "Ah yes! Aliruka Bilal. "Ndiyo sisi sote wanyama kwa asili. Lakini chembe ya asili haitoki ukiwa nayo mwilini…" kama virusi… kama virusiiiiiiiiii!" (Mohamed,2013,uk.246).

Mtaaalamu Darwin (1871) aliibua nadharia ya Uumbuji iliyokubaliwa na wengi na wakati huohuo kupingwa vikali na kwa ghadhabu na binadamu hasa viongozi wa kidini. Alieleza kuwa binadamu asili yake ni mnyama, yeye na tumbili ni ndugu. Akaendelea kueleza kuwa mabadiliko ya kimazingira ndiyo yaliyomfanya kubadilika. Hivyo yaonekana Bilal anaifahamu nadharia hii na anakubaliana na mawazo yake Darwin. Kadhalika, maovu aliyofanyiwa na walio mamlakani ya kunyang'anywa bibi kwake ni ithibati tosha kuwa wanadamu wana chembechembe za unyama ndani yao.

> "Usinisimbulie…bia ni mkojo wa Firauni tu, ambao ukiingia mwilini mwako unageuka mkojo wako mwenyewe wakati huohuo na kukuendesha chooni kila mara, na ndani unaacha sumu inayobakia kichwani mwako milele" (Mohamed,2013,uk.246)

Mbali na kuwa bia inafananishwa na mkojo wa Firauni, yaani kitu kisicho na thamani yoyote, tafiti nyingi zilizofanywa na wataalamu wa masuala ya afya zimethibitisha kuwa pombe na vileo kwa jumla vina madhara mengi kwa afya ya binadamu. Escandon na Galvez (2016) wanakubaliana na Voltaire

aliyesema kuwa pombe ni maji yanayoleta kifo. Wanafafanua madhara mengi ya pombe kama yafuatayo:husababisha maradhi ya figo na maini,huathiri utendakazi wa akili za binadamu hivi kwamba anashindwa kufanya maamuzi yanayofaa, huleta udhaifu wa ufahamu na kumbukumbu, huathiri umilisi wa lugha na mhusika hushindwa kutatua matatizo. Wanawake wajawazito wanapata hatari ya kuupoteza ujauzito kabla ya wakati wa kujifungua au wakifanikiwa kukamilisha kipindi cha ujauzito kuna uwezekano wajifungue watoto wenye aina mbalimbali za ulemavu.

Kadhalika, ulevi huathiri utendakazi wa viungo vya mwili na kuleta ulegevu,mlevi hukosa hamu ya kula, kuna hali ya utepetevu kazini miongoni mwa wahusika na uzembe. Uchumi pia hudorora. Migogoro nyumbani, uharibifu na mienendo potovu pia huletwa na pombe. Ajali nyingi barabarani na kazini husababishwa na ulevi,fikra za kujitia kitanzi huwajia walio nauraibu uliozidi kiasi cha kuwa wategemezi wa pombe na mwisho, vifo vingi vimetokana na ulevi wa madereva.(t.y)

> Nambie pia kama wewe pia ni mwendawazimu?
>
> “Labda!” safari hii Soud alikimbia kuambiwa anasimbulia watu.
>
> “Sitaki labda niambie kwa hakika”.
>
> “Kila mtu ana wazimu wake” .
>
> “Ewaaaa…”
>
> “Na je, hapo ulipo upo uchi?’’
>
> Hilo lilimwemeza na kumfurahisha wakati mmoja Soud.Alipasua kicheko na kuashiria mazungumzo ya mwendawazimu huyu yakimvutia ingawa yalikuwa yakienda mbali pia.

"Wewe waonaje? (Mohamed,2013,uk.247).

Mawazo ya Bilal yanaungwa mkono na mtaalamu Rieger anaposema kuwa hakuna jambo linalotenganisha wendawazimu na urazini barabara. Anaendelea kufafanua kuwa wengi wetu hudhibiti hisia za wendawazimu kwa sababu ya miiko ya jamii. Mawazo ya Bilal yanaambatana na ya Rieger. Anamwambia Soud amweleze kama yeye pia ni mwendawazimu na kukubaliana na mawazo kuwa kila mtu ana wazimu wake. Rieger anafafanua kuwa katika fasihi kuna uwezekano wa kueleza hisia hizi bila wasiwasi. Japo wengi wetu sio wendawazimu tuna migogoro ya kinafsia. Waandishi wanaweza kuandika kazi zinazosawiri hali halisi ya kisaikolojia ya watu kupitia kwa wahusika Rieger (1994). Mawazo haya yanaambatana na mhimili wa nadharia ya uchanganuzi nafsia unaoeleza kuwa mwandishi huitumia kazi ya fahisi kuyalipulia majipu yake.

> "Kwani wewe mwenyewe hujioni hata wataka mimi nikuone?"
>
> "Aaaa, mimi najiona nimevaa shati, suruali, ndengarizi…" "Aaaa,hizo ni alama za kudanganyia tu…ungekuwa na jicho la x-rays kama mimi, ungeona watu wote wanatembea uchi kila siku, kila wakati…"
>
> Soud alicheka tena. "Kwa bahati mbaya sina jicho hilo", alijibu kwa uchangamfu.
>
> "Ukimwona mtu amevaa nguo, sivyo alivyo katika dhahiri ya mambo. Nguo humsitiri kijuuujuu tu. Ukimtazama sana utamwona uchi. Uchi kabisa!"

Ukweli ulioje! Aliwaza soud huku akiyahusisha mawazo ya Bilal na dukuduku lake analolala nalo na kuamka nalo. Mwanadamu ni mnyama anayekwenda uchi bila ya kujua. Nguo humsitiri kijuujuu tu. Kwa dhati ya mambo ya uchi kabisa… muhtasari gani wa ukweli huu? Ndani ya kichwa Soud mliwaa na

kumemetuka kianga cha ukubalifu wa mwendawazimu kikajipenyeza. Ilikuwa kama ule ulimi mdogo wa kibatari ulimwagiwa petrol na kuripuka. Atayameza maneno hayo… (Mohamed,2013,uk.247).

Soud anakubaliana na Bilal kuwa nguo humsitiri mtu kijuujuu tu. Mtu afanyapo matendo ya aibu au yakiukayo maadili ya jamii, hupatwa na aibu kubwa. Matendo hayo humwanika na kujulikana hulka na mienendo yake. Hali hii ni sawa na kumvua nguo na kumwacha uchi. Ndiyo maana Bilal anasema kuwa nguo humsitiri mtu kijuujuu. Nguo hazisitiri matendo yanayodhihirisha kama mtu ana utu. Kwa vile mtu ni utu, matendo yasiyodhihirisha utu humwacha mtu uchi.

> “Sina hadithi kwa hakika”, aliendelea Bilal. “Labda kadhia”Soud alijaribu kuvipekua vivuli vinavyofunika maana za maneno mawili hayo: hadithi na kadhia. Labda hadithi inaambatana zaidi na ubunifu na kadhia iko karibu na ukweli. Viwe viwavyo, Soud alitunga makini kumsikiliza. (Mohamed,2013,uk.248)

Kulingana na *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011), hadithi ni masimulizi ya kubuni, kisa cha kutunga ambacho hakikutokea kweli, habari za kubuni. Kadhia ni jambo linalofanyika, tukio au mgogoro. Bilal anapomweleza Soud kuwa hana hadithi na kwamba anayosimulia ni kadhia, maneno yake yanaonyesha kuwa anafahamu tofauti kati ya mambo haya mawili.

> “Ualimu ni kazi ya Mungu. Niliuingia kwa hamu si kwa sababu hakukuwa na kazi nyingine ya kufanya kwa mwendawazimu mwenye kichwa kibovu kama changu, baada ya kushindwa na mtihani wa kuingia Sekondari…ha, ha, ha…”Alicheka kwa ule ule wazimu wake halafu akaendelea.

> "Nyinyi ndio wakocho, wenye bongo za smaku, mlipata fursa ya kuendelea mbele mpaka mkawa Wanasheria", alisita hapo.
>
> "Tazama hata manabii na mitume wote walikuwa walimu. Walitumwa na Mwenyezi Mungu kuja kuifunza dunia" (Mohamed,2013,uk.248)

Madai ya Bilal kuwa Manabii na Mitume ni walikuwa waalimu ni ya kweli. Tunapata mifano mingi ya mafundisho katika Biblia katika Agano la kale na Jipya. Kwa mfano:

Isaya 40:30-31.

> *Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume na vijana wataanguka; bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya;watapanda juu kwa mbawa kamatai;watapiga mbio, wala hawatachoka;*
>
> *Watakwenda kwa miguu,wala hawatazimia".*

Isaya 57:21 *Hapana amani kwa wabaya;asema Mungu wangu.*

Mathayo 5:1-6

> 1.*Naye alipowaona, alipanda mlimani;na alipokwisha kuketi,wanafunzi wake walimjia;*
>
> 2 *akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema,*
>
> 3 *Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*
>
> 4 *Heri wenye huzuni;maana hao watafarijika.*
>
> 5 *Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi.*
>
> 6 *Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.*

Kutokana na nukuu hizi, ni kweli kuwa Manabii waliwafundisha watu na mafunzo yao yalikuwa ya kushauri, kuwapa watu matumaini, kuwaonya na

kuwapa ari ya kuishi maisha yenye maadili mema. Haya yote Bilal aliyaelewa.

Bintiye Mkamandume, Viwe walishirikiana na Soud na vijana wenzao kuandaa maonyesho ya tamthilia. Vijana hawa waliweza kuandika tamthilia nyingi na kuziigiza jukwaani. Tamthilia hizi zililenga jamii na historia yake. Zilijadili matendo ya jamii, migongano yake,mikinzano yake, historia, siasa ,ujumi na usanii wake uliteka hadhira kiakili na kihisia, (Mohamed,2013,uk.472). Zilielimisha na kuonyesha ukweli ulio katika jamii. Maonyesho haya yalifikisha harakati za vijana kileleni. Ziliwavutia vijana wengi. Hatimaye,Soud na Viwe wakarudi kwao Malelejimema kuwazindua vijana wenzao, Mkamandume naye alirudi akiwa na nia ya kuleta mageuzi katika jamii. Katika hali hii elimu inachangia katika juhudi za kuikomboa jamii kutokana ma dhuluma.

Ni bayana kuwa japo Mkamandume hajasoma elimu ya vitabu, dunia imemfunza mengi. Vilevile mambo mengi ambayo Bilal anamweleza Soud yanatokana na tajriba yake katika maisha.

Bilal anapoeleza kadhia yake anasema kuwa yeye alipata elimu iliyomwezesha kuwa mwalimu. Awali, anamweleza Soud kuhusu Mwalimu wake Seyyid, mwalimu aliyewaeleza mengi. Si ya vitabuni tu bali hata elimu dunia. Analinganisha akili zake na za Soud na kusema kuwa Soud alikuwa na akili za Sumaku zilizomwezesha kuendelea na masomo ya sekondari na hata kuwa Mwanasheria.

Bilal anamweleza Soud jinsi waliojiunga na mafundisho ya Uanajeshi walivyoheshimika. Anamweleza kuwa wazazi walionea fahari jambo la kuwaoza mabinti zao kwa wanajeshi. Wakati huu walimu nao walidharauliwa kweli kweli na ndio maana anawalaumu waliohalalisha hali hii.

Baada ya Viwe bintiye Mkamandume kujifungua kitoto cha kiume, alimwajiri jiraniye Anna Msija kukilea kitoto kile naye akajiunga na shule ya watu wazima. Alisoma asubuhi hadi mchana na kufanya kazi ya biashara usiku. Mwandishi anaeleza kuwa:

> "Alipoondoka kwao alikuwa kafika kidato cha tatu.Hapa alijiendeleza na kufanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne, akafaulu vizuri… baada ya kufaulu mitihani ya darasa la kumi na mbili, aliendelea na masomo, akafanya mitihani ya kidato cha sita na kufaulu vizuri. Hakupoteza muda akajiunga na chuo kikuu huria na huko akapata digrii ya mwanzo. Alipokuwa akisoma na kufanya mitihani alipanua biashara yake ya vyakula na alipopata digrii tu, aliamua kuanzisha mkahawa wa kisasa wa vyakula vya ki- Swahili aliouita Ufufuzi." (Mohamed,2013,uk.468-469)

Manufaa ya elimu ya ni mengi. Viwe, aliyekuwa amefukuzwa kwao kwa kuwa mjamzito anaitumia elimu kama silaha ya kumwezesha kupigana na changamoto za maisha ya jiji. Anatia fora na kupata digrii. Hatimaye, maarifa haya yanamwezesha kupanua biashara yake na hata kuanzisha mkahawa. Elimu yake inamwezesha kuvuka daraja kutoka tabaka la wachochole na kuwa mwenye chake. Alitaka elimu yake imwezeshe kuandika kazi za sanaa au maonyesho ya tamthilia, jambo alilofaulu kufanya kwa ushirikiano na Soud.

### 2.2.6.2.3 DHULUMA

Kuna matukio mengi katika riwaya yanayothibitisha ukatili wa wahusika dhidi ya wengine.Mwalimu wake Bilal aliachishwa kazi bila sababu, jambo lililomfanya kutaabika sana. Mkewe Bilal pia alichukuliwa na Brigadia na Bilal hajui amlilie nani. Jambo hili linasababisha wendawazimu wake.

> "… alichukuliwa na Brigadia nakusudia" "Nilimpenda Bishara kupita kiasi. Sikusudii mapenzi ya vitabuni. Mapenzi yangu yalikuwa nadhifu yasiyo na doa. Maisha yangu yote alikuwa kayadhibiti mikononi mwake". (Mohamed,2013,uk250)

Ni dhahiri kuwa Bilal anakiri kwamba sababu yake ya kufunga ndoa na mkewe ilikuwa mapenzi ya dhati. Yeye pia anatofautisha mapenzi ya kweli na ya vitabuni. Sababu kuu ya kuwehuka kwake ni kunyang'anywa bibi aliyemwoa kutokana na mapenzi ya dhati kwake na kutwaliwa na Brigadia. Kama tujuavyo, Brigadia ni mwanajeshi mwenye cheo kikuu. Kulingana na anavyoeleza ni wazi kuwa kutokana na mfumo wa uongozi uliokuwapo uliohalalisha haramu kuwa halali, haki ilikuwa ndoto kupatikana kwa wananchi maskini. Hali hii ilisababisha uchakaramu wake.

Mkamandume anaidhulumu familia yake. Anamuuza ng'ombe wao wa pekee aliyekuwa tegemeo la familia kwa Soud bila kumjuza wala kumshirikisha mkewe kwa bei ya shilingi laki moja na kuondoka nyumbani na kumwacha mkewe akiteseka. Huu pia ni ubinafsi kwani haijali aila yake. (Mohamed,2013,uk388-389).

Hata hivyo,mjadala anaozua kati yake na Soud unadhihirisha kuwa bado anafahamu mengi. Vilevile, maneno ya mwandishi, matendo ya Bilal

mwenyewe na baadhi ya mawazo yake na ya Soud kumhusu yanadhihirisha kuwa Bilal angali na urazini katika akili zake. Anapomkuta Soud katika Starehe Club anamsaili,

> Hunijui? Alianza huku akionyesha mshangao. "Aaaa, bila shaka hunijui. Ha ha ha…nani anayetaka kumjua shetani? Nani anayetaka kumjua mwendawazimu? Ha, ha, ha …wuuu…waw! (Mohamed,2013,uk.243)

Kauli hii ya Bilal inadhihirisha kwamba anafahamu unyanyapaa unaowakumba wanyonge hasa wendawazimu katika jamii. Anaelewa kuwa hakuna mtu anayetaka kushirikishwa au kuwa na uhusiano nao. Kila mtu hujitenga nao. Ndiyo maana anacheka kicheko cha kejeli na kumwuliza "...nani anayetaka kumjua shetani?"

Binti yake anaporingwa anamfukuza kutoka nyumbani kusudi asimletee aibu. Kupitia urejeshi Mkamandume anaikumbuka siku ile aliyopambana na wanawe na mkewe alipokuwa akimbinginya bintiye Viwe. Mwandishi anaeleza kwamba angelimuua kama si kuja kwa watu wengi kumpapatua na matokeo yake yalikuwa ni kumfukuza bintiye. Hatimaye, bintiye alikwenda jijini kujitafutia riziki, babake asijali yaliyompata huko. Aidha, hakujali kuwa mkewe Tufaa alijawa na simanzi baada ya kufukuzwa kwa bintiye. (Mohamed,2013,uk.320). Huu ni ukatili wa hali ya juu.Bintiye Time pia hakusazwa. Alikatazwa na babake kuolewa na Soud, kijana aliyempenda kwa dhati. Hii ni kwa sababu kijana huyu yaani Soud na Mkamandume walikuwa mahasimu kutokana na misimamo pinzani ya kisiasa kati ya babake Soud na Mkamandume. (Mohamed,2013,uk.318).

Waliopigania Madaraka hawakunufaika, ndiposa Mkamandume anatamauka. Kazi aliyoifanya ni ya chura. Kwa kweli ilikuwa kazi ya kudunisha kwani vifaa vya kusafisha vyoo na hata maji hayakupatikana yalikuwa adimu. Umaskini uliokithiri ulimtamausha Mkamandume. Wao waliopigania Uhuru ndio walikosa pesa hata za mahitaji ya kimsingi, jambo lililomkera sana. Wasiojua maana yakupigania uhuru ndio waliowatawala.Wafanyakazi walilipwa vipesa vichache na walipopewa likizo, hawakulipwa hata senti moja.uk.(Mohamed,2013,uk.328 ,332).

Wakati Mkamandume alimkuta Bi.Tukaije kisimani akikoga, picha ya mwanamke huyu inamkumbusha kwamba imepita miaka mingi ya matatizo iliyombaradhulisha.

> “Katika miaka yote hiyo Mkamandume amejikuta analala na Tufaa kitaanda kimoja huku yeye kampa mgongo mwenzake” (Mohamed,2013,uk.368).

Hii ni dhuluma ya kimapenzi kwa mkewe aliyelihitaji pendo lake lakini hakumjali. Mwandishi anaeleza yafuatayo:

> “Bi. Tukaije alikuwa mdogo sana kwake (Mkamandume), na mdogo kwa mumewe pia. Kwa nini wanaume huoa watoto wadogo kama hawa? Labda hali hii ya kulazimishwa kuolewa na watu wazima au wazee ndio iliyomfanya Tukaije awe mtundu kidogo ingawa mke wa mtu. Alipomwona Mkamandume (ingawa naye mzee). Tukaije alijiregeza maungo na sauti yake. (Mohamed,2013,uk.369)

Bibi huyu baada ya kujaribu kumtongoza Mkamandume alimshawishi amtwike hando kisimani lakini mwanaume mwenzake Bwana Rajab alipotokea, alikata shauri kuwa Mkamandume ndiye kamtongoza mkewe Sheha , (Mohamed,2013 uk.367-370). Hii ni ishara ya maonevu dhidi ya

jinsia ya kiume ambapo waja wengi wanawahukumu kuwa ndio tu wanaoweza kuwatongoza wanawake ingawa ukweli ni kuwa jamii ya sasa haina miiko. Yeyote anaweza kumtongoza mwenzake kwani katika hali hii Bi. Tukaije ndiye aliyemtongoza Mkamandume.

Kadhalika, tunaelezwa kuwa Bi.Tukaije hakuolewa na Sheha kwa hiari ,alilazimwishwa. Alikuwa msichana mchanga sana akilinganishwa na umri wa mumewe. Dhuluma ya mtoto wa kike inashuhudiwa hapa. Ndoa za lazima na mapema ni baadhi ya mambo yanayosababisha masaibu kwa wasichana wenyewe. Wanateseka sana kwa kunyimwa uhuru wa kufanya uamuzi kuhusu maisha yao na zaidi ya hayo, kutokubaliwa wakomae kiakili kabla ya kuingia katika asasi ya ndoa.

Katika maisha kuna hatua tatu muhimu ambazo aghalabu kila mtu sharti azipitie. Kuzaliwa, kuoa au kuolewa na kufa. Kwa bahati mbaya, ya kwanza na ya tatu mtu binafsi hutegemea kudura. Mtu hachagui azaliwe lini, wapi na wazazi wake pia hachagui. Vivyo hivyo, asipotamauka na kujitia kitanzi, hawezi jua siku yake ya mauko na kitakachoyasababisha. Ni fumbo kubwa kwake. Ndiyo maana si haki kumnyima mtu uhuru wa kuchagua aolewe lini, wapi, na na nani(mchumba).

### 2.2.7.0 HITIMISHO

Sura hii imeangazia mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui ya riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Dhana ya uhusika na wahusika, usawiri wa wahusika na wahusika wendawazimu katika riwaya teule zimeshughulikiwa. Tumebainisha kuwa kuna aina tatu kuu za

wahusika: wahusika wakuu , wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Katika riwaya, wawili hawa ni wahusika wajenzi ambao ni bapa. Wahusika bapa hutumiwa na mwandishi kuwasilisha dhana fulani kama wanavyofanya Matuko Weye na Bilal. Hii ni kwa sababu wametumiwa kukejeli tabia, mienendo au mambo fulani katika jamii kwa njia ya kuchekesha. Wahusika hawa wanafanyiwa stihizai ama mzaha na watu wa jamii zao. Vile vile, tumetoa mwangaza kuhusu dhana ya wazimu hasa wahusika wendawazimu na sababu za waandishi kuwasawiri wahusika wendawazimu katika kazi zao.

Kadhalika imeangazia wahusika Matuko Weye na Bilal waliosawiriwa kama wendawazimu na waandishi. Imejadili na kuthibitisha kuwa wahusika hawa ni mwendawazimu kutokana na vitendo vyao, maneno yao na maneno ya wahusika wengine. Vilevile, utafiti huu ulithibitisha kuwa Matuko Weye na Bilal ni wahusika wenye nafsi mbili kutokana na maneno na pia vitendo vyao. Imebainika wahusika hawa wameshirikishwa na waandishi katika kuendeleza maudhui katika riwaya teule. Matuko Weye anakuza amechangia kukuza vita dhidi ya udhalimu, ukombozi na uongozi mbaya na Bilal amefaulisha maudhui ya uongozi mbaya, elimu na dhuluma.

Sura inayofuata ambayo ni ya tatu inayoshughulikia uhakiki wa mchango wa wahusika wendawazimu katika kukuza mbinu za uandishi katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea na Mkamandume*.

# SURA YA TATU

# UHAKIKI WA MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUKUZA MBINU ZA UANDISHI

## 3.0 UTANGULIZI

Lengo la pili la utafiti huu lililenga kuchunguza jinsi wahusika wendawazimu wamefanikisha mbinu za uandishi katika riwaya za Kidagaa Kimemwozea na Mkamandume. Mbinu za uandishi ni ubunifu wa kisanifu ambao hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi (Wamitila,2008). Mbinu za uandishi ni nyingi lakini katika utafiti huu tumewasilisha na kuchambua zifuatazo: balagha, kinaya, kejeli, ucheshi, taswira,mbinu rejeshi na dayalojia.

## 3.1. MCHANGO WA MATUKO WEYE KATIKA MBINU ZA UANDISHI

Matuko Weye amechangia katika kuendeleza mbinu za uandishi .Baadhi ya mbinu hizi ni pamoja na:

### 3.1.1 BALAGHA

Ni mbinu inayohusisha maswali yasiyohitaji majibu yanayoulizwa kwa nia ya kusisitiza au kumfanya msomaji atafakari zaidi kuhusu yanayozungumziwa. Katika riwaya Matuko Weye alipokuwa akihutubu aliuliza maswali kadhaa. Mathalani,

> "Tumetoshwa.Weye mwananchi mlalahoi huoni hivyo weye?Weye mwananchi huoni tunavyodhalilishwa?Huoni weye?Kwa nini weye umefumba macho?" (Walibora,2012,uk.71)

Mifano hii inadhihirisha jinsi Matuko alivyokuwa na ari ya kupinga na kupigana na utawala dhalimu wa Mtemi Nasaba Bora.

> Alaa bwan'mdogo hata weye ushaletwa humu ikuluni? …na hata kama umeua weye sasa nini? Weye askari njoo umfungulie huyu kijana aende zake weye. Au mnishitaki miye kwamba nimeua Eeh? (Walibora,2012, uk.84)

Katika kauli hizi Matuko anamtetea Amani wakati walikuwa seli kwamba hawezi kuua, kauli ambazo zinadhihirishwa na wahusika Lowela, Mwalimu Majisifu Dj na Bi. Zuhura.

> Hata nyie ndio mmenichosha na wazimu wenu. Maana mtu na akili zake timamu atawezaje kuwatia mbaroni watoto wema kama hawa? Huoni weye hapa hali ya mahakama kuwa na hatia huku washtakiwa wakiwa hawana hatia? (Walibora,2012, uk.86)

Kauli hizi za Matuko ni za kweli kwani Askari hawakufanya uchunguzi wowote kuhusiana na kifo cha kitoto Uhuru. Waliyachukulia maaneno ye Mtemi kuwa ya kweli na kuwalaumu Imani na Amani. Matuko anauona huu kuwa wazimu kwani haikuwa haki kuwahukumu kuwa wauwaji bila ushahidi. Matuko pia anawauliza askari sababu za kumwachilia bila kumpa kiamsha kinywa na pia bila kumfikisha mahakamani.Kutokana na maswali hayo ni bayana kuwa Matuko Weye alifahamu haki za wafungwa barabara.

### 3.1.2 KINAYA

Ni hali ya mambo kutukia kinyume na matarajio. Kwa mfano, ni kinaya kuwa wananchi wenye akili razini waliogopa na kunyamaza wakidhulumiwa na Mtemi ilhali Matuko Weye ambaye ni mwendawazimu anajijasiri na kumshambulia mtemi hadharani.

Ni kinaya kuwa Matuko anampiku mfawidhi wa sherehe maarifa. Anakinyakua kipaza sauti bila yeyote, hata mfawidhi wa sherehe kugundua. Yaonekana alikuwa amepanga kulitekeleza jambo lile na kwa bahati nzuri akafanikiwa.

Watu wa Sokomoko wanafumba macho na kujitia hawaoni wakinyanyaswa na kudhalilishwa na Mtemi. Imani anamweleza Amani kuwa kilichomkera zaidi ni kimya cha watu wa Baraka wakati Shamba lao lilinyakuliwa na baadaye nyumba yao kuchomwa moto. Wao walinyamaza tu hawakuwatetea.

Askari wanamkamata na kumtia ndani Matuko sikukuu ya Wazalendo. Yeye pia kama wazalendo wengine alistahiki kuenziwa kama mojawapo wa mashujaa lakini badala yake anafungwa siku ya kuwaenzi mashujaa. " Alikwenda Burma kupigania Uingereza katika Vita vya Pili vya Dunia akiwa na akili zake timamu. Aliporudi alikuwa na mahoka au amewehuka kabisa". (Walibora,2012, uk.72). Badala ya Matuko kutafutiwa daktari wa akili, anatelekezwa. Wajibu wa kumtafutia daktari unapangwa kutekelezwa na Amani baada ya mapinduzi anaposema, "Tutamtafutia daktari wa akili na wauguzi kumsaidia.

Kinaya pia kinajitokeza askari wanapomwita Matuko mwendawazimu lakini wanayoyatenda na kuyasema yakilinganishwa na anayosema Matuko Weye, matendo na maneno yao yanaonyesha kuwa ndio wendawazimu. Askari hawana ushahidi wowote ,kwa kejeli kuwa hukumu yao ni kitanzi bila shaka. (Walibora,2012, uk.83,86).

### 3.1.3.KEJELI

Hii ni mbinu ya kumfanyia mtu dhihaka, stihizai au kumkebehi mtu mwingine. Lengo lake huwa ni kumuudhi, kumkera au kumbeza mtu. Kejeli ni maneno ya kuonyesha dharau kwa mtu. Matuko anawakejeli kwa kufumbia macho dhuluma za Mtemi ambazo zilithibitishwa katika kuwapokonya mashamba,mali, mabinti na hata wake zao. Mambo haya yaliwadhalilisha japo walinyamaza tu. Matuko anashangazwa na wananchi wenzake kwa kuchelea kuchukua hatua yoyote.

Anamkejeli Mtemi na kumkumbusha kwamba anaweza kuporomoshwa, *"Usione weye kwenda mbele kurudi nyuma si kazi"* (Walibora,2012, uk.72). Analikejeli jina la Mtemi anapomwita Mtemi Nasaba Mbaya Mbovu. Hili linnaonyesha kuwa haoni chochote kizuri ambacho kingemfanya yeye kumwita Nasaba Bora. Ndiyo maana anamwita Nasaba Mbaya Mbovu.

Anaukejeli ukoloni mamboleo unaoendelezwa na Mtemi Nasaba Bora Anaafadhalisha mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi. Maana huyu mweusi anadharau Waafrika wenzake vibaya sana. Yaani anawatumia Waafrika wenzake kama kopo la msalani (Walibora,2012, uk.85)

Anawakejeli askari kwa kuupuuza uchunguzi "Hata ninyi ndio mmenichosha zaidi maana mtu na akili zake timamu atawezaje kuwatia mbaroni watoto wema kama hawa? Huoni hapa weye hali ya mahakama kuwa na hatia huku washtakiwa wakiwa hawana hatia? Fikiria hilo weye mwenyewe". Anaendelea kwa kejeli…sijui na sitaki kujua. Na weye mama aliyekuzaa aliwakosea wanadamu. Haki ya Mungu! Kumbuka weye utakuja kuongezewa jina

"marehemu" siku moja! Weye na huyo Mtemi wenu Nasabaa Mbaya-Mbovu… (Walibora,2012, uk.86)

Matuko vile vile anaukejeli ufisadi unaoendelezwa na viongozi wa Sokomoko. Anamwambia Amani,

> "Weye miye nakujua sana miye. Naweza kukufanya waziri wa ufisadi na Magendo ukitaka. Lakini mwanzo sharti utoe kitu kidogo weye. (Walibora,2012,uk.84).

Kauli hii inaonyesha kwamba Matuko alifahamu ufisadi ulivyokita mizizi Sokomoko. Alifahamu vyema kuwa ili mtu apate madaraka au cheo katika Sokomoko, ilimbidi atoe hongo, la sivyo awe na uhusiano wa karibu na walio mamlakani.

Tunashuhudia akiwakashifu Askari kanaeleza jinsi walivyowachosha na wazimu wao.wanamshangaza mzee huyu kwa kuwatia mbaroni watoto wema kama Amani na Imani. Jambo hili analifananisha na hali ya mahakama kuwa na hatia huku washtakiwa wakiwa hawana hatia. Kadhalika anamweleza Askari kuwa mama aliyemzaa alikuwa amewakosea wanadamu. Anamkumbusha kuwa siku moja wataaga dunia na kuwa marehemu pamoja na Mtemi wao Nasaba Mbaya- Mbovu. (Walibora,2012,uk.86)

### 3.1.4 UCHESHI

Hii ni mbinu ambayo hutumiwa kwa kusudi la kufurahisha wasomaji au hadhira katika kazi ya fasihi au kwa kusudi la kuepusha uchovu kwa kutumia maneno, kauli au sentensi zinazosaidia kujenga kichekesho cha aina fulani. Mbinu hii pia hufafanua jinsi kauli hizo zinaweza kumchoma mhusika au wahusika katika kazi ya fasihi. Usemaji wa Matuko akitumia neno *weye*

badala ya *wewe* unaleta ucheshi. Pia anasema *tumetoshwa* badala ya *tumechoshwa* (Walibora,2012, uk.71).

Baadhi ya sifa zake kama mwendawazimu zinachekesha .Kwa mfano, mwandishi anaeleza haya:

> "…alipopewa chakula kilichohitaji kutowelewa, alipenda kufagia kitoweo kikesha mwanzo kabla ya kuanza kukila chakula chenyewe…na kila alipopewa chakula au kinywaji hula na kunywa na kuondoka bila shukrani wala rabsha.
>
> Akipenda kupiga kwata na kusema "mark-time" na "about-turn", "left right" akili zake zilipompeleka miaka ya nyuma huko alipokuwa jeshini. Alipita akitoa simulizi za vituko na visa vya vitani, simulizi ambazo nusu zilikuwa ukweli na zile nusu nyingine vifundiro vya akili yake chakaramu (Walibora,2012, uk.72)

Mhusika huyu anaiita seli "ikulu" na kujirejelea kama "Rais". Anasema:

> "Sitaki kelele hapa kwenye ikulu ya Rais", aliamrisha Mzee Matuko kwa sauti yake ya kitata cha uzee. Miye Mtukufu Rais bado nalala na mwanileteea kelele" (Walibora,2012,uk.84).

Kama tujuavyo, seli ni mahali ambapo kila raia huhofia kupelekwa. Ni mazingira yasiyopendeza kwa kuwa mtu hutengwa na wengine na hunyimwa baadhi ya haki za kimsingi. Ndiyo maana ni jambo linalochekesha kumsikia mhusika Matuko akipaita pahali hapa ikulu.

Kauli yake kuwa anaweza kumfanya Amani waziri wa ufisadi na magendo akitaka kwa masharti ya kutoa kitu kidogo kwanza inachekesha. Mwandishi anaeleza kuhusu kauli hii na kusema:

> “kwa mara ya kwanza tangu kukamatwa Amani alijikuta anatabasamu. Alitaka kucheka akajirudi”. (Walibora,2012,uk.84).

### 3.1.5.TASWIRA

Ni picha ya mtu au kitu inayotokea katika fikra au akili za mtu na mwandishi wa fasihi kwa kutumia maneno**.** Mwandishi anamsawiri Matuko kama mwendawazimu. Anaeleza kuwa Mzee Matuko alikuwa mwendawazimu maarufu ambaye hakuwa na mbele wala nyuma.Hakumiliki chochote. Aliweza kulala popote pale. Alivaa kaptura juu ya suruali, zote mararumararu na kutembea miguu mitupu. Aliboboja maneno ovyoovyo. Riziki yake ilikuwa ya kutopelea na alipopewa chakula kinachohitaji kutowelea, alipenda kufagia kitoweo kikesha mwanzo kabla ya kuanza kukila chakula chenyewe. Alipenda kupiga kwata akili zake zilipompeleka miaka ya nyuma huko alipokuwa jeshini. Alipata kutoa simulizi za vituko na visa vya vitani, simulizi ambazo nusu nyingine vifundiro vya akili yake chakaramu. Maelezo haya yanaonyesha wazi kuwa mzee huyu hakuwa na akili timamu.

Mandhari ya seli yanasawiriwa na mwandishi kama pahali pachafu na pasipo na nafasi ya kumwezesha aliyetiwa ndani kupumua hewa safi. Ni ajabu kwamba Matuko aliweza kulala unono katika hali ile ya kukera. Anaeleza:

> “Seli yenyewe haikuwa seli kitu bali hasa choo cha umma kilichokuwa na lindi refu. Ukuta umeakwa kwa matofali yaliyofyatuliwa na kuchomwa. Paa lake la magome ya miti ya miyaa lilivuja. Palikuwa na tundu dogo ukutani karibu na mtambaapanya la kuleta hewa. Ndani mlikuwamo mnuko kama wa mfu au kitu kilichokufa. Nafasi ya ndani haikutosha mtu mmoja kulala, sembuse watatu. Mzee Matuko Weye alilazimika

> kujipinda kama upinde ili aweze kulala. Imani na Amani walisimama walisimama tu.”( Walibora,2012,uk.83)

Ukatili wa askari pia unasawiriwa wazi na mwandishi wanapomlazimisha Matuko kutoka seli baada ya kudai kuwa hawakumpa hata kiamsha kinywa. Askari anatumia nguvu na kumtupa nje hadi anaanguka na kuumia.

> “Toka. Nilisema mzee toka”, askari Yule mweusi alikuli akaingia ndani na kumkamata Mzee Matuko Weye ukosi na kumtosa nje ya ‘ikulu’ kwa nguvu zake zote. Akaanguka kifudifudi na kuchubuka ngozi magotini. Akaamka ghafla na kuondoka mbio huku akiboboja bo-bo-bo maneno yasiyoandikika wala kutamkika.” (Walibora,2012, uk.87)

## 3.2 MCHANGO WA BILAL KATIKA KUENDELEZA MBINU ZA UANDISHI.

### 3.2.1. TASWIRA

Taswira ni mfano wa vielelezo vya kifikra vinavyoundika akilini kutokana na maelezo Fulani katika kazi ya riwaya, ushairi, tamthilia,hadithi fupi na fasihi simulizi. Kama kawaida, watunzi wa riwaya mara nyingi huunda taswira kutupatia sisi wasomaji picha kamili za kimawazo za yale wanayoyasimulia. Picha hizo huweza kufafanua tukio, hali fulani ya mhusika au kisa fulani (King’ei na Amata,2001).Mbinu za tashbihi na sitiari husaidia mno katika kujenga taswira. Mbinu hii humsaidia pakubwa msomaji au msikilizaji katika kuelewa mandhari na vitu vinavyoonekana. Hutilia mkazo au msisitizo kauli zilizokwisha kutolewa. Katika riwaya ya *Mkamandume*,mwandishi amemsawiri Bilal kama mwendawazimu. Maelezo kumhusu mhusika huyu yanaeleza kuwa bila shaka ni mwendawazimu. Anasema,

> “…kinyago cha mtu kilikuwa kimekaa juu ya kiti mbele yake. Upongoo wa mtu, mweusi wa rangi ya maumbile na wa guo la uchafu alilovaa kwa kutojitia maji kwa miezi kama si miaka. Mwili wake ni mwili wa chungu kisichotoka mekoni. Alikuwa kajitupia shuka kwa mtindo wa lubega, shuka ambayo upya wake ilikuwa nyeupe lakini sasa imechukua rangi isiyo na jina. Na kisha imeshirai mafuta, majasho, mavumbi na mapuuza… Mwili wake wote ulikuwa umemwota ukurutu, upele na vidonda.miuundu miembamba kama spoki na miguu imegawana viatu vibovu, wa kulia umevalia maklipa yaliyochanikachanika na kushoto malapa yaliyokatika kanda. Bahasha yake ya matambara na jumla ya vitu anavyoviokota majaani na kwenye mapipa ya taka alikuwa kaiweka chini sasa. Ananuka utadhani fungo! (Mohamed,2013,uk.242).

Uchafu wa mwili, mavazi, kusokotana kwa nywele, kubeba matambara aliyookota mapipani na uvundo wake ni mambo yanayooshesha kuwa mtu huyu hana akili timamu.

Vilevile, baada ya kusimulia kadhia yake, mwandishi anaeleza:

> ‘‘… Kufumba na kufumbua, alikuwa kasimama uchi kama alivyozaliwa. Na kabla mwemeo huo haujapita vyema machoni mwa waliokuwepo, alimshika bamkubwa wake kwa mkono wa kulia na mkono wa kushoto alikamata ile picha na kuanza kuikojolea, huku akisema,”Nitakukojolea kila siku mpaka nitakapokufa. Jicho kwa jicho! Kisasi changu! Huyu ndiye aliyesababisha yote haya! Huyu ndiye adui wa kila mtu!” vituko hivi vinadhihirisha kuwa bila shaka Bilal hana akili timamu. Kuvua nguo hadharani bila kujali alipo na waliopo na kuikojolea picha kwa nia ya kulipiza kisasi kwa mwenye picha kana kwamba mwenye picha anafahamu yanayoendelea ni ishara za wendawazimu’’. (Mohamed,2013 , uk.251)

Maelezo haya yanamsawiri Bilal kuwa mwendawazimu haswa. Anavyooneka mchafu kupindukia, alivyovalia matambara na maneno yake yanathibitisha hali yake ya uchakaramu.

### 3.2.2 KEJELI

Hii ni mbinu ya kumfanyia mtu dhihaka, stihizai au kumkebehi mtu mwingine. Lengo lake huwa ni kumuudhi, kumkera au kumbeza mtu. Kejeli ni maneno ya

kuonyesha dharau kwa mtu. Bilal anamkejeli Soud anapofahamu kuwa Soud hamtambui. Anamwambia,

> “ Hunijui? Alianza huku akionyesha mshangao. “Aaaa, bila shaka hunijui. Ha ha ha…nani anayetaka kumjua shetani? Nani anayetaka kumjua mwendawazimu? Ha, ha, ha …wuuu…waw! (Mohamed,2013 , uk.242).

Kauli hii ya Bilal inadhihirisha kwamba anafahamu unyanyapaa unaowakumba wanyonge katika jamii. Anaelewa kuwa hakuna mtu anayetaka kushirikishwa au kuwa na uhusiano nao. Kila mtu hujitenga nao. Ndiyo sababu akamwambia “...nani anayetaka kumjua shetani?”

Kadhalika, Kinibu anapoonyesha dharau kwake anapoitisha bia, Bilal anamdhihaki,

> “Watu wengine bwana …nini wewe? Kama hatukununua sisi bia huli wewe! Tazama vile! Muuzapombe ana heri gani? (Mohamed,2013 , uk.244-245).

Bilal anaukejeli mfumo mbaya wa uongozi uliowatukuza wanajeshi na askari polisi na kuwadharau waalimu kwa kusema, “Mara walimu tukajikuta jaani ambako kila mwenye taka zake alikuja kutupa. Wacha dada zetu waingie wazimu. Hata mpumbavu kiasi gani, maadamu alikuwa mwanajeshi alipewa au alimchukua mwanamke yeyote”.

“Kwa kweli ilifika hadi kwamba ukienda kuposa pahala kwanza utaulizwa kazi yako. Ukiwa wewe mwanajeshi hata hukuchunguzwa kama wewe una akili timamu au la, mwizi, lusu au mnyang’anyi, ulipewa mtoto wa watu tu. Lakini akina sisi wapi. Na hata kwa bahati kama tulipata mke kuoa, ilibidi

tuzilinde nyumba zetu kwa silisili. Na haikusaidia kitu. Mke wangu alichukuliwa na Brigadia nakusudia" (Mohamed,2013, uk.250).

### 3.2.3 MBINU REJESHI

Hii ni mbinu ambapo mtunzi anatangulia kuandika mambo ambayo kwa mantiki ya msomaji yangekuja nyuma. Pia inaweza kuhusu mhusika fulani kurejelea mambo ambayo yalitendeka kitambo na ambayo hayamo katika muktadha wa wakati unaohusika. Mbinu hii husaidia kuelewa chanzo cha matukio fulani ambayo yanatendeka katika hadithi na pia kuifahamu historia ya mhusika na mchango wake kwa hali, tabia na matendo yake.

Katika mazungumzo baina ya Bilal na Soud, Bilal anamweleza Soud kwamba kuna wakati alikuwa na akili zake timamu. Anamweleza , *Mimi nilikuwa na akili nyingi kama wewe pia au zaidi…*, anakumbuka kadhia yake ambayo kwa hakika ndiyo ilisababisha wendawazimu wake. Anamsimulia Soud jinsi alivyokuwa mwalimu wakati ualimu uliheshimiwa na kuhusudiwa. Anasimulia jinsi mambo yalivyobadilika wakati utawala uliokuwapo ulitukuza uanajeshi na kazi ya askari polisi, anaeleza jinsi walimu walivyodhalilishwa. Yeye mwenyewe alidhurika na mfumo huo kwani mkewe Bishara alichukuliwa na Brigadia. Tukio hili liliubadilisha mkondo wa maisha ya Bilal kabisa. Kadhia hii inatuwezesha kufahamu lililomtamausha Bilal na kusababisha wendawazimu wake.

Bilal anamsimulia Soud jinsi mwalimu wao Seyyid Kakhtan alivyodhulumiwa kwa kuachishwa kazi bila hatia. Hili lilimfanya mwalimu wao kutaabika sana. Anaeleza, "…namkumbuka mwalimu wetu

mmoja…Nani vile? Alijivuta kufikiri, “Nani vile?”…Aaa! Seyyid Kakhtan…marehemu maskini, mungu amlaze pahala pema huko aliko…walimdhulumu vibaya vibaya. Walimwachisha kazi na kumwacha atambe na njia ugenini- alikuwa akitwambia, kufanikiwa masomoni si kufanikiwa na maisha.” (Mohamed,2013 ,uk.244).

### 3.2.4 DAYALOJIA

Haya ni mazungumzo baina ya wahusika. Ni kitendo cha kuambizana au kusemezana baina ya watu wawili au zaidi. Bilal na Soud wanashiriki katika mazungumzo ambayo yanampatia Bilal fursa ya kummwagia Soud dukuduku lake. Jambo hili ni muhimu kwa sababu linatuwezesha kufahamu mizigo ambayo mhusika huyu amebeba.Mazungumzo kati ya Bilal na Soud yanatupa mwangaza kuwa Bilal kwa kiasi fulani ni mhusika mwenye nafsi mbili, yaani kama mtu mwenye akili razini na pia mwendawazimu. Hali hii inamwezesha kuwa kipaza sauti cha mwandishi. Ametumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu katika jamii ambao wahusika wengine anachelea kutoa. Kwa mfano katika (Mohamed,2013 ,uk.243)

> *Mimi nilikuwa na akili nyingi kama wewe pia au zaidi…*
>
> *“Najua”*
>
> *Lakini ncha za akili na wendawazimu hazitengani kwa masafa makubwa mno… au unasemaje?*
>
> *“Kweli”*
>
> *“Unakubali?”*
>
> *“Ndiyo nakubali kabisa”*
>
> *Mbona wewe si mwendawazimu basi?”*

*Inategemea unaouita wendawazimu. Kila mtu ana wendawazimu wake . au labda mimi sikuwa na akili nyingi kama wewe"*

Pia , anajadiliana na Soud kuhusu dhana kuwa binadamu ni wanyama,wako uchi, na ni mwendawazimu. Maovu aliyofanyiwa na walio mamlakani ya kunyang'anywa bibi kwake ni ithibati tosha kuwa wanadamu wana chembechembe za unyama ndani yao.Nguo humsitiri mtu kijuujuu tu. Mtu afanyapo matendo ya aibu au yakiukayo maadili ya jamii, hupatwa na aibu kubwa. Matendo hayo humwanika na kujulikana hulka na mienendo yake. Hali hii ni sawa na kumvua nguo na kumwacha uchi. Ndiyo maana Bilal anasema kuwa nguo humsitiri mtu kijuujuu. Nguo hazisitiri matendo yanayodhihirisha kama mtu ana utu. Kwa vile mtu ni utu, matendo yasiyodhihirisha utu humwacha mtu uchi.

Bilal anaendelea kumhusisha Soud katika mjadala muhimu.Anajadiliana na Soud kuhusu dhana kuwa binadamu ni wanyama, wako uchi, na ni mwendawazimu. .

*"Niambie, hivi wewe ni mnyama?"...*

*"Hapana, mimi sidhihaki- yaani nakuuliza kweli kama wewe mnyama au..."*

*"Asili yangu labda"*

*"Ah yes! Aliruka Bilal. "Ndiyo sisi sote wanyama kwa asili. Lakini chembe ya asili haitoki ukiwa nnayo mwilini..." kama virusi... kama virusiiiiiiiiii!" Alicheka na kicheko chake kikachukuliwa na hewa kuelea na ndege waliokuwa juu ya anga la bahari Hindi wakidowea ngawira.*

*Unambie pia kama wewe pia ni mwendawazimu?*

*Soud alicheka tena. "Kwa bahati mbaya sina jicho hilo",alijibu kwa uchangamfu.*

> *"Ukimwona mtu amevaa nguo,sivyo alivyo katika dhahiri ya mambo. Nguo hunsitiri kijuuujuu tu. Ukimtazama sana utamwona uchi. Uchi kabisa!" (*Mohamed,2013 uk.247)

Mazungumzo haya ya ana kwa ana kati ya Soud na Bilal yanatuwezesha kumhukumu Bilal kama mhusika mwenye nafsi mbili: ya uchakaramu na ya mtu mwenye akili timamu.

### 3.2.5. BALAGHA

Huu ni umbuji wa kutumia lugha ya kuvutia katika uandishi au mazungumzo. Ni maswali yanayoulizwa ila hayahitaji jibu. Maswali haya hayamhitaji msomaji au msikilizji kufikiria ili kupata jibu la swali hilo. Jibu huwa limo akilini mwa anayeulizwa au anayesoma kazi husika au huwa tayari analijua. Hisia za ndani au mawazo ya msemaji ni kulifanya jambo fulani kuonekana wazi kwa hadhira au kwa msomaji na kinachozungumziwa katika swali hilo kuangaliwa kwa makini. Maudhui fulani pia huweza kuwasilishwa kwa maswali haya.

Bilal anamwuliza Soud maswali mbayo yanamfanya Soud na pia wasomaji kutafakari zaidi kuhusu masuala ambayo Bilal anazungumzia.

> *"…hunijui? Alianza huku akionyesha mshangao. "Aaaa, bila shaka hunijui. Ha ha ha…nani anayetaka kumjua shetani? Nani anayetaka kumjua mwendawazimu? Ha, ha, ha …wuuu…waw*! (Mohamed,2013 uk.242)

Kauli hii ya Bilal inadhihirisha kwamba anafahamu unyanyapaa unaowakumba wanyonge katika jamii. Anaelewa kuwa hakuna mtu anayetaka kuhusishwa au kuwa na uhusiano nao. Kila mtu hujitenga nao. Ndiyo sababu akamwambia ,

*"...nani anayetaka kumjua shetani"*

*"Ndege hutua juu ya miti, akili za binadamu huelea hewani…hakika binadamu tumo hasarani! "Unaziona akili zetu zinavyoogelea hewani? Yaani yangu, yako, yake…" akaashiria upande wa mhudumu wa baa, Kinibu.*

*"Aaa, hata mimi hunijui? Hata mimi? Alikuwa akisema hivyo kwa kuiga sauti fulani ya kitoto. Kwa nini hata wewe?" aliemewa Soud. "kwa sababu mimi Bilal…"* (Mohamed,2013, uk. 243)

*Bilal aligeuka na kubwata kwa hamaki. "Watu wengine bwana …nini wewe? Kama hatukununua sisi bia huli wewe! Tazama vile! Muuzapombe ana heri gani? (*Mohamed,2013, uk.244*)*

Maneno haya yanaonyesha kuwa Bilal alifahamu kuwa Kinibu alimdharau. Hata vivyo, alitaka kumkumbusha kuwa wanadamu hutegemeana kwani ni kutokana na kununua kwao ambapo yeye hupata riziki. Kwa hivyo, asiwadharau wateja.

> *"Kuna ubaya gani kuwa mnyama? Kuna hasara gani kupoteza akili yote? Kuna aibu gani kwenda uchi? Sote si tulizaliwa wanyama na kila siku tunadhihirisha unyama wetu. Kwa ushahidi kamili sisi sote ni wendawazimu watupu. Sote sisi tulizaliwa uchi na tunakwenda uchi bila kujiona- nguo au bila ya nguo! Tatizo liko wapi basi?"*

Bilal anapozungumza kuwa sote tulizaliwa wanyama na kila siku tunadhihirisha unyama wetu, kauli hii ni ya kweli tukirejelea maneno na matendo ya baadhi ya wahusika katika riwaya . kwa mfano, (Mohamed,2013, uk.245)

Soud anashangaa yu wapi mwendawazimu humu? Soud alimtafuta Bilal kimoyomoyo. Alipomtazama kwa waziwazi, aliuhisi uso wake umejaa nuru ya akili. Ile nuru ilithibitisha kwamba maneno ya Bilal yakitoka katika kina

cha ndani kabisa ya nafsi yake. Yalikuja na hisia na hamasa na ukweli mbichi unaondondoka damu.

### 3.3. HITIMISHO

Sura hii imeshughulikia uhakiki wa mchango wa wahusika Matuko Weye na Bilal katika kukuza mbinu za uandishi katika riwaya teule. Tumethibitisha kuwa wamefanikisha kuendeleza na kukuza mbinu za uandishi. Wameendeleza mbinu zikiwemo balagha, kinaya, kejeli, ucheshi, taswira, mbinu rejeshi na dayalojia. Sura inatofuata ya nne imechunguza namna wahusika hawa wamefanikisha dhamira ya waandishi wa riwaya teule.

# SURA YA NNE

# UCHUNGUZI WA MCHANGO WA WAHUSIKA WENDAWAZIMU KATIKA KUENDELEZA DHAMIRA YA MWANDISHI

## 4.0 UTANGULIZI

Kulingana na Njogu na Chimera (1999), dhamira ni mojawapo kati ya vipengele vilivyounda maudhui katika kazi ya fasihi. Vipengele vingine ni migogoro, ujumbe, falsafa, msimamo na mtazamo wa mwandishi. Wamitila (2008) naye anaeleza kuwa dhamira ni yale mawazo makuu ambayo yanamsukuma mwandishi wa kazi ya fasihi kuyaandika na kuyabainisha vizuri katika kazi husika. Kadhalika dhamira ni lengo kuu la mtunzi wa kazi ya fasihi ambalo analenga lifikie hadhira aliyoiteua (Kezilahabi,2003). Vilevile mtaalamu huyu anaeleza kuwa si kila mtu anaweza kuwa ni hadhira ya kazi fulani ya fasihi kwa sababu kila mwandishi huandika kazi yake akiwa na lengo kuu ambalo anataka hadhira yake ilipate. Kulingana naye lengo hilo kuu ndilo linalofahamika kama dhamira ya mwandishi.

Kwa mujibu wa Ali (2017) dhamira ya mwandishi hugawika katika sehemu mbili kuu ambazo ni dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Dhamira kuu ni ile ambayo inakuzwa na kujitokeza katika kazi nzima ya fasihi na dhamira ndogondogo ni zile ambazo zipo kwa ajili ya kukamilisha dhamira kuu.

Fasihi ni kioo cha jamii. Kioo hiki hakionyeshi sura ya jamii iliyo tulivu bali huonyesha sura ya jamii ya watu walioshughulika na kazi mbalimbali wenye nasaba tofauti na wanaotoka katika matabaka mbalimbali. Mwanafasihi ni

mwanajamii na ndiyo maana maswala yanayoendelezwa katika jamii hudhihirika katika fasihi. Kile tunachokisema katika fasihi huwa tunakifanikisha na matukio ya kawaida katika jamii.

Waandishi Walibora Ken na Said Ahmed Mohamed wameziandika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* zikisheheni ukwasi mkubwa wa riwaya zenye mafunzo kwa jamii. Dhamira zinazofanikishwa na wahusika Matuko Weye na Bilal katika riwaya hizi zimeshughulikiwa kama ifuatavyo:

## 4.1.0 JINSI MHUSIKA MATUKO WEYE ANAVYOENDELEZA DHAMIRA YA MWANDISHI .

### 4.1.1 MAONEVU DHIDI YA WANYONGE

Mwandishi wa riwaya amemsawiri Matuko ili kupitia kwake aweze kufafanua waziwazi maonevu ya wanyonge katika hafla ambayo wahusika wanaoonekana wakiwa na akili timamu hawawezi kusema. Anatumia fursa hii kumshambulia Mtemi.Anasema bila woga,

> Tumetoshwa na dhuluma za Bwana Mtemi. Anatudhulumu sana sana. Anatupokonya mashamba,mali, mabinti na hata wake zetu wenyewe. Weye mwananchi huoni tunavyodhalilishwa.Huoni weye?Umefumba macho tu weye? (Walibora,2012, uk.68)

Wahusika wengine katika riwaya hii kama Balozi wanamsifu mtemi, hawamkosoi au kuukosoa udhalimu wake. Badala yake anammiminia sifa kama vile,ni kiongozi mwenye utambuzi na anayetabasuri kuliko wazungu wote wakiwekwa pamoja. Kadhalika, anadai kuwa anatambulikana kwa fadhili na utu wema wake katika Tomoko nzima na Kiongozi aliyeteuliwa na Mungu mwenyewe. Ni bayana kwamba Balozi na wengineo walimvisha Mtemi

kilemba cha ukoka. Lakini Matuko ametumiwa na mwandishi kumwambia Mtemi na Wanasokomoko ukweli mchungu. Matuko aliyedhaniwa mwendawazimu anamwambia Mtemi na Askari wake ukweli ambao wengine wanaaogopa kusema.

### 4.1.2 KUPIGANIA HAKI

Matuko weye anajaribu kuwashawishi wananchi wamuunge mkono kupinga udhalimu wa Mtemi. Anapotiwa kizuizini anakutana na Amani na Imani. Anamwambia Imani kuwa anafaa aolewe, ajifungue watoto watakaoikomboa nchi yao kutoka kwa mkoloni mweusi. Naye Amani anaahidiwa kufanywa waziri kwa masharti ya kutoa hongo. Jambo hili linaonyesha kuwa Matuko anafahamu kuwa vyeo katika nchi yao vinapatikana kwa hongo na hivyo anaukashifu mfumo huu.

> “Kwa nini weye umefumba macho? Twataka aondoke madarakani huyu nduli Mtemi Nasaba Mbaya mara moja ili… usione weye kwenda mbele kurudi nyuma si kazi weye. Usione..” (Walibora,2012, uk.72)

Anaendelea kutahadharisha wananchi kuwa afadhali mkoloni mzungu kuliko mweusi. Maana mkoloni mweusi huwadharau Waafrika wenzake vibaya sana. Yaani anawatumia kama kopo la msalani.” (Walibora,2012,uk.85)

## 4.2.0 MCHANGO WA BILAL KATIKA DHAMIRA YA MWANDISHI.

### 4.2.1 MAONEVU DHIDI YA WANYONGE

Mohamed (2013) amemsawiri Bilal kama mhusika katika riwaya yake ili kupitia kwa mhusika huyu, aweze kufafanua waziwazi masaibu ya wanyonge katika jamii.Wendawazimu ni miongoni mwa watu wanaokumbana na

unyanyapaa katika jamii. Bilal anapomkuta Soud Starehe Club, anagundua kuwa Soud hamtamfahamu. Anachukua fursa hii kumweleza kuwa sababu ya kutomtambua ni kuwa alikuwa mwendawazimu. Hili linaonyesha kuwa mwandishi anaukashifu unyanyapaa dhidi ya wanyonge hasa wendawazimu katika jamii.

### 4.2.2 ATHARI ZA UONGOZI MBAYA

Mwandishi pia anaangazia na kutoa funzo kuhusu athari za uongozi mbaya. Kutokana na uongozi mbaya, viongozi wanawagawanya wananchi kwa misingi ya matabaka.Bilal anafafanua kwamba Uanajeshi ulitukuzwa na kazi ya Ualimu ikadharauliwa. Ndiyo maana, kwa vile alikuwa mwalimu, bibi yake Bishara alitwaliwa bila hiari yake na kuozwa Brigadia. Anaeleza kwa uchungu kuwa anawalaumu waliohalalisha udhalimu huu. Haya aliyopitia na kusababisha wehu wake ni matokeo ya uongozi dhalimu.

### 4.2.3 KUKASHIFU UJINGA

Mohamed anakejeli namna binadamu anavyojidanganya kwamba amejisitiri kwa kujivika mavazi wakati yuko uchi. Anatukumbusha kuwa binadamu anaweza kuwa uchi na nguo haziwezi kuusetiri uchi wake. Haya hutokea wakati binadamu ametenda mambo ya aibu, udhalimu ambayo humfanya kuwa uchi yaani kuaibika. Anamtumia Bilal kueleza haya kwa nia ya kukashifu matendo maovu katika jamii. “Na je, hapo ulipo upo uchi?... Ungekuwa na jicho la x-rays kama mimi, ungeona watu wote wanatembea uchi, kila siku, kila wakati….” (Mohamed,2013, uk.247).

Vilevile, anakejeli jinsi binadamu wanavyodai kuwa na urazini kwa kueleza kuwa kila mtu ana wazimu wake na hakuna mja aliyekamilika. Maovu wanadamu wanayofanya yanadhihirisha kuwa ni wanyama,asili yao ni wanyama na virusi vya unyama vinajidhihirisha kutokana na vitendo vyao vya kikatili. (Mohamed,2013, uk.246)

## 4.3.0 HITIMISHO

Wahusika hawa wamechangia katika kufanikisha dhamira ya waandishi ya kusuta maovu katika jamii na kutuwezesha kuwatathmini wahusika wendawazimu kwa jicho pevu. Matuko Weye na Bilal wameweza kupinga dhuluma ambazo watu wenye akili timamu wanachelea kupinga. Wanathibitisha kuwa wao ni kipaza sauti cha waandishi . Walibora na Mohamed wamewatumia kama chombo cha kuyalipulia majipu yao, dhana inayojitokeza wazi katika maudhui na dhamira na kuthibitisha umuhimu wa kuwachora wahusika hawa katika kazi zao.

Sura inayofuata ni ya tano na ya mwisho.Sura hii itahitimisha tasnifu. Itashughulikia muhtasari, hitimisho, matokeo na pia mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.0 UTANGULIZI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya teule: *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* . Malengo ya utafiti huu ni: Kuchunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika kufanikisha maudhui ya riwaya teule, kubainisha mchango wa wahusika hawa katika kuendeleza mbinu za uandishi pamoja na kuthibitisha jinsi wahusika wendawazimu wanafaulisha dhamira ya waandishi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi nafsia ambayo mwasisi wake Freud (1915) anaifananisha kazi ya fasihi na ndoto. Kwa kuwa riwaya, tamthilia na ushairi ni kazi bunifu, kazi hizi zinaashiria matumaini na matamanio ya mwandishi. Nao wahusika wanaopatikana katika fasihi ni wanadamu wanaoishi katika ndoto na njozi za mwandishi. Hawa ni kama vile wanadamu wanaoshirikiana na mwandishi katika matarajio na matatizo yake. Aidha, anaiona kazi ya fasihi: maudhui yake, mtindo na wahusika wake kuwa ndoto inayoweza kumliwaza anapoipitia. Vitengo hivi vya fasihi humwathiri msomaji kikweli licha ya kwamba anayoyasoma ni ya kubuni.

Kulingana na fikra za Freud, inakusudiwa kuwa mhakiki anatazamiwa kuichanganua kazi ya fasihi kwa lengo la kubainisha wazi Saikolojia ya mtunzi. Msomaji anaweza kujisoma katika maandishi anayoyasoma. Kutokana na usomaji, msomaji anaweza kusherehekea pamoja na nafsi yake au kuililia

nafsi hiyo. Ataonyesha uafikiano uliopo kati ya tajriba zake na tajriba za wahusika anaokabiliana nao.Freud anathibitisha kwa shauku kuwa wahusika katika kazi ya fasihi hukua na kubadilika kutokana na misukumo mbalimbali ya maisha yao. Pia, nadharia hii inamhamasisha mhakiki wa fasihi kutilia maanani mshikamano uliomo katika kazi ya fasihi hata ile ambayo sentensi zake hazionyeshi muwala na mshikamano waziwazi.

Utafiti huu umeongozwa na mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ni: msanii huathirika na mazingira anamoishi hivi kwamba atakapoiandika kazi ya kifasihi atakuwa kama anaeleza imani, ndoto na tamaa zake. Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, mhusika Matuko Weye anajitokeza waziwazi kueleza yanayomkera kuhusu uongozi wa Mtemi Nasaba Bora. Anaeleza jinsi walivyochoshwa na dhuluma za Bwana Mtemi. Anapowekwa seli anachukua fursa ile kupinga kuwekwa ndani kwa Amani na Imani na pia kuwakemea askari. Anataka kujua kwa nini wanamwachilia huru bila kumpeleka kortini kushtakiwa kama kweli alikuwa na makosa.Katika riwaya ya *Mkamandume,* Bilal pia anasimulia jinsi alivyodhulumiwa na kunyang'anywa mke na Mkuu wa Jeshi.

Mhimili wa pili ni kuwa kazi ya fasihi huonyesha mwandishi amebeba mizigo gani moyoni na analenga uchafu gani katika jamii. Huwa ni chombo cha mtunzi cha kuyalipulia majipu yaliyomlemea. Wahusika Matuko Weye na Bilal katika riwaya teule wanalalamika kuhusu dhuluma wanazofanyiwa na viongozi. Mhimili wa tatu ni kuwa kuna uhusiano kati ya saikolojia-changanuzi na mtindo katika kufafanua hali halisi ya maisha ya binadamu.

Waandishi wa riwaya hizi ambao ni Walibora na Mohamed wamewasawiri wahusika wendawazimu katika kazi zao ili kukejeli maovu yaliyo katika jamii.

Utafiti huu ulifanyika kwa mapana katika maktaba ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta ambapo ulihusisha kusoma na kuchanganua matini. Mbinu hii ilitumika ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Aina mbili za data zilikusanywa ambazo ni data ya msingi na data ya upili. Data ya msingi ilikusanywa kutoka katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Riwaya hizi zilichanganuliwa kwa kina.

Data ya upili ilikusanywa kutoka machapisho mbalimbali ya waandishi. Data hii ilichangia kudhihirisha data ya msingi. Katika hali hii, ilisaidia katika na kufikia lengo la utafiti huu. Data hii ilipatikana baada ya kusona makala mbalimbali maktabani kama vitabu, majarida, makala, magazeti na mtandao ili kupata data iliyofaa ya mada ya utafiti katika riwaya zilizoteuliwa kwa kuzingatia misingi ya nadharia teule. Vitabu vinavyofafanua nadharia ya Uchanganuzi Nafsia vilisomwa ili kubainisha mihimili iliyoongoza kuchanganua data ya utafiti. Tafiti zilizotangulia zinazohusiana na nafasi ya wahusika wendawazimu zilichunguzwa ili kupata data iliyoufaa utafiti huu.

**5.1 MUHTASARI WA TASNIFU.**

Kazi hii iliwasilishwa katika sura tano.Sura ya kwanza inajumlisha sehemu ya usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia ya utafiti na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imechunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika kukuza maudhui ya riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* ambao ni Ken Walibora na Said A. Mohamed, dhana ya uhusika na wahusika katika fasihi na kuchunguza kwa kina wahusika wendawazimu katika fasihi kisha kubainisha wahusika wendawazimu katika riwaya teule ambazo ni *KidagaaKimemwozea* na *Mkamandume.*

Sura ya tatu imeshughulikia uhakiki wa mchango wa wahusika Matuko Weye na Bilal ambao ni wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* katika kuendeleza mbinu za uandishi riwaya teule.

Sura ya nne inachunguza nafasi ya wahusika wendawazimu katika kufafanua dhamira ya waandishi wa riwaya za *Kidagaa Kimemwozea Mkamandume*. Ilichunguza jinsi wendawazimu Matuko Weye na Bilal wamesawiriwa kama kipaza sauti cha waandishi cha kukashifia maovu yanayotekelezwa na waandishi.

Sura ya tano imehitimisha tasnifu. Hitimisho limetoa muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye sura hii inaeleza matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, matatizo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi yanatolewa. Viambatisho mbalimbali pia vinafuata sura hii.

## 5.2 MATOKEO YA UTAFITI

Malengo ambayo utafiti huu ulikusudia kuyatimiza ni matatu ambayo ni pamoja na: kuchunguza mchango wa wahusika wendawazimu katika

kufanikisha maudhui ya riwaya teule. Utafiti huu umebainisha kuwa wahusika wendawazimu katika *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume* wamechangia kukuza maudhui ambayo ni pamoja na vita dhidi ya udhalimu, uongozi mbaya, elimu na ukombozi.

Wahusika wengi katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* wamedhulumiwa na Mtemi Nasaba Bora. Matuko Weye hata baada ya kuwa baadhi ya mashujaa walioshiriki Vita vya Pili vya Dunia na kuwa mzee anakamatwa na askari kwa kisingizio kuwa alivuruga Sherehe za wazalendo. Matuko analalamika kuwa Mtemi anawadhulumu wananchi. Analalamikia kung'anyangwa kwa mashamba, mali, mabinti na hata wake wao na Mtemi. Analalamikia kutiwa seli na kuachiliwa kwake bila kufikishwa mahakamani. Anawatetea Amani na Imani waliowekwa kizuizini kwa tuhuma za kukiua kitoto Uhuru.

Mwalimu Majisifu pia anaunga mkono vita hivi anapomweleza mtemi kuwa si haki kuwazuilia Amani na Imani kwa tuhuma za mauaji wakati Majisifu ana ithibati kutoka kwa madaktari kuwa kitoto Uhuru kilifariki kutokana na ugonjwa wa kichomi.

Katika riwaya ya *Mkamandume,* ni wazi kuwa Bilal na mwalimu wake Seyyid Khahktan wanaathirika na ukatili wa viongozi wao. Bilal anaeleza kuwa mwalimu wake aliachishwa kazi bila sababu na kuachwa akitaabika. Mateso yale mwalimu huyu alipitia yalitokana na ukatili. Mkewe Bilal, Bishara aliyempenda kwa dhati alichukuliwa na Brigadia. Hali hii ilitokana na utawala kutukuza kazi ya Uanajeshi na kuudhalilisha Ualimu. Walimu walidunishwa.

Hakuna hatua inayochukuliwa kwa Brigadia kwani waliokuwa mamlakani waliihalalisha hali hiyo.

Uongozi mbaya ni maudhui mengine yaliyoendelezwa na wahusika hawa. Hili linadhihirishwa na matumizi mabaya ya vyombo vya dola. Askari wanamkamata Matuko, kumwekwa seli na kumchapa kwa sababu ya kumshambulia Mtemi hadharani kuhusu maovu anayowatendea. Hii ni ishara ya uongozi mbaya.Amani na Imani wanashikwa kwa tuhuma za kukiua kitoto ambacho Amani alibambikizwa na Mtemi na kufungiwa seli. Huko wanapata kichapo cha mbwa.

Utawala mbaya katika riwaya ya *Mkamandume* unasababisha mateso kwa wanyonge. Bilal ananyang'anywa mkwewe mpendwa na Brigadia na hana wa kulilia kwani utawala uliopo unahalalisha yaliyo haramu. Mwalimu wake aliachishwa kazi bila sababu na kuachwa akitanga na jua na kuteseka. Hata katika familia, Mkamandume anaongoza familia yake kwa njia isiyofaa. Ana ubinafsi kwa sababu anamuuza ng'ombe wake wa pekee aliyekuwa tegemeo la familia yake na kuondoka nyumbani na kumwacha bibiye akiteseka. Bintiye Viwe anaporingwa anamfukuza nyumbani. Naye bintiye Time anamkataza kuolewa na Soud kijana aliyempenda tangu utotoni wake.

Ukombozi umeangaziwa na wahusika Matuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na Bilal katika *Mkamandume.* Wamejizatiti kuwakomboa wananchi wenzao. Katika sherehe ya Sikukuu ya Wazalendo, Matuko anajitolea kuikomboa nchi yake kwa kuupinga udhalimu kwa kuwazindua wananchi wenzake kuhusu maovu wanayotendewa na Mtemi, jambo

linalomfanya akamatwe na askari na kuwekwa seli. Anajijasiri na kuwaeleza askari kuwa hata wakimpiga risasi wajue kwamba wakimwua watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi. Wataikomboa nchi yao kutoka kwa Mkoloni Mweusi, ukombozi wa pili.(Walibora,2012,uk.87).

Katika riwaya ya *Mkamandume,* Bilal anamkomboa Soud kimawazo. Anamweleza kuwa ncha za akili na wendawazimu hazitengani kwa masafa makubwa mno, jambo ambalo Soud anakubaliana nalo. Kadhalika, anamweleza Soud kuwa mwalimu wake, marehemu Seyyid Khakhtan aliwahi waeleza kuwa kufanikiwa maasomoni si kufanikiwa katika maisha (Mohamed,2013,uk.244). Soud pia analiona jambo hili kuwa la kweli. Anaendelea kumweleza Soud kuwa sisi sote ni wanyama kwa asili. Lakini chembe ya asili haitoki ukiwa nayo mwilini. Aidha, anamdokezea kuwa pombe ni mkojo wa Firauni tu, ambao ukiingia mwilini mwako unageuka mkojo wako mwenyewe wakati huohuo na kukuendesha chooni kila mara, na ndani unaacha sumu inayobakia kichwani mwako milele. (Mohamed,2013,uk.246)

Bilal anamfafanulia Soud ukweli kuwa nguo humsitiri mtu kijuujuu tu. Ukimtazama utamwona uchi. Soud aliyaona mawazo ya Bilal kuwa ukweli akiyalinganisha na dukuduku lake analolala nalo na kuamka nalo. Kadhalika, anaitukuza kazi ya Ualimu.Anamweleza kuwa hata manabii na mitume wote walikuwa walimu. Walitumwa na Mwenyezi Mungu kuja kuifunza dunia. Madai yake ni ya kweli. Kinibu, mhudumu pale Starehe Club alipoonekana kumdharau alimweleza wazi kuwa kama hawanunui bia yeye hawezi pata

riziki. Aliyanena haya kumjuza kuwa waja hutegemeana na hakuna haja ya kumdharau mwenzako.

Maudhui ya elimu yanaendelezwa na mhusika Bilal anapoeleza kuwa alipata elimu iliyomwezesha kuwa mwalimu. Anaeleza pia kuhusu mwalimu wake Seyyid Kakhtan aliyedhulumiwa kwa kuachishwa kazi bila sababu. Anaeleza pia jinsi utawala ulivyowabagua watu kulingana na elimu yao. Waliopata mafunzo ya Uanajeshi walitukuzwa na ya Ualimu wakaja kudharauliwa.Hili linadhihirishwa wakati bibi yake anachukuliwa na Brigadia lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi ya unyama wa Brigadia. Kutokana na hali hii, wasichana wao walipendelea kuolewa na wanapolisi.

Utafiti huu pia umefaulu kubainisha mchango wa wahusika hawa katika kuendeleza mbinu za uandishi.Wahusika wendawazimu ambao ni Matuko na Bilal wamechangia kukuza mbinu za uandishi kama vile taswira, kejeli , mbinu rejeshi, kinaya, balagha, dayalojia na ucheshi.

Waandishi wa riwaya hizi wametumia mtindo wa taswira kutuchorea picha za wendawazimu hawa. Kutokana na mavazi yao, maneno na vitendo vyao inadhihirika kuwa hawana akili timamu. Kuhusu mhusika Matuko tunaelezwa "… hakumiliki chochote. Hakuwa na shamba, au mke, mwana wala binti. Aliweza kulala popote pale. Alivaa kaptura juu ya suruali, zote mararumararu.

Tangu atoke vita Burma hakuwahi kuvaa viatu. Alikwenda Burma kupigania Uingereza katika Vita vya Pili vya Dunia akiwa na akili zake razini. Aliporudi alikuwa mwenye wazimu. Aliboboja maneno ovyoovyo. Riziki yake ilikuwa

ya kutopelea…. Alipopewa chakula kinachohitaji kutowelea, alipenda kufagia kitoweo kikesha mwanzo kabla ya kuanza kukila chakula chenyewe. Ilmuradi alipopewa sima na mboga, kwanza alifyeka mboga zote zikaisha. Ndiposa akaanza kubugia sima kavu. Apewapo kuku na chapati hufukamia kuku ikesha ndipo ageukie chapati. Na kila apewapo chakula au kinywaji hula na kunywa na kuondoka bila shukrani wala rabsha. Akipenda kupiga kwata na kusema *marktime* na *about turn,left right* akili zake zilipompeleka miaka ya nyuma huko alipokuwa jeshini. Alipata kutoa simulizi za vituko na visa vya vitani, simulizi ambazo nusu nyingine vifundiro vya akili yake chakaramu (Walibora,2012,uk. 72-73).

Mohamed anatueleza kuhusu Bilal "… kiumbe huyo alimtazama Soud kijichoupembe. Katu hakuwa kiumbe wa kutazama jicho kwa jicho au uso kwa uso siku hizi .Macho yake yalikuwa yameupiga wekundu utadhani pilipili kichaa. Usingizi labda, pondeponde za pombe zisizomtoka kichwani mwilini mwake daima, sumu ya unga au masalio ya haba au yote labda! Alipokaa lile lubega lake lilipanda juu na Soud akasadifu kumwona bamkubwa akining'inia na nanga zake katikati ya kichaka. Mwili wake wote ulikuwa umemwota ukurutu, upele na vidonda. Miundu miembamba kama spoki na miguu imegawana viatu vibovu, wa kulia umevalia maklipa yaliyochanikachanika na kushoto malapa yaliyokatika kanda. Bahasha yake ya matambara na jumla ya vitu anavyoviokota majaani na kwenye mapipa ya taka alikuwa kaiweka chini sasa. Ananuka utadhani fungo!" (Mohamed,2013,uk.241-42).

Wahusika wendawazimu pia wametumiwa kuikejeli hali mbaya ya maisha inayosababishwa na uongozi mbaya.Katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, Matuko anawakejeli wananchi kwa kunyamaza wanapodhulumiwa, anamkejeli Mtemi kwa kuwadhulumu badala ya kuwaongoza kwa haki. Anawakejeli askari kwa kutumiwa kama vyombo vya kuwanyanyasa wananchi. Vivyo hivyo Bilal anaukejeli utawala uliohalalisha ukatili wa askari. Anamkejeli Soud kwa kutomtambua kutokana na hali yake ya wendawazimu. Anauona huu ukiwa unyanyapaa anapomweleza kuwa hakuna anayetaka kumjua shetani. Maana yake ni kuwa wenye wazimu wanaonekana kama watu waosiofaa na waovu katika jamii.

Kupitia urejeshi Bilal anamweleza Soud kuhusu maisha yake ya awali na chanzo za wehu wake. Maelezo yake yanathibitisha jinsi utawala mbaya unaweza kupanda mbegu za udhalimu na ubaguzi wa watu kwa misingi ya kazi zao. Hali hii inaweza kuleta maafa katika nchi na katika maisha ya wananchi kama alivyoathirika Bilal. Ni funzo kwa walio mamlakani kuzingatia na kulinda haki za wote bila ubaguzi.

Kinaya ni mbinu inayotawala riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*.Mtemi anawaongoza wananchi kusherehekea sikukuu ya wazalendo lakini kinyume na matarajio yao, haonyeshi ishara za uzalendo. Anawaamuru askari wamweke ndani Matuko japo anaelewa wazi kuwa Matuko ni mwendawazimu na chanzo cha wazimu wake wanakifahamu kama jamii. Badala ya kuamuru aondolewe tu jukwaani wanampeleka seli na kumtesa kwa kichapo. Anawahutubia

wananchi kwa lugha wasiyoifahamu kama anavyolalamika Bi. Kizee mmoja baada ya kuwalazimisha kuhudhuria sherehe ile (Walibora,2012,uk.70).

Kupitia kwa wahusika Matuko na Bilal, waandishi wa riwaya hizi wametumia mbinu ya balagha. Mbinu hii inawapa wasomaji fursa ya kutafakari zaidi kuhusu maneno wanayoyasema. Kupitia kwa maswali hayo, inadhihirika kuwa wahusika hawa wanaufahamu na kuusema ukweli ambao wahusika wenye akili timamu wanahofia kusema ili kujiepusha na adhabu ya walio katika utawala.

Mazungumzo kati ya wahusika wendawazimu na wengine katika riwaya yanatuwezesha kuwaelewa wahusika hawa kikamilifu. Sifa zao za wehu,uzushi na ujasiri zinajitokeza katika wanayoyasema. Kauli zao zinadhihirisha kuwa wahusika hawa wana nafsi mbili.Kuna baadhi ya kauli zao zinazothibitisha kuwa ni wendawazimu na kunazo zinazowasawiri watu wenye akili timamu.

Ucheshi ni mbinu inayotumiwa kama kipumuo, kupumbaza kupunguza machovu na kama njia ya kukejeli maovu katika jamii. Kwa mfano, Matuko na kina Amani wakiwa katika seli anamweleza Amani kuwa yeye kama rais anaweza kumfanya waziri wa ufisadi na magendo akitaka ikiwa atatoa kitu kidogo. Japo hili linachekesha, linaonyesha jinsi uozo umekithiri katika Sokomoko na nchi ya Tomoko kwa jumla hivi kwamba kupata cheo kulitegemea hongo.

Bilal anapomweleza Soud kuwa bia ni mkojo wa Firauni ambao huacha sumu kichwani mwa aliyeibugia anaongea ukweli, lakini kwa njia ya kuchekesha. Bia huleta madhara mengi ya kiafya. Anapomweleza soud kuwa hawezi mjua

kwa kuwa hakuna anayetaka kumjua shetani ni ishara kuwa anafahamu na kukashifu unyanyapaa uliopo katika jamii yao.

Lengo la tatu ni kuthibitisha ufaafu wa wahusika wendawazimu katika kuendeleza dhamira ya waandishi.Mohamed na Walibora wamewasawiri Bilal na Matuko kama wahusika wendawazimu katika riwaya zao ili kupitia kwa wahusika hawa, waweze kufafanua waziwazi masaibu ya wanyonge katika jamii.Wendawazimu ni miongoni mwa watu wanaokumbana na unyanyapaa katika jamii. Bilal anapomkuta Soud Starehe Club, anagundua kuwa Soud hata hamfahamu. Anachukua fursa hii kumweleza kuwa sababu ya kutomtambua ni kuwa alikuwa mwendawazimu. Hili linaonyesha kuwa mwandishi anaukashifu unyanyapaa dhidi ya wanyonge hasa wendawazimu katika jamii. Kauli ya Mashaka katika sherehe ya Sikukuu ya wazalendo pia inafafanua hali hii. Anapomwona Matuko anauliza, "Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?"(Walibora,2012,uk.69) .

Waandishi hawa pia wanaangazia na kutahadharisha kuhusu athari za uongozi mbaya. Kutokana na utawala mbaya, viongozi wanawagawanya wananchi kwa misingi ya matabaka. Bilal anafafanua kwamba Uanajeshi ulitukuzwa na kazi ya Ualimu ikadharauliwa. Ndiyo maana, kwa vile alikuwa mwalimu, bibi yake Bishara alitwaliwa bila hiari yake na kuozwa Brigadia. Anaeleza kwa uchungu kuwa anawalaumu waliohalalisha udhalimu huu. Haya aliyopitia na kusababisha wehu wake ni matokeo ya uongozi dhalimu.

Walibora amemsawiri Matuko ili kupitia kwake aweze kufafanua waziwazi maonevu ya wanyonge katika hafla ambayo wahusika wanaoonekana wakiwa na akili timamu hawawezi kusema. Anatumia fursa hii kumshambulia Mtemi. Anasema bila woga, "Tumetoshwa. Weye mwananchi mlalahoi huoni, hivyo weye? Tumetoshwa na dhuluma za Bwana Mtemi. Anatudhulumu sana, sana. Anatupokonya mashamba,mali, mabinti na hata wake zetu wenyewe. Weye mwananchi huoni tunavyodhalilishwa. Huoni weye? Umefumba macho tu weye? (Walibora,2012,uk.71)

Mohamed anakejeli namna binadamu anavyojidanganya kwamba amejisitiri kwa kujivika mavazi wakati yuko uchi. Anatukumbusha kuwa binadamu anaweza kuwa uchi na nguo haziwezi kuusetiri uchi wake. Haya hutokea wakati binadamu ametenda mambo ya aibu, udhalimu ambayo humfanya kuwa uchi yaani yanamwaibisha. Anamtumia Bilal kueleza haya kwa nia ya kukashifu matendo maovu katika jamii. "Na je, hapo ulipo upo uchi?... Ungekuwa na jicho la x-rays kama mimi, ungeona watu wote wanatembea uchi, kila siku, kila wakati….''(Mohamed,2013,uk.247).

Vilevile, anakejeli jinsi binadamu wanavyodai kuwa na urazini kwa kueleza kuwa kila mtu ana wazimu wake na hakuna mja aliyekamilika. Maovu wanadamu wanayoyafanya yanadhihirisha kuwa ni wanyama,asili yao ni wanyama na virusi vya unyama vinajidhihirisha kutokana na vitendo vyao vya kikatili. (Mohamed,2012,uk.246)

## 5.3 MCHANGO WA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu imebainika kuwa fasihi ya Kiswahili hususan riwaya inaweza kutumiwa kuangazia nafasi ya wahusika wendawazimu katika jamii ya kisasa. Watunzi wa riwaya teule wamejikita katika nadharia ya uchanganuzi -nafsia kufafanua nafasi ya wahusika wendawazimu katika kazi ya fasihi. Wahusika hawa ni vipaza sauti vya watunzi. Kwa vile mikatale ya kijamii inatukwaza kueleza mambo mengine waziwazi, kazi za fasihi kama zilivyo ndoto kupitia wahusika hufafanua mawazo, imani na mitazamo ya waandishi kuhusu dhana fulani, kama lilivyo jukumu la ndoto kufafanua yaliyo katika sehemu ya ung'amuzi bwete katika fikra za mwandishi.

Wanafunzi wanapopitia kwenye wahusika hawa, wanakumbana na miiko na matakwa ya jamii ambayo yanawafanya wanajamii kuhukumiwa visivyo. Mtazamo wa Rieger unawawezesha kukabiliana na dhana ya wendawazimu katika nyanja mbalimbali kama Uanasheria, Utabibu, maadili na unavyofasiriwa na jamii. Mijadala mingi inayozuka hudhibitisha jinsi tofauti ya wendawazimu na urazini ni ndogo sana. Huwawezesha wanafunzi kuhakiki, kutafakari, kuchunguza, kuajabia na wakati mwingine kupinga dhana fulani katika jamii. Inachunguza matatizo ya Kisaikolojia ambayo chanzo chake ni hali ya mhusika. Inawawezesha wasomi kupata tajriba ya kufafanua maaadili na kutatua matatizo yanayowakumba katika ulimwengu huu changamani.

Sharti watu wazinduke, walizungumzie suala hili lau sivyo watabaki kuwa wafungwa wa mtazamo wa jamii kuhusu wendawazimu huku wakishiriki katika wendawazimu ulio na kila mja unaotufanya sote kutokuwa

razini.(Rieger,1994:125). Anafafanua kuwa uhusiano kati ya fasihi na wendawazimu hutuwezesha kujielewa, kuuelewa ulimwengu kupitia kwa ubunifu (ulimwengu wa kidhahania). Uhusiano huu ukishamiri katika kazi yoyote ya fasihi huiboresha zaidi.

## 5.4 MATATIZO YA UTAFITI

Changamoto zilizoukumba Utafiti huu ni: mtafiti alikumbana na ukosefu wa makala,majarida na vitabu vya lugha ya Kiswahili vilivyoshughulikia utafiti kuhusu dhana ya wahusika wendawazimu katika fasihi ya Kiswahili. Tatizo hili liliweza kukabiliwa kwa kusoma vitabu na makala ya Kingereza, kisha kuyatafsiri kwa Kiswahili na pia kupitia kwa matumizi ya vitabu, makala na maelezo ya mitandao yaliyopatikana kupitia kwa wavuti. Gharama ya karo, kuchapisha na kutoa nakala za pendekezo la utafiti na pia tasnifu ilikuwa juu. Tatizo hili lilitatuliwa kwa kujinyima na kupata mkopo kutoka kwa benki.

## 5.5 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.5.1. MAPENDEKEZO KWA WATAFITI WENGINE

Utafiti huu umeshughulikia nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume.*Tunapendekeza utafiti zaidi kuhusu nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya nyingine na tanzu nyingine za fasihi kama tamthilia na hadithi fupi ufanywe. Utafiti huu umetumia nadharia ya uchanganuzi-nafsia, tunapendekeza utafiti kuhusu suala hili ufanywe kwa kutumia nadharia nyinginezo za Kisaikolojia kama vile Ubwege. Aidha tunapendekeza utafiti zaidi kuhusu wahusika wazee, mayatima na mahabusu katika riwaya za Kiswahili.

Utafiti kuhusu riwaya hizi pia unaweza kufanywa ukiegemea vipengele vingine vya fani na maudhui kwa kutumia nadharia nyingine.

### 5.5.2. MAPENDEKEZO KWA SERIKALI.

Tunapendekeza serikali kuwapa mamlaka viongozi waadilifu na wanaowajibika ambao watahakikisha kuwa kuna utawala wa haki na usawa. Kwa kufanya hivi wataweza kusaidia kukabiliana na hali zinazosababisha matatizo ya kisaikolojia kwa raia. Vilevile tunapendekeza kuandaliwa kwa utaratibu mzuri na utawala wa kuwatibu wendawazimu kwa kuongeza vituo vinavyoshughulikia wagonjwa wa akili na kuboresha zaidi vituo hivi ili kukabiliana vilivyo na tatizo hili. Kwa kufanya hivi, jamii itasaidika kusuluhisha na kuepukana na matatizo ya kisaikolojia.

### 5.5.3. MAPENDEKEZO KWA JAMII.

Jamii ina dhima kubwa ya kujifunza taaluma mbalimbali ikiwemo taaluma ya fasihi. Tunapendekeza kuwa wanajamii wakumbatie utamaduni wa kusoma vitabu kwa bidii ya maksuudi. Utamaduni huu wa kusoma vitabu utasaidia sana kuongeza maarifa na kuwafanya wanajamii hao waweze kufanya yaliyo mema na kuacha yaliyo maovu. Sambamba na hilo tabia ya usomaji wa vitabu ikiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi kama vile riwaya,tamthilia,ushairi,tasnifu na makala mengineyo ya kitaaluma ni nyenzo muhimu katika kuinua upeo wa maarifa na akili kwa maendeleo ya mtu binafsi hadi taifa kwa jumla.

## MAREJELEO

Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University Press.

Adam, O.A. (2014). " Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya ya Kiswahili:Mifano kutoka *Kuli* na *Vuta N'kuvute*."Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu huria Cha Tanzania.

Alembi, E. (2000). *Appreciating Drama*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Ali, J.A.E. (2017). "Kuchunguza Dhamira katika riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed" Tasnifu ya Uzamili, chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Barthes, R. (1975). *An Introduction to the Structural Analysis of Narration Discourse.* Oxford: Blackwell.

Bal, M. (1997) . *Narratology:Introduction to the Theory of Narrative*. (2nd ed.)Toronto: university of Toronto Press.

Bennet, A. & Royale, N.(1999). *Introduction to Literature,Criticism and Theory.* (2nd ed.). England:Prentice Hall.

Buliba, A.*et.al* (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers LtD

Cuddon, J.A. (1979).*The Penguin Dictionary of Literary terms and Literary Theory*. London: Wiley Publishers.

Culler, J.D (1975). *Structuralist Poetics: Structuralism,Linguistics and the Study of Literature.* Newyork:Routledge & Kegan Paul

Darwin, C. (1874). *The Descent of* Man (2nd edition) London:J.Murray.

Debra, (1998). *The Madness of Epic: Reading Insanity from Homer to Statius*. Claredon Press: Oxford.

Devlieger, P.J.(1999). "Frames of Reference in African Proverbs on Disability'' in *International Disability and Education,* 46,439-451.

Encyclopaedia Americana Corporation (1977). *The Encyclopaedia Americana*. New York: Grolier Ltd.

Escandon & Galvez (2016) *Free from Addictions.* (8th ed) Thailand: Editorial Safeliz team.

Freud , S .(1900) *The Interpretation of Dreams.* Norton & Company: Standard Edition

Freud ,S. (1913) *The Interpretation of Dreams.* (3rd edition). England: Macmillan.

Freud, S. (1915) *The Unconsious.* Norton & Company :Standard Edition.

Freud , S (1923) *The Ego and the Id*. Norton & Company :Standard Edition.

Haji , A.V. (2018) Kutathmini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu:* Utafiti Linganishi.Tasnifu ya Uzamili,Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (Haijachapishwa)

Hossain, M.(2017) Global Journal of human Social- Science:G *Linguistics and Education*. Volume 17 Issue1 Version1.0 .

*http://www.academia.edu.pdf. Aspects of the Novel.* E.M.Forster 1879-1980.

Ingstad,B & Whyte, S.R. (1995). *Disability and Culture*. California: University of California Press.

Irwin,M. & Moeller,R.(2010).. 'Seeing Different; Portrayals of Disability in Young Adult Hraphic Novels,' in *School Library Research:American Library Association.*13,1-13.

Jung, C.G.(1990) *The Archetype and the Collective Unconsious*. New York: Princetown University Press.

Kezilahabi,E.(1976) "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (2003) "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi", katika,*Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili* Dar es Salaam:Tuki.3,226-243.

King'ei, K. (2009) "*Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*". Chemchemi. 1, 82-93.

King'ei, K & Amata, J.K. (2001) *Taaluma ya Ushairi*.
Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kombo, D.K & Trump, D.L.A (2006) *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*.Nairobi. Paulines Publication.

Kothari, C.R. (2008) *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi.New Age International Publishing Ltd.

Madumulla, J. S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Mture Education Publishers.

Magare, F. (2002) "Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* kama Kazi ya Kiubwege" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mahochi , E. (1995) "Fani katika Hadithi Fupi" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Egerton. (Haijachapishwa)

Mayieka ,N.M.(2015) "Masuala Ibuka Katika Riwaya za Kisasa: *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi Yangu."* Tasnifu ya Uzamili,Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mbatia ,H.(2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mdee, J. S,*et.al* (2011) (*eds).* Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed. S. A (2013) *Mkamandume*.Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed. S.A (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili:Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi: EAEP.Ltd.

Mlacha, S.A. K (1991) "Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels" katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*.Juz.58,Kur.54-61.Dar es Salaam:Tuki.

Mlacha,S.A.K & Madumulla,(1991). *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Saalam University Press.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EAEP.Ltd.

Mulready, S.(2003). Oedipus the King-Imagery and Humanism, in *Iris: Journal of the Classical association of Victoria,*16 (17)40-45

Mutugu, B.N. (2019). "Taswira za Ulemavu kama Mtindo katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi."Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwangi, J.N. (2022) "Usawiri wa vijana Katika Ujenzi wa Jamii Mpya Katika Riwaya Teule ya Kiswahili" Makala, Chuo kikuu Cha Laikipia.

Ndalu, E. et.al. (2014) *Kamusi Teule ya Kiswahili.* Nairobi: EAEP.Ltd.

Ndungo, C.W & Mwai, W (1991) *Kiswahili Studies Part Two:Misingi ya Nadharia ya Kiswahili*. Nairobi*:* University of Nairobi.

Njogu, K. & Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.*Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njue, P. (2011) *"*Vichekesho vya Machang'i na Kihenjo: Mtazamo wa Sanaa yaUbwege"Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Nyamari ,R .K. (2016) "Mtindo Katika Utenzi wa Katirifu*"* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa)

Ongechi, N.O.& Ruto,S.J.(2002). "Potrayal of Disability Through Personal Naming and Proverbs in Kenya: Evidence from Ekegusii and Nandi",in *Vienna Journal of African Studies,* 3(2),63-83.

Ponera, A.S (2014) *Utangulizi wa Nadhariia ya Fasihi Linganishi.* Dodoma:Karljamer Print Technology.

Rieger, B .M.(1994)(ed) *Dionysus in Literature:Essays on Literary Madness.* Bowling Green State: University Press

Senkoro, F. (1982) *Fasihi.* Dar es salaam: Press and Publication Centre.

Siva,A.(2015) "Tusiwapuuze Walemavu",*Taifa Leo*,Machi19,uk.13

TATAKI,(2014)(3rded) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*East Africa: Oxford University Press.

Thomas , N. (1982) *The Holy Bible,New King James Version.*Wisconsin, The Gideons International

Uraia Trust (2012) *The Constitution of Kenya 2010*. Nairobi: National Council for Law Reporting.

Wade & Tavris (2011) *Psychology.* (10th edition). Pearson.www.pearson.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Waliaura, W.K. (2009). Negotiating local Knowledge 11: Kiswahili and attitude towards disability, in *Disability Studies Quartely*,4(29)

Walibora, K. (2012) *Kidagaa Kimemwozea* . Nairobi: Target Publication.

Wamitila ,K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila ,K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.

Wright, P.(2006). *A Language of the Body; Images of disability in the Works of D.H. Lawrence.* Washington:Washington State University.

www.swahili.com/Blogu-na-ukumbi/Hugholinkimaro.Thursday,Nov.27th,2018.